# ILANI YA CCM KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2015

UMOJA NI USHINDI

Imetolewa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Julai 2015


UMOJA NI USHINDI

# ILANI YA CCM KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2015

## Utangulizi

1. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 wa kuwachagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani imeandaliwa ikiwa ni mkataba kati ya CCM na wananchi. Ilani hii imeandikwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Mwelekeo wa Sera za CCM zenye lengo na nia ya kuendelea kuwatumikia wananchi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020).
2. Ilani hii ni tamko maalumu kwa wapiga kura kuhusu nia ya CCM ya kuendelea kushika dola na kuwaongoza Watanzania kwa njia ya kidemokrasia, na hasa kuendelea kudumisha amani, umoja wa Kitaifa, usawa, ustawi wa wananchi, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa kipindi kingine cha miaka mitano.
3. Nia na uwezo wa CCM wa kuendelea kuongoza Taifa hili unajidhihirisha katika uzoefu ambao tumeupata kwa miaka 38 tangu kuanzishwa kwake na kuwa madarakani, ambapo katika kipindi chote hiki kimeiwezesha nchi yetu kupata mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.
4. Katika miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM ikiwa madarakani, itazielekeza Serikali zake kutumia nguvu zake zote kuendelea kupambana na changamoto kubwa nne:- **Kwanza** kuondoa umaskini; **pili** kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana; **tatu** kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; na **nne** kuendelea kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi na mali zao.

## Kupambana na Umasikini

5. Pamoja na mafanikio ya kukua kwa uchumi na ongezeko la huduma za kijamii yaliyopatikana katika kipindi hiki, bado ipo changamoto kubwa ya umasikini wa kipato na usio wa kipato. Takwimu zinaonesha kwamba asilimia 28.2 ya Watanzania ni masikini. Wengi wa wananchi hao wanaishi vijijini (asilimia 75) na wanategemea kilimo katika maisha yao.

Wapo pia wananchi masikini wanaoishi mijini ambao wanaendesha maisha yao kupitia shughuli za biashara ndogo ndogo zisizo rasmi.

6. Katika kupambana na changamoto hii, CCM itazielekeza Serikali zake kuboresha maisha ya wananchi wote na hususan wa vijijini, kwa kuchukua hatua zifuatazo:-
   (a) Kuhamasisha kilimo kupitia kauli mbiu ya **Kilimo Kwanza** kwa kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa, pembejeo, zana za kisasa na wataalamu wa ugani pamoja na mbinu za kuyafikia masoko ya uhakika ya mazao yao;
   (b) Kuongeza kasi ya kupima ardhi yao na kuwapatia hati miliki za kimila ambazo watazitumia kama dhamana ya kuwawezesha kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zao za kilimo, ufugaji na uvuvi;
   (c) Kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji, umeme na ujenzi wa nyumba bora; na
   (d) Kuongeza kasi ya kurasimisha biashara na kuwapatia wafanyabiashara wadogo maeneo ya kufanyia biashara, leseni na fursa za kupata mikopo yenye masharti nafuu.

7. Mafanikio ya utekelezaji wa masuala haya yote kwa pamoja yanatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo mijini na vijinini, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa hali ya umasikini nchini.

**Ajira kwa Vijana**

8. Suala la ukosefu wa ajira kwa vijana ni moja ya changamoto zinazolikabili Taifa letu na dunia yote kwa ujumla. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yapo mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza ajira. Hata hivyo, mafanikio katika upanuzi wa elimu ya Sekondari na Vyuo yameongeza mahitaji ya ajira ya vijana wasomi kila mwaka ikilinganishwa na nafasi zinazokuwepo.

9. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo jitihada za kulipatia ufumbuzi tatizo la ajira nchini zitaendelezwa. Kipaumbele kitakuwa katika kukuza na kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vilivyo na uwezo wa kuajiri watu wengi na vyenye kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi wa ndani ya nchi na zile za kuuza nchi za nje. Aidha, kwa upande

wa Tanzania Zanzibar, mikakati ya kuongeza ajira kwa vijana itazingatia mazingira maalamu ya fursa za uchumi wa visiwa.

10. Katika kipindi cha 2015-2020, sekta za uzalishaji mali kama kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda vikubwa na vidogo na huduma za kiuchumi kama vile miundombinu ya nishati, uchukuzi na ujenzi zitaelekeza mipango yao katika kupunguza umasikini na kuanzisha ajira hususan kwa vijana. Aidha, huduma za jamii za elimu, afya na maji zitajielekeza kusaidia kuondoa umasikini na kuongeza ajira.

**Vita dhidi ya Rushwa**

11. Jitihada za kuinua uchumi na kuongeza huduma za jamii hazitaleta manufaa kwa wananchi na kuondoa umasikini iwapo adui rushwa ataendelea kulitafuna Taifa letu. Rushwa ni adui wa haki pia ni adui wa maendeleo na ustawi wa wananchi, hivyo ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili nchi yetu na dunia kwa ujumla.

12. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itazielekeza Serikali zake kuendeleza mapambano dhidi ya adui rushwa kwa nguvu zake zote na kuendelea kuziba mianya ya rushwa katika taasisi za umma; kuchukua hatua kali na za haraka kwa wale wote watakaobainika kuendeleza rushwa Serikalini na katika sekta binafsi; na kuimarisha vyombo na taasisi zinazohusika na kuzuia na kupambana na rushwa; ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mahakama Maalumu kwa ajili ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

13. Sambamba na kupambana na tatizo la rushwa, Serikali pia zitatakiwa kushughulikia kwa ukali zaidi tatizo la ubadhirifu na wizi wa mali ya umma, matumizi mabaya ya madaraka, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na utumishi wa umma, kuchelewesha kutoa maamuzi yenye maslahi kwa umma na kusimamia uwajibikaji katika kutekeleza masuala yenye maslahi kwa umma.

**Ulinzi na Usalama**

14. Nchi yetu imepata mafanikio makubwa ya kuwa na amani na utulivu tangu tupate uhuru mwaka 1961 na Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Imekuwa kimbilio la watu wa Mataifa ya jirani kila wapatapo matatizo ya uvunjifu wa amani katika nchi zao. Hata hivyo, siku za karibuni vimeanza kuonekana viashiria vinavyoleta hofu ya usalama wa

wananchi, hasa vitendo vya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino), kuuawa kwa vikongwe, ukatili dhidi ya wanawake na watoto na tishio la vitendo vyenye mwelekeo wa kigaidi.

15. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itazielekeza Serikali zake kuendelea kuimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea raslimali fedha, raslimali watu, maslahi, zana za kisasa na mafunzo. Aidha, elimu kwa umma itatolewa ili kukomesha imani potofu za kishirikina zinazosababisha mauaji ya albino na vikongwe na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya mauaji ya makundi hayo.

**Utekelezaji wa Ilani**

16. Kazi kubwa ya Serikali za CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo itakuwa ni kuendeleza mapambano dhidi ya umasikini, ukosefu wa ajira, rushwa; na kudumisha umoja, amani, ulinzi na usalama. Ili kutimiza azma hiyo, CCM itazielekeza Serikali zake zisiwe kubwa, zenye watumishi weledi, waadilifu na wawajibikaji. Serikali zisizo na urasimu unaokwamisha na kuchelewesha maamuzi na utekelezaji. Serikali zitakazongeza maradufu au hata zaidi ukusanyaji wa mapato yake ili zijitegemee kadri inavyowezekana kwenye bajeti zake.

17. Vile vile katika kipindi cha Ilani hii, Chama Cha Mapinduzi kitaziagiza Serikali zake kuendeleza na kuimarisha mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN na BRP) katika kutekeleza Ilani na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kipaumbele unaozingatia nidhamu ya utekelezaji katika muda uliopangwa, ufuatiliaji makini na wa kina, pamoja na kupata ufumbuzi wa vikwazo na changamoto za utekelezaji.

# SURA YA KWANZA
# HALI YA UCHUMI - MWAKA 2010 – 2015
# NA MALENGO YA MWAKA 2015 – 2020

18. Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010–2015, ililenga katika kutekeleza kipindi cha kwanza cha Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010–2020 na kutekelezwa katika kipindi cha pili na cha mwisho cha Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kipindi hiki, Serikali imetekeleza kwa mafanikio makubwa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010–2020 kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Malengo ya Milenia. Aidha, kutokana na mafanikio hayo, Serikali imeweza kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Hali ya Uchumi**

19. Katika kipindi hiki, Serikali imeweza kutekeleza mipango yake kwa ufanisi mkubwa licha ya changamoto zilizokuwa zikijitokeza na kuleta mafanikio ya kiuchumi yafuatayo:-
    (a) Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, umekua kwa wastani wa asilimia 7 kwa mwaka;
    (b) Ukusanyaji wa mapato ya ndani umeongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 390 kwa mwezi mwaka 2010 na kufikia wastani wa Shilingi bilioni 850 kwa mwezi, mwaka 2014/15;
    (c) Misaada na mikopo ya Washirika wa Maendeleo kwenye bajeti ya Serikali imepungua kutoka asilimia 42 mwaka 2005 hadi asilimia 8 mwaka 2015/2016;
    (d) Mapato ya kodi yameongezeka kutoka Shilingi trilioni 5.74 mwaka 2010/11 na kufikia shilingi trilioni 7.42 mwaka 2014/15;
    (e) Mfumko wa bei umeendelea kubakia tarakimu moja (single digit) na umepungua kutoka wastani wa asilimia 19.8 Desemba, 2011 hadi kufikia asilimia 4.8 Desemba, 2014 na asilimia 4.3 Machi, 2015.

(f) Bajeti ya Serikali imeongezeka kutoka Shilingi trilioni 4.18 mwaka 2010/2011 hadi Shilingi trilioni 22.49 mwaka 2015/2016; na

(g) Wastani wa pato kwa kila mwananchi limeongezeka kutoka Shilingi 770,000 mwaka 2010 hadi wastani wa Shilingi 1,675,232 mwaka 2014.

20. **Sekta ya Fedha ndio kipimo kinachoweza kuonesha viwango vya uchumi wa nchi vilivyofikiwa katika vigezo mbalimbali kama vile Pato la Taifa, Ukuaji wa Uchumi na Mfumko wa Bei. Maendeleo ya haraka katika nyanja hizo yatategemea uimara na uwezeshaji wa sekta ya fedha.**

**Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo na kuhakikisha kwamba:-**

(a) Uchumi unaendelea kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 8 au zaidi na kuinua ustawi wa Watanzania kwa kuongeza mapato ya wananchi kufikia kiwango cha wastani wa nchi ya uchumi wa kati na hivyo, kuongeza fursa za ajira na kupunguza umasikini; na

(b) Kunakuwepo utulivu wa uchumi jumla ambao ni endelevu (sustainable macroeconomic stability) kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kudhibiti mfumko wa bei ili uendelee kubaki kwenye tarakimu moja na hivyo kuzuia kasi ya kupanda kwa gharama za maisha;

(ii) Kudhibiti nakisi ya bajeti ili iendelee kushuka na kufikia kiwango kisichozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa ili pamoja na mambo mengine, Tanzania iendelee kuwa kivutio kwa wawekezaji na kupunguza gharama za kukopa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu;

(iii) Kusimamia Deni la Taifa liendelee kuwa himilivu ili lisiwe mzigo kwa uchumi wetu bali liendelee kuwa fursa na kichocheo cha maendeleo ya nchi yetu;

(iv) Kuhakikisha thamani ya Shilingi yetu inatengamaa ili kujenga imani ya uchumi wetu kwa lengo la kuongeza shughuli za uwekezaji, uzalishaji na biashara;

(v) Kuongeza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni na kuepuka kuagiza bidhaa zisizo za lazima kutoka nje ya nchi; na

(vi) Kuendelea kuwa na mikakati itakayowezesha kuwa na akiba ya fedha za kigeni zinazotosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje bila ya matatizo.

(c) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza vyanzo vipya vya mapato na kupanua wigo wa walipa kodi ili kuongeza uwezo wa Serikali wa kugharimia huduma za kijamii na kiuchumi;

(d) Kusimamia kwa ufanisi matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo ya ununuzi wa umma, ukaguzi na kusimamia mali za Serikali ili Watanzania wote wanufaike na rasilimali zilizopo; na

(e) Kuimarisha Sekta ya Fedha kwa kuhakikisha wananchi wananufaika kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kupanua huduma za fedha hadi vijijini kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi;

(ii) Kuhamasisha wananchi wajiunge na huduma za Bima ya Afya, Bima ya Maisha na Mifuko ya Hifadhi za Jamii ili kujihakikishia kinga dhidi ya majanga na maisha ya uzeeni na baada ya kustaafu; na

(iii) Kuweka mazingira yatakayowezesha kushuka kwa riba ya mikopo katika Taasisi za Fedha ili kutoa fursa kwa wananchi kupata mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa riba nafuu.

(f) Kutekeleza Sera na Sheria za kusimamia mapato yanayotokana na gesi asilia na mafuta ili kuhakikisha fedha zinatumika kwa manufaa ya Wananchi wa kizazi hiki na kijacho;

(g) Kuwawezesha wananchi kumiliki na kuwekeza kwenye soko la mitaji na dhamana kwa:-

(i) Kuongeza ufanisi wa shughuli za minada kwa njia ya simu na mtandao wa intaneti;

(ii) Kuelimisha umma kuhusu fursa za kujiongezea kipato kupitia masoko ya mitaji na uwekezaji; na

(iii) Kuendelea kutoa fursa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili waweze kunufaika na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kupitia dirisha maalumu la kukuza na kuimarisha masoko ya wajasiriamali wadogo na wa kati.

(h) Kuboresha mfumo wa kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa manufaa ya pande zote mbili za Muungano kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha asasi zinazohusika na masuala ya uhusiano wa kifedha kati ya SMT na SMZ;

(ii) Kukamilisha hatua za kuanzisha Akaunti ya Fedha ya pamoja ili kuzidi kuimarisha mshikamano na maelewano; na

(iii) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuweka utaratibu wa kuoanisha viwango vya kodi ya forodha kati ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano.

# SURA YA PILI
# MAFANIKIO NA MALENGO YA SEKTA ZA UZALISHAJI

## Kilimo na Ushirika

21. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Chama Cha Mapinduzi kiliweka kipaumbele cha kuhakikisha kuwa kilimo nchini kinakuwa endelevu na chenye tija ili kuliwezesha Taifa kujitosheleza kwa chakula; kuongeza mapato ya wakulima; kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi ya sekta ya viwanda; na kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi. Kwa kutekeleza azma hiyo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

   (a) Bajeti ya Sekta ya kilimo imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 903.8 mwaka 2010/11 hadi Shilingi trilioni 1.08 mwaka 2014/15;

   (b) Dirisha la kilimo limeanzishwa katika Benki ya Rasilimali (TIB) kwa lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima ili waweze kununua pembejeo na zana za kilimo. Aidha, imeanzishwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo mahususi kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima;

   (c) Katika kuimarisha huduma za ugani, udahili katika vyuo vya kilimo umeongezeka kutoka wanafunzi 1,246 mwaka 2010/11 hadi 2,500 mwaka 2013/14. Aidha, idadi ya maafisa ugani katika ngazi ya Vijiji na Kata imeongezeka kutoka 5,184 mwaka 2010/11 hadi 9,558 mwaka 2013/14;

   (d) Uzalishaji na usambazaji wa pembejeo bora za kilimo umeimarishwa ambapo:-

      (i) Uzalishaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 10,477.17 mwaka 2005 hadi tani 32,340 mwaka 2014; usambazaji umeongezeka kutoka tani 16,148.2 mwaka 2009/2010 hadi tani 35,352 mwaka 2013/14; na

      (ii) Usambazaji wa mbolea umeongezeka kutoka tani 302,200 mwaka 2009/2010 hadi tani 343,687 mwaka 2013/14.

   (e) Matumizi ya matrekta madogo na makubwa yameongezeka kutoka 11,223 mwaka 2010/11 hadi 16,412 mwaka 2013/14.

Ongezeko hili limechangia kuongozeka kwa eneo linalolimwa kwa matrekta kutoka asilimia 12 mwaka 2010/11 hadi asilimia 14 mwaka 2013/14;

(f) Ruzuku ya mbolea na pembejeo imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 7.5 mwaka 2005/06 hadi Shilingi bilioni 299.3 mwaka 2014;

(g) Kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula kimeendelea kuongezeka kutoka tani milioni 12.83 mwaka 2009/10 hadi tani milioni 16.01 mwaka 2014/15. Kwa ongezeko hilo Taifa limeweza kujitosheleza kwa chakula;

(h) Katika juhudi za kuhifadhi mazao kwa ubora unaostahili, jumla ya maghala 30 yenye uwezo wa kuhifadhi kati ya tani 5,000 hadi 10,000 yamekarabatiwa. Aidha, ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 umekamilika katika Wilaya ya Songea mwaka 2013/14 chini ya mpango wa SAGCOT;

(i) Hatua za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo cha mboga mboga na matunda zimechukuliwa kwa kujenga Maeneo ya Hifadhi ya Mazao (Packhouse and refeer container) katika Wilaya za Lushoto na Korogwe. Aidha, mashine za kusindika na kusafisha mafuta ya alizeti zimesambazwa kwa vikundi vya wazalishaji na wasindikaji wadogo katika mikoa inayolima alizeti nchini;

(j) Mchakato wa kuanzisha Soko la Bidhaa (Commodity Exchange) umeanza na imetungwa Sheria Na. 15 ya Mwaka 2015. Soko hilo litamwezesha mkulima kuwa na uhakika wa kuuza mazao yake na kupata bei nzuri;

(k) Hatua za kuimarisha soko la nafaka zimechukuliwa kwa kuondoa zuio la kuuza nafaka nje ya nchi; kuwezesha Wakala wa Taifa wa Chakula kununua nafaka kutoka kwa wakulima kwa bei ya soko; na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi;

(l) Hatua za kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa lengo la kuondoa migogoro katika maeneo mbalimbali nchini zimeendelea kuchukuliwa kwa kupima na kutoa hati miliki kwa wakulima vijijini; na kwa wawekezaji wakubwa na wadogo. Jitihada hizo zimewezesha upimaji wa jumla ya ekari 444,663.2 za mashamba ya wakulima;

(m) Kilimo cha umwagiliaji kimepewa kipaumbele kwa kupanua eneo la umwagiliaji ambapo Sheria ya Umwagiliaji Na. 5 ya mwaka 2013 imetungwa na kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Aidha, kutokana na utekelezaji wa Sera na Mikakati mbalimbali, kilimo cha umwagiliaji kimechangia asilimia 24 ya mahitaji ya chakula nchini; na

(n) Kwa muda mrefu Sekta ya Ushirika ilikabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zilidumaza jitihada za kuendeleza ushirika. Ili kuondokana na changamoto hizo, Sheria ya Vyama vya Ushirika ilifanyiwa mabadiliko na kuanzisha Sheria mpya (Sheria Na. 6 ya mwaka 2013) ambayo imeanzisha Tume Huru ya Maendeleo ya Ushirika.



*Kilimo cha Umwagiliaji kinachotumia zana bora kitaongeza tija kwa wakulima ambao ndio wengi nchini.*

22. **Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kutilia mkazo utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Kilimo *(Agricultural Sector***

***Development Programme – ASDP II)* pamoja na miradi ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ili kufikia malengo makuu ya kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara; chenye tija na ambacho mazao yake yatakuwa yameongezewa thamani. Lengo ni kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza kwa chakula; kuimarisha uchumi; kuongeza kipato cha wakulima; kuwa kichocheo cha kukua kwa viwanda; na kuongeza ajira kwa kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa hususan katika kuboresha mifumo ya utoaji wa ruzuku na pembejeo pamoja na kuwaunganisha wakulima na Benki ya Maendeleo ya Kilimo na taasisi nyingine za fedha;

(b) Kutoa elimu kwa wakulima juu ya kanuni bora za kilimo kwa kuongeza idadi ya maafisa ugani kutoka 9,558 waliopo sasa hadi kufikia 15,082 mwaka 2020; na kuanzisha Vituo vya Mafunzo ya Kilimo na Mifugo katika kila Kata nchini; na

(c) Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua kwa kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 461,326 mwaka 2014 hadi 1,000,000 mwaka 2020. Ili kufanikisha hilo, Serikali itafanya mambo yafuatayo:-

    (i) Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji kwa kujenga mifereji mikuu, mifereji ya kati na kujenga mabwawa ya kuhifadhia maji kwenye maeneo yenye ukame;

    (ii) Kuhamasisha wakulima kupitia vyama vyao vya umwagiliaji kuchangia katika ujenzi wa mifereji midogo ya kuingiza maji mashambani na kushiriki katika kutunza mifereji hiyo;

    (iii) Kuwafundisha kulima kwa tija na ufanisi kwa kutumia miundombinu iliyopo ikiwa ni pamoja na kulima zaidi ya mara moja kwa mwaka;

    (iv) Kukamilisha ujenzi wa skimu zote za umwagiliaji zilizoanza kujengwa miaka ya nyuma;

(v) Kujenga, kukarabati na kuboresha skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo na wa kati ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi bora ya rasilimali maji;
(vi) Kujenga na kuimarisha mabwawa ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji wa kilimo cha mpunga;
(vii) Kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji; na
(viii) Kuijengea uwezo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iongeze kasi ya ujenzi wa miundombinu.

(d) Kuboresha mfumo wa utafiti wa kilimo nchini ili matokeo ya tafiti hizo yawafikie wakulima kwa kufanya yafuatayo:-
(i) Kugundua na kutathmini aina za mbegu bora za mazao mbalimbali zenye sifa ya kutoa mavuno mengi, zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi na zenye viinilishe vingi;
(ii) Kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali kwa kushirikiana na taasisi za umma na binafsi ili kutosheleza mahitaji ya uzalishaji wa mbegu bora nchini;
(iii) Kutafiti magonjwa na visumbufu vya mimea vinavyoathiri mazao hasa migomba, mihogo, minazi, mahindi, mpunga, mboga na matunda ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao nchini;
(iv) Kuchambua mifumo ya kilimo, kutoa teknolojia za kurutubisha udongo na matumizi bora ya mbolea na kuandaa ramani za ikolojia kwa kila Kanda; na
(v) Kuboresha miundombinu ya utafiti na kuwajengea uwezo watafiti ili kuongeza ufanisi wa utafiti nchini.

(e) Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa kuendelea kupima mashamba ya wakulima na kutoa hati miliki za kimila kwa wakulima wadogo kwa lengo la kuondoa migogoro ya ardhi na kutumia hati hizo kama dhamana ya kupata mikopo; na

(f) Kuwawezesha wakulima hususan vijana na wanawake kujishughulisha katika kilimo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuainisha na kupima maeneo ya ardhi ya kilimo ili kuwawezesha wakulima kujiajiri katika sekta ya kilimo hususan kilimo cha mazao ya mboga mboga, matunda, maua, mbegu za mafuta na nafaka;
(ii) Kuendelea kupima maeneo na kuyapatia hati miliki ili kuwawezesha wakulima kushiriki katika kuyaendeleza maeneo hayo kwa kutumia hati miliki kama dhamana ya kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha;
(iii) Kuwaunganisha wakulima (Vijana na wanawake) na asasi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya pembejeo, zana bora na mashine za usindikaji kupitia vyama vyao vya ushirika na vikundi vya uzalishaji mali; na
(iv) Kuimarisha matumizi ya teknolojia zitakazorahisisha kazi ili kuwapunguzia harubu wanawake na vijana katika kilimo.

(g) Kuwezesha upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa kufanya yafuatayo:-
(i) Kushirikisha sekta binafsi kujenga miundombinu ya masoko na maghala bora ya kuhifadhia mazao mbalimbali hususan vijijini kwa kutoa elimu na kuondoa vikwazo vya utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani;
(ii) Kuanzisha Soko la Bidhaa kwa mujibu wa Sheria ya Soko la Bidhaa (Commodity Exchange Act) Namba 15 ya mwaka 2015;
(iii) Kujenga masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuwapa wakulima fursa ya kuuza mazao yao nje ya nchi;
(iv) Kuviimarisha na kuviwezesha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ya ndani na nje kwa kuweka mfumo madhubuti wa ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na biashara.

(h) Kuhamasisha sekta binafsi na vyama vya ushirika wa mazao kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hususan kwenye maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo kwa lengo la

kuongeza thamani na kuongeza ajira. Aidha, kuwawezesha wakulima kupata majokofu ili kuhifadhi matunda na mazao ya mboga mboga yanayoharibika haraka pamoja na vifungashio.

**Mifugo na Uvuvi**

23. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Sekta ya Mifugo na Uvuvi imeimarishwa ili kuwaongezea wafugaji na wavuvi kipato pamoja na kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa.

**Mifugo**

24. Katika kipindi hicho, Sekta ya Mifugo imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Mashamba matano yenye uwezo wa kuzalisha mitamba 5,000 kwa mwaka yameanzishwa. Aidha, Kituo cha Uhamilishaji cha NAIC kilichopo Arusha kimeimarishwa na kinazalisha mbegu bora za mifugo. Vituo vipya vya Uhamilishaji vimeanzishwa katika Mikoa ya Pwani, Dodoma, Mbeya, Katavi, Lindi na Mwanza. Sekta binafsi imezalisha mitamba 10,000 mwaka 2013/14 na kusambazwa kwa wafugaji;

(b) Ruzuku ya dawa za kuogeshea mifugo imetolewa ambapo lita 252,138 za dawa zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.2 zimenunuliwa na kusambazwa katika Mikoa yote nchini;

(c) Ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Mifugo vya Mabuki, Kikulula na Rorya umefanyika na kuwezesha mafunzo kwa wafugaji 2,000 pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Mifugo 2,000 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada;

(d) Dozi milioni 7.1 za Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, dozi 900 za chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa (RVF) na dozi milioni 12.8 za chanjo ya Sotoka zimenunuliwa na kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini;

(e) Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (ZVC) kimefunguliwa huko Sumbawanga kwa ajili ya kuhudumia Eneo Huru la Magonjwa; na

(f) Jumla ya wataalamu 900 wamesajiliwa ikiwa ni pamoja na kusajili vituo vya kutolea huduma za mifugo. Aidha, leseni 290 za

Wakaguzi wa Nyama, Wahamilishaji na Watalaamu wa Maabara za Mifugo zimetolewa.



*Ufugaji bora wenye tija kwa wafugaji ambao pia hupunguza uharibifu wa mazingira.*

25. **Katika kipindi cha Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali yake kuiendeleza Sekta ya Mifugo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) Kuongeza uzalishaji wa mitamba kwenye mashamba inakozalishwa na kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kuendelea kuzalisha mitamba ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa;

(b) Kutenga, kupima na kumilikisha wafugaji maeneo ya ufugaji nchini ili kuongeza maeneo ya ufugaji yaliyopimwa kutoka hekta milioni 1.4 za sasa hadi hekta milioni 5.0 mwaka 2020;

(c) Kujenga miundombinu ya mifugo kwa kuongeza idadi ya malambo kutoka 1,378 yaliyopo sasa hadi 2,000; na kujenga mabwawa katika mikoa yenye mifugo mingi. Aidha, vitajengwa visima virefu 300, majosho 50 na kuanzisha minada 164 ya mifugo katika maeneo yote yatakayotengwa kwa ajili ya ufugaji ili kuzuia kuhamahama kwa wafugaji kunakosababisha migogoro;

(d) Kutoa dhamana kwa vikundi vya wafugaji ili kupata mikopo kwenye asasi za fedha, hususan vijana na wanawake watakaokuwa kwenye vyama vya ushirika vya ufugaji wa ng'ombe, kuku, mbuzi na uzalishaji malisho pamoja na usindikaji wa mazao ya mifugo (nyama, maziwa na ngozi);

(e) Kuanzisha mashamba darasa ya malisho katika kila Halmashauri ya Wilaya ili wafugaji wa asili wajifunze jinsi ya kuboresha na kuhifadhi malisho (feed banks) hususan wakati wa kiangazi na ukame;

(f) Kueneza ufugaji wa mifugo bora kupitia mikopo ya mifugo kwa wafugaji watakaojiunga katika vikundi kupitia miradi ya kopa ng'ombe/mbuzi lipa ng'ombe/mbuzi au kopa ng'ombe/mbuzi lipa maziwa;

(g) Kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji wanaomiliki na watakaomilikishwa ardhi ili kutumia hati zao kama dhamana ya kupata mikopo kutoka asasi za fedha;

(h) Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya teknolojia ya uhamilishaji katika kuboresha koosafu za mifugo nchini kwa kutoa huduma za uhamilishaji kwa wafugaji kwa gharama nafuu kupitia ruzuku itakayowekwa katika mbegu za uhamilishaji;

(i) Kuboresha huduma za uhamilishaji kwa kuimarisha vituo vya uhamilishaji vya Taifa vya NAIC- Usa River (Arusha) na Sao Hill (Iringa); na vituo vya Kanda vya Kibaha (Mashariki), Lindi (Kusini), Mbeya (Nyanda za Juu Kusini), Dodoma (Kati), Mwanza (Ziwa) na Mpanda (Kusini Magharibi) ili kusogeza karibu huduma ya uhamilishaji kwa wafugaji na kujenga vituo vipya vya uhamilishaji vya Kanda vya Tabora (Magharibi) na Tanga (Mashariki);

(j) Kuendelea kukuza na kuendeleza masoko ya mifugo na mazao yake yanayozalishwa na wafugaji na kujenga viwanda viwili (2) vya ngozi katika mikoa ya Singida na Dodoma;

(k) Kuendelea kutoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo kiasi cha lita milioni 1.0 ili kuhakikisha kuwa majosho 2,428 yaliyopo nchini yanatumika kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo hususan ugonjwa hatari wa Ndigana kali. Aidha, Serikali itatoa ruzuku ya Chanjo ya Ndigana kali (ECF) na kushirikisha sekta binafsi na wadau wengine kufufua majosho 150 na kujenga majosho mapya 200 katika mikoa yenye mifugo mingi;

(l) Kuendelea kununua na kutoa chanjo za magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya mifugo na binadamu na kuwezesha biashara ya mifugo katika soko la kimataifa, hususan Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Bonde la Ufa (RVF) na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR);

(m) Kuendelea kuimarisha eneo huru la magonjwa ya mifugo katika Kanda ya Kusini Magharibi na kuanzisha vitalu huru vipya viwili (2) vya magonjwa katika ranchi za Kongwa na Ruvu ili kukidhi matakwa ya soko la kimataifa hivyo kuongeza ajira na Pato la Taifa; na kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake;

(n) Kuendelea kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo katika kituo cha Uzalishaji wa chanjo cha Kibaha (Tanzania Vaccine Institute);

(o) Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo kwa kuongeza udahili wa maafisa ugani kutoka 1,800 hadi 2,500 kwa mwaka katika vyuo vinane (8) vya Serikali na kushirikisha vyuo 21 vya sekta binafsi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maafisa ugani katika ngazi za vijiji na Kata ili kuimarisha huduma za mifugo;

(p) Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya nyama na mazao mengine yatokanayo na mifugo ikiwemo jibini na ngozi hususan katika maeneo yenye mifugo mingi ili kuongeza thamani; na

(q) Kuitafutia ufumbuzi wa kudumu migogoro ya wakulima na wafugaji.

**Uvuvi**

26. Kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo na wingi wa rasilimali za uvuvi tulizonazo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Usimamizi wa rasilimali za uvuvi Tanzania Bara umeimarishwa ambapo vituo 25 vya doria vimeanzishwa na kupewa zana za kisasa kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali nchini;

(b) Vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi 226 vimeanzishwa na kufanya idadi ya vikundi hivyo kufikia 749, kati ya hivyo 511 vimesajiliwa na vinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria ndogo ya mipango kazi yake;

(c) Ujenzi na uboreshaji wa mialo ya kisasa ya kupokelea mazao ya uvuvi umetekelezwa katika Kanda ya Pwani ya Bahari ya Hindi (3), Ziwa Tanganyika (4) na Ziwa Victoria (6). Aidha, mialo 19 ya ukanda wa Ziwa Victoria imekarabatiwa;

(d) Vituo vya kuzalisha vifaranga wa samaki wa maji baridi vimeanzishwa katika Mikoa ya Lindi, Kigoma, Ruvuma, Tanga, Pwani, Geita na Morogoro. Vituo hivyo kwa ujumla vina uwezo wa kuzalisha vifaranga 10,000,000 kwa mwaka;

(e) Sekta binafsi imeendelea kuhamasishwa kushiriki katika uvuvi ikiwemo kuanzisha viwanda vya kuchakata samaki. Hadi sasa kuna viwanda 48 vya kuchakata samaki na maghala 84 ya kuhifadhia mazao ya uvuvi; na

(f) Jumla ya vikundi 208 vya Kuweka na Kukopa (VICOBA) vimeanzishwa ambapo wananchi 5,573 wamenufaika na hivyo kuwawezesha kuendesha shughuli ndogo ndogo za uvuvi.

27. **Katika kipindi cha Ilani hii ya 2015–2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuiendeleza Sekta ya Uvuvi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi wadogo wadogo kwa lengo la kuwakopesha

vifaa vikiwemo zana za uvuvi katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, maziwa na mito kwa kupunguza kodi na kuviwezesha vikundi hivyo vikopesheke;

(b) Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Vyama vya Ushirika itanunua meli tano za uvuvi zenye uwezo wa kuvua samaki Bahari Kuu ambapo ajira zaidi ya 15,000 kwa mwaka zitapatikana;

(c) Kujenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli zinazovua Bahari Kuu kutia nanga kwa lengo la kuhaulisha samaki, kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine. Zaidi ya ajira 30,000 zitapatikana na kuongeza pato kwa jamii na Taifa;

(d) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo mitatu (Ziwa Victoria), minne (Ziwa Tanganyika) na miwili (Ziwa Nyasa) na hivyo kuongeza idadi ya mialo kutoka 39 hadi 48 na kuimarisha masoko ya samaki ya Feri (Dar es Salaam), Kirumba (Mwanza) na Muganza (Kagera) ili kuongeza thamani na ubora wa samaki pamoja na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kabla ya kumfikia mtumiaji;

(e) Kuimarisha hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu 18 pamoja na kuanzisha maeneo mengine sita (6) na hifadhi katika maziwa makuu, hususan Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kuhakikisha kuwa mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika yanarejeshwa katika hali yake ya awali;

(f) Kurejesha mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa kuweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari;

(g) Kushirikiana na Mashirika ya Umma yenye dhamana ya uvuvi nchini, kuwavutia wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, vyombo na zana za uvuvi;

(h) Kuboresha maeneo ya uvuvi kwa kutumia teknolojia rafiki ya mazingira kwa kuweka vifaa vya kuvutia samaki (Fish

Aggregating Devices) baharini ili kuwawezesha wavuvi wadogo kuyafikia maeneo yenye samaki wengi na hivyo kuongeza upatikanaji wa samaki;

(i) Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo kwa kuongeza udahili wa maafisa ugani wa uvuvi kutoka 1,200 hadi 2,500 kwa mwaka na kuwezesha upatikanaji wa Maafisa Ugani katika ngazi ya Kata ili kuimarisha huduma za uvuvi na ufugaji wa samaki;

(j) Kuendeleza utafiti wa kurudishia samaki na kupandikiza samaki ili kuongeza wingi katika maziwa, mito na mabwawa, hususan Ziwa Victoria;

(k) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji wa samaki kwa lengo la kukuza ufugaji wa samaki nchini;

(l) Kushirikiana na wadau wa ufugaji samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kujenga mabwawa ya kufugia samaki na kuongeza uzalishaji kutoka tani 10,000 hadi 50,000 kwa mwaka na kupanua wigo wa ajira kwa vijana;

(m) Kuwawezesha wakulima wa mwani, hususan vikundi vya akina mama na vijana wa mwambao wa pwani katika kuongeza uzalishaji kutoka tani 12,000 hadi tani 20,000 kwa mwaka, uzalishaji wa chaza wa lulu, kaa, kamba na viumbe wengine wa baharini kwa kuwapatia nyenzo na utaalamu;

(n) Kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kupata vifaa vya uvuvi kwa bei nafuu;

(o) Kuhamasisha uchimbaji wa mabwawa na ufugaji wa samaki katika maeneo yenye ukame kwa lengo la kuongeza lishe bora pamoja na kuongeza ajira kwa vijana; na

(p) Kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija.

## Utalii

28. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba Sekta ya Utalii inaimarishwa na kuendelezwa kwa

kuwa ni moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa na ajira kwa wananchi. Katika kipindi hicho, mambo yafuatayo yamefanyika:-

(a) Ujenzi wa Chuo Kipya cha Utalii, Kampasi ya Bustani umekamilika mwaka 2011 na kuwezesha idadi ya udahili wa wanafunzi kuongezeka kutoka 138 mwaka 2005 hadi wanafunzi 289 mwaka 2014. Ili kuongeza wataalam wa fani hii, Serikali imeruhusu taasisi binafsi na wakala kutoa mafunzo ya utalii na ukarimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada;

(b) Tanzania imefanikiwa kuviingiza vivutio vya utalii kwenye soko la Kimataifa ambavyo ni Mlima Kilimanjaro, Mbuga ya Serengeti na Bonde la Hifadhi la Ngorongoro kuwa kati ya Maajabu Saba ya Asili ya Afrika (*New Wonders of Africa*); na

(c) Makusanyo yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka wastani wa Shilingi trilioni 2.98 mwaka 2012/13 hadi Shilingi trilioni 3.94 mwaka 2013/14.

29. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitasimamia utekelezaji wa mikakati ya kukuza utalii nchini kwa kuhakikisha kwamba, Serikali inatekeleza mambo yafuatayo:-**

(a) Kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini kutoka 1,102,026 mwaka 2015 hadi 2,000,000 mwaka 2020 kwa kuwezesha Sekta Binafsi kuwekeza katika huduma za miundombinu ya utalii pamoja na kuendeleza Mkakati wa Kimataifa wa Utangazaji wa Utalii ili kuwavutia watalii wengi zaidi;

(b) Kuongeza msukumo katika utalii wa kihistoria kwa kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya malikale na kuyatangaza maeneo hayo;

(c) Kuongeza bajeti ya Sekta ya Utalii ili kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi;

(d) Kuimarisha mafunzo ya Hoteli na Utalii hususan katika ngazi ya shahada ili kuongeza ubora wa watumishi wa huduma za

Ukarimu na Utalii kwa kukifanya Chuo cha Taifa cha Utalii kutoa mafunzo ya ukufunzi;

(e) Kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii wa ndani na kuweka mazingira yatakayowezesha wawekezaji wa ndani kuendeleza biashara za utalii pamoja na kuwajengea uwezo waongoza watalii;

(f) Kufanya jitihada za kufungua fursa za utalii katika Kanda ya Kusini pamoja na kutumia fukwe zake;

(g) Kuendelea kujenga mazingira bora ya kuwawezesha vijana kuanzisha kampuni za kutembeza watalii katika maeneo mbalimbali ya utalii; na

(h) Kuhifadhi malikale kwa kuishirikisha jamii kutumia Malikale kama chanzo cha kujipatia kipato kwa kutoa elimu ya ujasiriamali, kutenga maeneo ya biashara, kuishirikisha sekta binafsi na kutoa elimu ya uhifadhi kwa umma.

**Maliasili**

30. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Sekta ya Maliasili, Serikali imechukua hatua za kuhakikisha kuwa sekta hii inapewa msukumo wa kutosha ili iweze kuchangia kikamilifu katika kuboresha maisha ya wananchi. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(a) Hatua zimechukuliwa za kuimarisha mahusiano mema baina ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Maeneo 16 yaliyokosa sifa ya kuendelea kuwa maeneo ya hifadhi yamerejeshwa kwa mamlaka za wananchi;

(ii) Vijiji vinavyopakana na hifadhi vimepatiwa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, barabara na masoko; na

(iii) Jumla ya wanavijiji 7,320 wamepatiwa mizinga ya nyuki 24,076 na kupewa mafunzo ya mbinu za kisasa za ufugaji nyuki na kutafuta masoko ya asali ikiwa ni pamoja kuwawezesha kushiriki katika maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi.

(b) Upandaji wa miti kwenye misitu ya jamii umeongezeka ambapo wastani wa miti milioni 200 kwa mwaka imepandwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ambapo asilimia 65 ya miti yote iliyopandwa imeendelea kukua vizuri.

31. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba Sekta ya Maliasili inazidi kuimarika ili kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili hususan misitu na nyuki yanaendelea kuchangia katika ukuaji wa uchumi, kuwaongezea wananchi kipato na kuongeza fursa za ajira. Ili kufikia azma hiyo Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kujenga mahusiano mema baina ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo kwa namna ambayo wananchi hao watanufaika na uwepo wa hifadhi hizo;

(b) Kutatua migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo ya jirani na hifadhi kwa kushirikisha wadau katika kuhakiki mipaka ya maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za kudumu; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na kuzingatia utawala wa Sheria katika kusimamia rasilimali za maliasili;

(c) Kuboresha miundombinu ndani ya Mapori ya Akiba na Vikosi dhidi ya ujangili na kuongeza vitendea kazi vya kisasa kwa ajili ya doria na upelelezi nje na ndani ya maeneo ya hifadhi;

(d) Kuendelea kutekeleza programu ya ufugaji nyuki ya mwaka 2007–2016 ili kuwajengea uwezo wadau wake kuzifahamu mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya nyuki na pia masoko ya asali na nta ya ndani na nje ya nchi;

(e) Kuendelea kuimarisha doria za ulinzi wa wananchi dhidi ya wanyamapori kwa kuboresha mfumo wa utoaji taarifa za wanyamapori waharibifu. Aidha, Serikali itaboresha na kutoa kwa wakati kifuta machozi kwa watu au familia zitakazoathirika kwa kiwango kinacholingana na athari zitakazotokea;

(f) Kuongeza eneo la kupanda miti kutoka hekta 60,000 mwaka 2015 hadi hekta 130,000 mwaka 2020 na kuhakikisha kwamba mbao zinazovunwa zinatumiwa kwa ajili ya kutengeneza samani na matumizi mengine hapa nchini badala ya kusafirisha magogo nje ya nchi;
(g) Kuweka utaratibu wa wazi utakaowawezesha wananchi wanaoishi jirani na hifadhi kufaidika na rasilimali hizo;
(h) Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori ambayo moja kati ya majukumu yake ni kuweka utaratibu utakaotumika katika kutoa vibali vya uvunaji wa raslimali za maliasili; na
(i) Kupambana na ujangili wa wanyama pori wakiwemo Tembo na Faru.

**Viwanda na Biashara**

32. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Ilani ya Uchaguzi iliweka msukumo mkubwa zaidi katika kuimarisha uzalishaji katika viwanda vilivyopo na kujenga viwanda vipya ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na michepuo ya bidhaa, kuhimiza mauzo ya bidhaa ndani na nje ya nchi na kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuendeleza viwanda vya kimkakati kupitia mashirikia ya Umma ya NDC na EPZA. Katika kipindi hicho mafanikio makubwa yamepatikana ambayo ni pamoja na:-

(a) **Ukuaji wa Sekta ya Viwanda:**
   (i) Sekta ya Viwanda imekua kutoka asilimia 7.7 mwaka 2010 hadi asilimia 7.9 mwaka 2013. Ukuaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kuimarika kwa uzalishaji viwandani, hususan viwanda vya vinywaji, saruji, bidhaa za chuma; na usindikaji wa mazao ya kilimo;
   (ii) Mwenendo wa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 9.6 mwaka 2010 hadi asilimia 9.9 mwaka 2013; na
   (iii) Miradi mipya ya viwanda vilivyosajiliwa na ujenzi kuanza katika kipindi husika imefikia 454.

(b) Ujenzi wa viwanda vinane vya Saruji ambao uko katika hatua za mwisho za kukamilika ambavyo vitawezesha Taifa kuongeza

uzalishaji zaidi ya maradufu na hivyo nchi yetu kuijitosheleza kwa saruji na nyingine kuuzwa nje. Aidha, ksukamilika kwa viwanda hivi kutaifanya bei ya saruji kushuka na pia kuongeza ajira mambo ambayo yataendelea kuboresha ustawi wa wananchi;

(c) Katika Kanda ya Ziwa, ujenzi wa Kiwanda cha Nguo unaendelea. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kutumia kiwango kikubwa cha pamba inayozalishwa katika ukanda huo hatua ambayo itahakikisha soko la uhakika la pamba na kuongeza ajira kwa wakazi wa eneo hilo na kwa Watanzania kwa ujumla;

(d) Ujenzi wa viwanda viwili vikubwa vya ngozi unaoendelea katika mikoa ya Arusha na Shinyanga ambapo utakapokamilika utafanya uuzaji wa ngozi ghafi nje ya nchi kuwa historia. Ngozi na bidhaa za ngozi zitauzwa nje ya nchi zikiwa zimeongezewa thamani na hivyo kuongeza ajira; na

(e) Uzalishaji wa mbolea za NPK na MRP katika kiwanda cha Minjingu umeongeza kutoka tani 75,000 hadi kufikia tani 100,000 kwa mwaka.

(f) **Mauzo ya Bidhaa za Viwandani:**

(i) Mauzo kwenda soko la nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yameongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 419 mwaka 2010 hadi dola milioni 450 mwaka 2013;

(ii) Mauzo kwenda soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yameongezeka kutoka dola za Marekani 625 mwaka 2010 hadi kufikia dola 1,209 mwaka 2013; na

(iii) Mauzo katika soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 51 mwaka 2010 hadi dola milioni 76 mwaka 2013.

(g) **Maeneo Maalumu ya Uwekezaji:**

(i) Mikoa 20 imetenga Maeneo Maalumu ya Uwekezaji ili yawekewe miundombinu ya msingi itakayovutia Sekta Binafsi kujenga viwanda na kufanya biashara katika maeneo hayo; na

(ii) Sheria za Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ) na Maeneo Maalumu ya Uchumi (SEZ) zimepitiwa ambapo vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na nafuu ya kodi vimebainishwa ili kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji.

(h) Benki ya Rasilimali imeanzisha Dirisha Maalumu kwa ajili ya kuwezesha wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kupata mikopo kwa riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda;

(i) Jumla ya makampuni 130 yamewekeza mitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 2,041.6 mwaka 2014 ukilinganisha na Shilingi bilioni 126.6 mwaka 2010 na kutengeneza ajira za moja kwa moja zilizotokana na uwekezaji huo kufikia 31,923; na

(j) Ekari 107 zimepimwa katika Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kuanzisha Vijiji vya Viwanda (Industrial Villages) na kupata hati miliki (Title Deeds) ili kuanzisha viwanda vya kusindika na kutengeneza bidhaa za ngozi.

(k) **Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI):**
Katika kipindi cha mwaka 2010-2013, jumla ya mikopo 56,517 yenye thamani ya Shilingi bilioni 30.6 imetolewa na kuwezesha upatikanaji wa ajira zipatazo 113,876 kupitia Mfuko wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo (NEDF).



*Mradi wa Kiwanda cha kukamua mafuta ya Alizeti kinachojengwa nje kidogo ya mji wa Dodoma.*

33. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015–2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuweka nguvu kubwa katika kukamilisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Awamu ya Tatu (2010–2020) ambayo malengo yake ni kuiwezesha Sekta ya Viwanda kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama ilivyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Aidha, Utekelezaji wa Ilani hii utakuwa ni sehemu ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16-2020/21) ambao lengo lake ni kuendeleza uchumi wa viwanda.**

**Katika kipindi hicho, utaanza ujenzi wa viwanda mama (basic industries) na kuimarisha viwanda vilivyopo lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba:-**

(a) Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa unaongezeka kutoka asilimia 9.9 mwaka 2013 hadi asilimia 15 ifikapo mwaka 2020;

(b) Sekta ya Viwanda inaongeza ajira kufikia asilimia 40 ya ajira zote ifikapo 2020 kwa kuweka kipaumbele cha kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini kama vile kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili; Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya nguo, sabuni, korosho, matunda n.k.

(c) Kuandaa mikakati thabiti ya kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vikubwa na vya kati na kuweka utaratibu wa kuvilinda dhidi ya viwanda vya nje;

(d) Kujenga mazingira rafiki yatakayowezesha kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji wa viwanda;

(e) Kuanzisha viwanda vya msingi vinavyotumia malighafi ya chuma katika maeneo ya Liganga na Mchuchuma;

(f) Sekta ya Viwanda inaongeza fursa za masoko hususan yenye upendeleo wa ushuru wa forodha kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Utatu wa COMESA-EAC-SADC na Umoja wa Ulaya, nchi rafiki kama India, China, Japan na Marekani; na

(g) Kuendeleza kasi ya ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati hasa vinavyosindika mazao.

(h) Kuhakikisha Benki ya Rasilimali (TIB) inapanua wigo wa Dirisha Maalumu ili liweze kutoa huduma zake kwenye maeneo yote nchini ikiwemo Tanzania Zanzibar.

**Madini**

34. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendeleza juhudi katika kuhakikisha Sekta ya Madini inachangia kikamilifu katika kukuza uchumi na ajira. Kutokana na juhudi hizo, mchango wa madini katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 3.3 mwaka 2010 hadi asilimia 3.5 mwaka 2014. Kuimarika kwa sekta hii kumetokana na kufanyika mambo yafuatayo:-

(a) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) limewezeshwa kumiliki hisa kwenye migodi ya STAMIGOLD (100%), Buchreef (45%),

Buhemba (100%), Kiwira (100%), Tanzaniteone (50%), Tulawaka (100%), NDC–Liganga (20%), Mchuchuma (20%), Ngaka Coal Projects (30%) na Mgodi wa Almasi wa Mwadui (25%);

(b) STAMICO imeanzisha Kampuni iitwayo Kyerwa Tin Company Limited (KTCL) ili kununua madini ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo wa madini hayo huko Kyerwa. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya tani 71.3 zimenunuliwa kwa gharama ya Shilingi 1,106,326,000. Aidha, tani 30 zimeuzwa kwa Dola za Marekani 201,000;

(c) STAMICO imefanikiwa kupata kandarasi nne (4) za uchorongaji na utafiti wa madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.35 ambapo jumla ya ajira mpya 78 zimepatikana kutokana na upatikanaji wa mashine za kisasa za uchorongaji;

(d) Ofisi mbili za madini za Kanda zimeanzishwa; moja katika Kanda ya Ziwa Nyasa inayohudumia Mikoa ya Njombe na Ruvuma; na nyingine kanda ya Ziwa ambayo inahudumia Mikoa ya Mara na Simiyu ili kusimamia na kudhibiti biashara ya madini. Kuanzishwa kwa ofisi hizo mpya kumeongeza idadi ya ofisi za Kanda kufikia kumi (10) na hivyo kuongeza ufanisi kwa wadau wa sekta hii; na

(e) Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) umeendelea kuwezeshwa kwa kupatiwa fedha na vitendea kazi ili kuimarisha utendaji kazi wake. Katika kipindi hicho Wakala wa Jiolojia amepata mafanikio yafuatayo:-

  (i) Mfumo wa utunzaji, uchakataji, na usambazaji/uuzaji wa takwimu na taarifa za upatikanaji madini ili kuvutia uwekezaji umeboreshwa;

  (ii) GST imejiunga na COSOTA ili kusajili machapisho yake na kupewa haki miliki (*Copyright)*;

  (iii) GST imejenga maabara ya kisasa ya kuchunguza miamba na madini baada ya kununua vifaa muhimu na vya kisasa; na

(iv) GST imefanikiwa kufanya ugani na uchoraji wa ramani za upatikanaji wa madini *(geological and mineral occurrence mapping)* kwa asilimia 92 ya ardhi kavu ya Tanzania Bara.

(f) Idadi ya leseni za madini imeongezeka hadi kufikia 37,261 mwaka 2015 ambapo leseni za uchimbaji mkubwa ni 15; uchimbaji wa kati ni 380; uchimbaji mdogo ni 33,131; na leseni za utafutaji madini ni 3,735. Watanzania wanamiliki asilimia 70 ya leseni hizo, wageni asilimia 25 na asilimia 5 ya leseni hizo zinamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na Wageni;

(g) Wachimbaji wadogo wametengewa maeneo 25 yenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,407 na jumla ya leseni 8,800 zimetolewa kwenye maeneo hayo;

(h) Wachimbaji wadogo 10,000 wamepatiwa mafunzo ya huduma za ugani (extension services) katika nyanja za kutambua umbile na tabia ya mashapo, masuala ya utunzaji wa mazingira, utambuzi wa madini na uboreshaji wa uchenjuaji madini;

(i) Jumla ya Shilingi milioni 909.5 zimetolewa kwa wachimbaji wadogo kama ruzuku;

(j) Mpango wa utunzaji mazingira katika maeneo ya uchimbaji wa madini *(Modern Environmental Protection Plan)* umeanzishwa na umewahamasisha wachimbaji wadogo kutunza mazingira na kuepuka kuchafua vyanzo vya maji;

(k) Mikataba ya madini imepitiwa kwa lengo la kulinda maslahi ya nchi ambapo baadhi ya vipengele vimefanyiwa marekebisho ili mrahaba ulipwe kwa kiwango cha asilimia 4 ya mauzo ghafi ya dhahabu (*gross value*) badala ya asilimia 3 ya mauzo halisi ya dhahabu (*Net Back Value*) iliyokuwa ikilipwa na wawekezaji hapo awali;

(l) Migodi ya Bulyanhulu, North Mara, Buzwagi na Geita imeanza kulipa ushuru wa huduma (service levy) kwa Halmashauri husika kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mapato ghafi ya migodi hiyo badala ya Dola za Kimarekani 200,000 zilizokuwa zinalipwa kwa mwaka;

(m) Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) imeanzisha madawati ya ukaguzi kwenye viwanja vya ndege vya Kimataifa ili kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nje ya nchi, hatua iliyowezesha kukamatwa madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 15; na

(n) Kamati Maalumu ya Kitaifa (National Local Content Committee) imeundwa ili kusimamia mikakati iliyowekwa na wadau kuhakikisha kuwa Makapuni ya Madini yanaongeza kiwango cha manunuzi ya bidhaa na huduma hapa nchini kwa lengo la kuongeza ajira na soko la bidhaa za ndani.

35. **Katika kipindi cha 2015 hadi 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali yake kutekeleza mambo yafuatayo ili kuendelea kukuza Sekta ya Madini na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa:-**

(a) Kuweka na kusimamia mfumo thabiti wa kukagua shughuli za migodi, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini kwa malengo mapana ya kuongeza mapato ya Serikali;

(b) Kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya kuvutia mitaji ya uwekezaji katika Sekta ya Madini, hususan kwenye madini adimu (Rare Earth Elements - REE);

(c) Kuhamasisha uzalishaji na masoko ya madini ya viwandani;

(d) Kuweka miundombinu muhimu (umeme, simu, maji, barabara) kupitia ushirikiano wa Serikali na Sekta Binafsi (PPP) kwenye maeneo yenye uwezekano wa kuanzishwa kwa migodi mikubwa mipya;

(e) Kuboresha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini, na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wadau kuhusu Sekta ya Madini;

(f) Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa upatikanaji, utunzaji, usafirishaji na matumizi ya baruti katika shughuli za migodi;

(g) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za utafutaji,

uchimbaji na utoaji huduma katika Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali na Watanzania wote;

(h) Kuendelea kuujengea uwezo wa kifedha na rasilimali watu Wakala wa Jiolojia Tanzania ili uweze kufikia kiwango bora zaidi katika ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu za kijiolojia na kijiofizikia zitakazosaidia katika kuchochea kasi ya utafutaji na upatikanaji wa mashapo ya madini hapa nchini yanayoweza kuchimbwa kwa faida;

(i) Kuendelea kuujengea uwezo Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania na Ofisi za Madini Mikoani ili zijiimarishe katika kukagua na kusimamia shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini, na hivyo kuongeza manufaa yatokanayo na Sekta ya Madini kwenye uchumi;

(j) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ili kukuza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa;

(k) Kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi itakayowezesha kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini;

(l) Kuweka na kutekeleza mikakati maalumu itakayowezesha soko la Tanzanite hapa nchini kuimarika zaidi na hivyo kuongeza manufaa yatokanayo na madini hayo yanayopatikana Tanzania pekee;

(m) Kuwawezesha wachimbaji wadogo kujiajiri kupitia sekta hii kwa kufanya yafuatayo:-

   (i) Kuwatambua, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji madini;
   (ii) Kuwapatia ruzuku, mafunzo, teknolojia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji;
   (iii) Serikali kupitia STAMICO kwa kushirikiana na wachimbaji wakubwa kuwawezesha kupata mikopo na masoko; na

(iv) Kuendelea kuongeza na kuwekeza mtaji wa Benki ya Rasilimali (TIB) ili iweze kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

(n) Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa migodi katika masuala ya usalama, utunzaji wa mazingira na afya migodini; na

(o) Kuhakikisha migodi yote mikubwa nchini inaendelea inanunua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadri ya upatikanaji wake.

## SURA YA TATU
## SEKTA ZA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA KIUCHUMI

**Ardhi**

36. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imepata mafanikio yafuatayo katika Sekta ya Ardhi:-

(a) **Utawala wa Ardhi**:

(i) Jumla ya vijiji 1,619 katika Halmashauri za Wilaya 37 vimepimwa;

(ii) Jumla ya vijiji 5,558 vimepatiwa vyeti vya Ardhi ya Kijiji;

(iii) Jumla vijiji 509 vimeandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya 69 nchini;

(iv) Jumla ya Hatimiliki za Kimila 348,000 zimetolewa; na

(v) Ofisi za Ardhi za Kanda zimeanzishwa na kuimarishwa.

(b) Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013-2033) umeandaliwa na utekelezaji wake umeanza ambapo Vijiji 509 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya 69 nchini na kufanya vijiji vilivyoandaliwa mipango hiyo kufikia 1,560.

(c) **Mipango Miji**:

(i) Programu ya Kurasimisha na Kuzuia Makazi Holela imeandaliwa mwaka 2012;

(ii) Elimu ya Urasimishaji na Kuzuia Makazi Holela imetolewa katika mikoa mbalimbali;

(iii) Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Dar es Salaam zimetoa leseni za makazi 35,362 na kutoa Hati 2,204 za kumiliki Ardhi;

(iv) Huduma za upimaji na ramani zimepelekwa katika ofisi mbalimbali za Kanda;

(v) Ili kupunguza msongamano katika miji mikubwa nchini hususan Dar es Salaam na Arusha, mipango kabambe ya

kujenga miji midogo ya Luguruni (ekari 156.53), Mji Mpya wa Kigamboni (ekari 16,047) na Kawe (ekari 267.71) imekamilika. Aidha, miji midogo ya Burka/Matevesi (ekari 579.2) na eneo la Usa River (ekari 296) katika Jiji la Arusha itajengwa; na

(vi) Mpango wa kuanzisha mji mpya wa kisasa wa Kigamboni ili kukabiliana na ukuaji wa kasi wa Jiji la Dar es Salaam umekamilika. Hatua ambazo zimefikiwa katika uanzishwaji wa mji huo wa kisasa ni:-

- Wakala wa kusimamia utekelezaji na uendelezaji wa Mpango wa Mji mpya wa Kigamboni (KDA) umeundwa;
- Rasimu ya Mpango Kabambe wa Mji mpya wa Kigamboni imeandaliwa (Kigamboni New City Master Plan – 2011 – 2031);
- Ujenzi wa daraja la Kigamboni na barabara kiunganishi unaendelea chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi;
- Eneo la upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam katika Kata ya Vijibweni limebainishwa na kazi ya uthamini inaendelea; na
- Utaratibu mpya wa uendelezaji wa Mji wa Kigamboni umepitiwa na kuridhiwa na Kamati ya Wadau wa Kigamboni ambapo Serikali itajihusisha zaidi na uwekezaji katika kuweka/kujenga miundombinu kama vile barabara, umeme na maji. Wananchi wataruhusiwa kufanya yafuatayo:-
    - Kuwa waendelezaji wenyewe katika eneo la mradi kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa kuendeleza Mji wa Kigamboni; au
    - Kuingia ubia na mwekezaji, ambapo thamani ya ardhi ya mwananchi itakuwa ndio mtaji wake; au

- Kulipwa fidia/kuuza eneo lake kwa wawekezaji/Serikali kwa bei ya soko.

(d) Kazi ya kuanzisha Benki ya Ardhi (Land Bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje imeendelea kutekelezwa na jumla ya Shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kianzio cha Mfuko wa Fidia ya Ardhi (Land Compensation Fund). Aidha, mashamba 66 mkoani Morogoro yameainishwa kwa ajili ya kuingizwa kwenye Hazina ya Ardhi na mashamba 112 mkoani Arusha yamekaguliwa na kupendekezwa kuingizwa kwenye Hazina ya Ardhi;

(e) Baadhi ya Halmashauri za Miji na Wilaya nchini zimewezeshwa kutumia mfumo wa teknolojia ya kompyuta katika kutoa huduma za ardhi;

(f) Halmashauri za Miji na Wilaya zimeendelea kujengewa uwezo kupitia Mfuko wa Mzunguko (Plot Development Revolving Fund) wa kupima viwanja na kuviuza kwa wananchi ambapo jumla ya Halmashauri 14 zimeidhinishiwa mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 2.67; na

(g) Hatua zifuatazo zimechukuliwa katika kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji ili kuhakikisha majukumu ya Sekta ya Ardhi yanatekelezwa ipasavyo:-

   (i) Kompyuta 100 kwa ajili ya matumizi ya shughuli za Sekta ya Ardhi katika Halmashauri 100 hapa nchini zimenunuliwa na kusambazwa;

   (ii) Vifaa vya upimaji vimenunuliwa na kufikishwa katika Halmashauri ya Manyoni (Total station 1), Jiji la Mbeya (Total station 1), Ofisi ya Mkoa wa Mwanza (GPS 1 na Total station 1); na

(h) Pamoja na changamoto zinazoyakabili Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, hatua zifuatazo zimechukuliwa katika kushughulikia mashauri yahusuyo ardhi na nyumba:-

   (i) Mabaraza 39 ya wilaya mbalimbali yamepatiwa watumishi, samani na vitendea kazi;

(ii) Mabaraza mapya 10 yameanzishwa katika wilaya za Nzega, Manyoni, Kilosa, Tunduru, Mpanda, Kyela, Muleba, Ngara, Karagwe na Ngorogoro hivyo kufanya mabaraza yanayotoa huduma kufikia 49; na

(iii) Hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya wenyeviti wa mabaraza ya wilaya waliokiuka maadili ya umma.

(i) Shirika la Taifa la Nyumba (NHC) kwa kushirikiana na sekta binafsi limeendelea kujenga nyumba kwa ajili ya makazi na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Ujenzi wa majengo ya biashara 81 na nyumba za makazi 5,900 umekamilika;

(ii) Ujenzi wa majengo 50 ulioshirikisha sekta binafsi umekamilika; na

(iii) Ardhi yenye ukubwa wa ekari 4,642 katika maeneo mbalimbali nchini imenunuliwa kwa ajili miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba.

(j) Wakala wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) umefanya yafuatayo:-

(i) Utafiti kuhusu mashine za kufungamana (interlocking press machine), kofia, mashine za "hydraform", majaribio ya sampuli ya udongo, ujenzi wa zege na kofia za vigae vya kuezekea ulifanyika na matokeo ya utafiti huo yameenezwa katika Halmashauri za Wilaya za Namtumbo, Karatu, Monduli, Simanjiro, Sumbawanga, Bariadi, Kilombero, Rungwe na Halmashauri za Manispaa za Temeke, Kinondoni, Ilala, Tabora, Iringa, Dodoma na Halmashauri ya Jiji la Tanga; na

(ii) Jumla ya mashine za kufyatulia matofali 1,105 ziligawiwa kwa Halmashauri mbalimbali nchini.

(k) Uanzishwaji wa vyama vya Ushirika wa Nyumba umeendelea kuhamasishwa ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini kunufaika na mikopo ya nyumba ambapo:-

(i) Vijana 150 wamepewa mafunzo ya teknolojia ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika ofisi za Wakala, katika Mkoa wa Kagera (vijana 55) na Jiji la Dar es Salaam (vijana 95);

(ii) Mwongozo kuhusu kuanzisha na kusimamia vyama vya Ushirika wa Nyumba umeandaliwa; na

(iii) Jumla ya mashine 656 za kufyatulia matofali yanayofungamana zimetolewa kwa Halmashauri 163 ambapo kila Halmashauri ilipatiwa wastani wa mashine nne.

(l) Ujenzi wa mtandao wa upimaji nchini wenye alama 640 za madaraja mbalimbali umekamilika kwa asilimia 98;

(m) Upimaji wa njia za kuingia katika bandari (port approaches) za Dar es Salaam na Zanzibar umekamilika;

(n) Kampuni ya Dhamana ya Mikopo ya Nyumba *(The Tanzania Mortgage Refinancing Company)* imeanzishwa kwa lengo la kutoa mikopo ya muda mrefu kwa benki za biashara ili nazo zitoe mikopo ya nyumba ya muda mrefu kwa wananchi ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

i. Benki za biashara 20 zimetoa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi 3,598;

ii. Mfuko wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba *(Housing Micro-finance Fund)* umeanzishwa chini ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Aidha, mtaji wa Shilingi bilioni 36 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Nyumba (TMRC);

iii. Mwongozo kuhusu sifa za taasisi za fedha zinazostahili kupata mkopo kutoka TMRC umeandaliwa; na

iv. Mpango wa kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za mikopo ya nyumba umeandaliwa.

(o) **Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali:**

Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015, Serikali kupitia Wakala wa Majengo (TBA) imendelea na ujenzi wa ofisi za Serikali, nyumba za viongozi na mradi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya watumishi wa umma katika mikoa mbalimbali nchini**.** Ujenzi wa majengo ya umma umekuwa ukizingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu.

37. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza mipango ya kuendeleza ardhi katika maeneo yafuatayo:-**

(a) **Utawala wa Ardhi**

(i) Kujenga mfumo utakaorahisisha umilikishaji wa ardhi na uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi kwa kukamilisha ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi *(Integrated Land Management Information System)*;

(ii) Kuimarisha huduma za ardhi katika Kanda kwa kujenga majengo manane (8) ili kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Moshi), Magharibi (Tabora), Kati (Dodoma), Kusini (Mtwara), Kanda ya Mashariki, na Kanda ya Dar es Salaam inayohudumia mkoa wa Dar es Salaam;

(iii) Kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi katika Kanda nane (8) za Ardhi nchini kwa lengo la kuongeza kasi ya utoaji wa Hatimiliki za Kimila nchini;

(iv) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Miji na Wilaya kwa kuzipatia mafunzo, vifaa, rasilimali fedha na wataalamu ili ziweze kupima viwanja na mashamba nchini;

(v) Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi ili uweze kufidia ardhi itakayotwaliwa kwa matumizi ya umma na uwekezaji;

(vi) Kufanya uhakiki wa mashamba pori yasiyoendelezwa kwa kipindi kirefu na kugawa upya kwa wananchi;

(vii) Kuanzisha Baraza la Taifa la Ushauri la Ardhi (*National Land Advisory Council*) ili kuwezesha ardhi kutumika kwa ufanisi;

(viii) Kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Sheria zingine zinazohusiana na utawala wa ardhi;

(ix) Kuimarisha huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kuanzisha Mabaraza mapya 100 ya Ardhi na Nyumba kwenye wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi;

(x) Kuhakikisha maafisa ardhi wasio waaminifu wanashughulikiwa; na

(xi) Kuanzisha akiba ya ardhi (land bank).

(b) **Utayarishaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya ardhi nchini**

(i) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi;

(ii) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 7,500 na mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya 25;

(iii) Kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini;

(iv) Kuwapatia wananchi hatimiliki za kimila 2,500,000 pamoja na kujenga masjala za ardhi 250 katika ngazi za Wilaya na Vijiji; na

(v) Kuwapatia wananchi hati miliki 2,000,000 pamoja na kusajili nyaraka nyingine za kisheria.

(c) **Nyumba**

(i) Kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kwa masharti nafuu;

(ii) Kuwaelimisha wananchi kuzielewa sheria za mikopo ya nyumba ili wazitumie kupata mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba na kuhamasisha mabenki na asasi nyingine za fedha zitoe mikopo ya nyumba kwa muda mrefu na yenye riba nafuu;

(iii) Kuweka utaratibu utakaowezesha kuanzisha Benki ya Nyumba ya Taifa;

(iv) Asasi za Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zitajenga nyumba za gharama nafuu zisizopungua 50,000;

(v) Kuwawezesha wanavijiji kujiunga kwenye vikundi vya ujenzi vitakavyopatiwa elimu ya jinsi ya kujenga nyumba bora vijijini;

(vi) Kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwa Mwendelezaji Miliki Mkuu (*Master Estate Developer*);

(vii) Kupunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu hususan vijijini;

(viii) Kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika vya ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu;

(ix) Kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu; na

(x) Kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya serikali yenye kuzingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu kwa:-

- Kuanza ujenzi wa majengo yatakayotumika kama Ofisi kwa Taasisi za Serikali ili kuipunguzia Serikali gharama ya kodi kubwa ya pango katika soko huria;
- Kuendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya watumishi wa umma ambapo asilimia 50 zitajengwa katika maeneo ya vijijini; na
- Kuboresha karakana 6 za kutengeneza samani za ofisi na nyumba za Serikali ili kupunguza gharama za uagizaji wa samani kutoka nje ya nchi.

(xi) Kukamilisha utungaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba (*Housing Policy*).

(xii) Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti na Uendelezaji wa Miliki (*Real Estate Regulatory Authority*) ambayo pamoja na majukumu mengine itasimamia udhibiti wa kodi za pango kwa nyumba za makazi na biashara.

(d) **Mipango Miji na Vijiji**

(i) Kukamilisha uandaaji wa Mipango Kabambe (*Master Plans*) kwa miji mikuu yote ya mikoa;

(ii) Kuhimiza ujenzi wa miji ya pembezeno (Satilite cities) katika jiji la Dar es Salaam pamoja na miji mingine ili kufanya miji hiyo ikue kwa kuzingatia mipango miji;

(iii) Kuendelea kujenga mji mpya wa Kigamboni (*Kigamboni New City*) kwa kuzingatia matakwa, maslahi na ushiriki wa wananchi wa Kigamboni;

(iv) Kuendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi yaliyopo katika maeneo ambayo hayajapimwa kwa lengo la kuyapanga na kuyapima viwanja katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro na Mbeya. Program hii itatoa hatimilki za Makazi; na

(v) Kuendeleza maeneo yaliyoiva (*re-development scheme*) ya Kipawa, Namanga, Vingunguti, Manzese, Buguruni, Msasani Bonde la Mpunga na Kawe, Jijini Dar es Salaam.

(e) **Upimaji na Ramani**

Upimaji wa ardhi na utayarishaji wa ramani ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya matumizi ya ardhi kwa sekta mbalimbali. Hadi sasa ni sehemu ndogo tu ya ardhi ya nchi imepimwa, hivyo ili kuifanya ardhi kuchangia katika kukuza Pato la Taifa, kutoa fursa za ajira na kuvutia uwekezaji ipo haja ya kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi. **Katika kipindi hiki, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(i) Kuendeleza upimaji wa ardhi katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuimarisha ulinzi na usalama;

(ii) Kuimarisha alama za mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani za Kenya, Burundi, Zambia, Malawi, Uganda, Rwanda, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

(iii) Kujenga kituo cha kupokea picha za anga (*Satellite Receiving Station*) kitakachojengwa katikati ya nchi (Chuo Kikuu cha Dodoma) ambacho kitawezesha utayarishaji wa

ramani za msingi (*base maps*), kupanga na kuongeza kasi ya kupima ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali; na

(iv) Kuzijengea uwezo wa rasilimali watu na fedha Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji na kuzipatia zana za kisasa za kupima ardhi na usanifu wa ramani na kuwapatia mafunzo stahiki watalaamu wa ardhi.

**Usafirishaji na Uchukuzi**

38. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji umechochea kukua kwa shughuli za kiuchumi ambazo zimewezesha pia kuongeza ajira nchini. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, reli, madaraja, vivuko na viwanja vya ndege ambao umekuwa msingi wa kukua kwa uchumi wetu na shughuli nyingine za kijamii. Tanzania imepiga hatua kubwa katika sekta hii na kuifanya kuwa moja kati ya nchi zenye mtandao mzuri wa miundombinu ya usafiri hususan barabara katika Bara la Afrika.

(a) **Barabara**

Nchi yetu ina mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa kilometa **35,000** zinazojumuisha kilometa **12,786** za barabara kuu na kilometa **22,214** za barabara za mikoa.

Katika kipindi cha miaka kumi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **13,753** zimekuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa **4,691** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **2,358** zimeendelea kujengwa katika kiwango cha lami. Aidha, jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa **3,419** zimefanyiwa upembuzi na usanifu kwa ajili ya ujenzi. Barabara hizo ni kama zilivyoanishwa:-

(i) **Barabara ambazo zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami:**

- Korogwe – Handeni (km 65)

- Dumila – Rudewa (km 45)
- Lwanjilo – Chunya (km. 36)
- Tanga – Horohoro (km 65)
- Masasi – Mangaka (km 54)
- Minjingu – Babati - Singida (km 222)
- Mwandiga – Manyovu (km 60)
- Handeni – Mkata (km 54)
- Barabara ya Kilwa/Dsm (km 12)
- Barabara ya Mandela/Dsm (km 16)
- Msimba – Ikokoto – Mafinga (km 219)
- Arusha – Namanga (km 105)
- Chalinze – Segera –Tanga (km 245)
- Isaka – Ushirombo (km 132)
- Rau Madukani – Mawela – Uru Njari (km 12.5)
- Tunduma – Sumbawanga (km 230)
- Sehemu ya Bonga – Babati (km 19.2)
- Dodoma – Iringa (km 260)
- Puge – Tabora (km 56)
- Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.30)
- Tabora – Ndono (km 42)
- Uvinza – Kidahwe (km 77)
- Daraja la Malagarasi na Barabara zake (km 48)
- Namtumbo – Songea (km 70)
- Peramiho – Mbinga (km 78)
- Ujenzi kwa sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 12.9)
- Segera – Korogwe (km 20)
- Korogwe – Mkumbara (km 76
- Arusha – Minjingu (km 104)
- Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85)
- Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 3.2)
- Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass) Km 10)
- Barabara ya Mafia (Mafia Access Road) (km 14)
- Barabara ya Dodoma University (km 12)

(ii) **Barabara ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi:**

- Mziha – Turiani – Magole (km 84.6)
- Dumila – Kilosa (km 63)
- Dumila – Turiani - Handeni (km 174)
- Bariadi – Lamadi (km 71.8)
- Mbeya – Chunya – Makongolosi (km 115)
- Makofia – Msata (km 64)
- Kisarawe – Maneromango (km 54)
- Ushirombo – Lusahunga (km 110)
- Kwa Sadala – Masama (km 12.2)
- Kibosho Shine – Kwa Raphael – International School (km 43)
- Kirua Nduoni – Marangu Mtoni (km 31.5)
- Kahama Mjini (km 5)
- Bunda – Kisorya – Nansio (km 93)
- Dodoma – Babati (km 261)
- Sumbawanga – Kinyani – Nyakanazi (km 562)
- Nzega – Tabora (km 116)
- Manyoni – Itigi – Tabora (km 264)
- Mangaka – Mtambaswala (km 65)
- Mto wa Mbu – Loliondo – Mugumu – Nata-Makutano (km 452)
- Tunduru – Namtumbo (km 194)
- Tabora – Urambo (km 90)
- Uyovu – Bwanga – Biharamulo (km 112)
- Kisesa – Usagara (km 17)
- Kyaka – Bugene (km 59)
- Segera – Same – Himo (km 261)
- Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 140)
- Nyanguge – Musoma – Sirari (km 262)
- Katumba – Mbambo – Tukuyu (km 80)
- Kaliua – Kazilambwa (km 56)
- Barabara ya Kibamba – Monganzila (km 4.0)

- Barabara ya KIA – Mererani (km 26)
- Mafinga – Igawa (km 137.9)
- Mwigumbi – Maswa – Bariadi (km 100)
- KAMATA – Bendera Tatu (km 1.3)
- Ardhi – Makongo – Goba (km 9)

(iii) **Barabara ambazo zimefanyiwa upembuzi na usanifu na baadhi ya maeneo ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea:**

- Makurunge – Saadan – Pangani – Tanga (km 178)
- Rujewa – Madibira – Mafinga (km 151)
- Matai – Kasesya (km 50)
- Mbinga – Mbamba Bay (km 66)
- Kamwanga – Sanya Juu (km 75)
- Makambako – Songea (km 295)
- Mtwara – Masasi (km 200)
- Sanya Juu – Bomang'ombe (km 25)
- Tabora – Mbambali – Bukene – Itobo – Kahama (km 149)
- Lupilo – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda (km 96)
- Ifakara – Mahenge (km 67)
- Kibondo – Mabamba (km 35)
- Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Jct (km 328)
- Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)
- Mpemba – Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49)
- Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)
- Makofia – Mlandizi – Vikumburu (km 148)
- Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 162)
- Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 428)
- Makongolosi – Rungwa – Mkiwa (km 412)
- Mtwara – Newala – Masasi (km 209)

- Handeni – Kiberashi – Kondoa – Singida (km 460)
- Kibaha – Mapinga (km 23)
- Geita – Bukoli – Kahama (km 107)
- Mbande – Kongwa Jct – Mpwapwa (km 50)
- Njombe – Makete (km 109)
- Nata – Fort Ikoma (km 141)
- Ipole – Koga – Mpanda (km 255)
- Dsm (Port) – TAZARA – JNIA – Pugu (km 29)
- Outer ring road (Pugu – Kinyerezi – Mbezi (Morogoro) – Mpiji Magore – Bunju (km 34)
- Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200)
- Sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 100) "Express way"
- Musoma – Makojo – Busekela (km 92)
- KAMATA – Bendera Tatu (km 1.3)
- Ardhi – Makongo – Goba (km 9)
- Daraja jipya la Selander (DSM)
- Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430)
- Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)
- Barabara ya Murugarama – Rulenge – Nyakahura (km 85)
- Barabara ya Ipole – Rungwa (km 172)
- Barabara ya Uongozi Institute (km 8.8)
- Barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 149)

(b) **Madaraja**

(i) Ujenzi wa daraja la Kilombero umeanza.
(ii) Ujenzi wa daraja la mto Mwatisi (Morogoro) umekamilika.
(iii) Ujenzi wa daraja la mto Malagalasi Kigoma, umekamilika.

(iv) Ujenzi wa daraja la Kigamboni ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam umekamilika kwa zaidi ya asilimia 80.

(v) Ujenzi wa daraja la Nangoo (Masasi), Ruhekei (Mbinga) na Mbutu (Igunga) umekamilika.

(vi) Ujenzi wa daraja la Rusumo (Kagera) umekamilika.

(vii) Ujenzi wa daraja la waenda kwa miguu la Mabatini (Mwanza) umekamilika.

(viii) Ujenzi wa daraja la Sibiti (Singida) unaendelea.

(ix) Upembuzi yakinifu na usanifu wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma) umekamilika.

(x) Ujenzi wa daraja la Kavuu (Katavi) unaendelea.

(c) **Vivuko**

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) imenunua vivuko vinane kwa ajili ya kutoa huduma katika maeneo mbalimbali Nchini.

(i) Msangamkuu (Mtwara)
(ii) Rusumo (Kagera) na
(iii) Ilagala (Kigoma)
(iv) Kahunda – Maisome
(v) Kahunda – Musoma – Kinesi
(vi) Kahunda – Kisorya – Rugezi
(vii) Dar es Salaam – Bagamoyo

(d) **Kupunguza Msongamano katika Jiji la Dar es Salaam**

Ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

(i) Usanifu wa kina umekamilika kwa makutano ya TAZARA na Ubungo kwa ajili ya kujenga barabara za juu; na

(ii) Serikali inaendelea kupanua mtandao wa barabara kwa kujenga na kukarabati barabara zifuatazo:-

- Mbezi (Morogoro road) – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14.0)
- Tegeta Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi mwisho (km 20.0)

- Tangi Bovu – Goba (km 9.0)
- Kimara – Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6)
- Kimara – Kilungule – External Mandela road (km 9.0)
- Ubungo Bus Terminal – Mabibo – Kigogo Round about (km 6.4)
- Kigogo Round about – Bonde la Msimbazi – Twiga/Msimbazi (km 2.7)
- Tabata Dampo – Kigogo – Ubungo Maziwa (km 2.25)
- Old Bagamoyo – Garden Road (km 9.0) Usanifu umekamilika
- Jet Corner – Vituka – Devis Corner (km 6) ujenzi umekamilika

(iii) Ujenzi wa awamu ya kwanza ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (Bus Rapid Transit – BRT): Kimara – Kivukoni, Fire-Kariakoo na Magomeni – Morocco (km 20.9) unaendelea.

39. **Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na huduma za kijamii. Aidha, kipaumbele katika ujenzi wa barabara kitazingatia barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani; barabara zinazounganisha mikoa; na barabara zinazokwenda kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi kama vile Liganga, Mchuchuma n.k. Ili kutimiza azma hiyo Serikali itafanya mambo yafuatayo:-**

(a) **Kuimarisha Mfuko wa Barabara (Tanzania Road Fund)**

(i) Kubuni vyanzo vipya na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya sasa ili kuongeza mapato;

(ii) Kubuni/kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kwamba thamani na ubora wa kazi unaendana na fedha zilizotumika (value for money); na

(iii) Kuanzisha wakala/taasisi itakayosimamia kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara za miji na majiji na Halmashauri ambazo ziko chini ya TAMISEMI.

(b) **Masuala ya Kisera**

Ili kupunguza umasikini, kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza kasi ya maendeleo, Serikali itashughulikia masuala yafuatayo:-

(i) Kuunganisha makao makuu ya mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami na kujenga barabara kuu zote zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kwa kiwango cha lami;

(ii) Kuhakikisha kuwa makao makuu ya Wilaya ambazo bado barabara zake hazipitiki majira yote zinafanyiwa ukarabati angalau kwa kiwango cha changarawe na kuzifanya zipitike majira yote ya mwaka;

(iii) Kupunguza umaskini kwa kushirikisha kikamilifu vikundi vya wananchi katika kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara kama vile kazi za kufyeka nyasi, kuzibua mifereji na kufanya usafi wa barabara zinazopita katika maeneo yao; na

(iv) Makandarasi wazalendo wanaoonesha nia ya kushiriki katika kazi kubwa za ujenzi wa barabara watapatiwa dhamana na Serikali ili kuwajengea uwezo na kuwapatia fursa za kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za sekta ya ujenzi.

(c) **Kukamilisha ukarabati wa barabara zote unaoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika barabara kuu na barabara za mikoa:-**

(i) **Kukamilisha Ujenzi (km 2,439.35)**

- Sumbawanga - Matai - Kasanga (km 56 kati ya km 112)

- Mziha - Turiani - Magole (km 75 kati ya km 84.6)
- Dumila - Kilosa ( km 18 kati ya km 63)
- Dumila – Turiani - Handeni (km 174)
- Bariadi - Lamadi (km 13 kati ya km 71.8)
- Mbeya - Chunya - Makongolosi (km 56 kati ya km 115)
- Bagamoyo - Makofia - Msata (km 7 kati ya km 64)
- Kisarawe - Maneromango (km 48 kati ya km 54)
- Kibosho Shine - Kwa Raphael - International School (km 24 kati ya km 43)
- Kirua - Nduoni - Marangu Mtoni (km 16 kati ya km 31.5)
- Nyamuswa - Bunda - Kisorya - Nansio (km 117 kati ya km 117.5)
- Babati - Dodoma (km 195.15 kati ya km 251)
- Sumbawanga - Kanyani - Nyakanazi (km 483.7 kati ya km 562)
- Nzega - Tabora (Puge) (km 20.5 kati ya km 116)
- Manyoni - Itigi - Tabora (km 113 kati ya km 264)
- Mangaka - Mtambaswala ( km 65)
- Makutano - Nata - Mugumu (km 125)
- Kyaka - Bugene (km 28 kati ya km 59)
- Tunduru - Namtumbo (km 194)
- Tunduru - Mangaka (km 137)
- Mwigumbi - Maswa - Bariadi (100)
- Tabora - Urambo (km 8.8 kati ya km 90)
- Uyovu - Bwanga - Biharamulo (km 112)
- Kisesa - Usagara (km 17)
- Mganza - Kasenda (km 4.2)
- Katumba - Mbambo - Tukuyu (km 80)
- Kidahwe - Kasulu (Kanyani) (km 50)
- Kikusya - Ipinda - Matema Beach (km 39.5)
- KIA - Mererani (km 26)

- Mwanga - Kikweni - Lomo (km 7.5 kati ya km 22.5)
- Kaliua - Kazilambwa (km 42 kati ya km 56)
- Singida - Sepuka - Ndago - Kizaga (75 kati ya km 89)
- Dodoma University Road (km 12)

(ii) **Kukamilisha Ukarabati (km 517.2)**

- Ushirombo - Lusahunga (km 67 kati ya km 110)
- Kawawa Jct - Mwenge (km 4.3)
- Segera - Same - Himo (km 131 kati ya 285)
- Nyanguge - Musoma - Sirari (km 177 kati ya km 262)
- Mafinga - Igawa (km 137.9)

(d) **Kuanza ujenzi mpya na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami**

(i) **Kuanza ujenzi (km 5,427.0)**

- Njombe - Makete (km 109)
- Nata - Fort Ikoma (km 30)
- Mto wa Mbu - Loliondo (km 213)
- Sanya Juu - Bomang'ombe (km 25)
- Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 359)
- Matai - Kasesya (km 50)
- Sanya Juu - Kamwanga (km 75)
- Rujewa - Madibila - Mafinga(km 151)
- Makurunge - Saadani - Pangani - Tanga (km 178)
- Mbinga - Mbamba bay (km 66)
- Mtwara - Mingoyo - Masasi (km 200)
- Mpemba - Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49)
- Makongolosi - Rungwa - Mkiwa (km 412)
- Mtwara - Newala - Masasi (km 209)
- Kibaha - Mapinga (km 23)
- Geita - Bukoli - Kahama (km 107)
- Mbande - Kongwa Jct - Mpwapwa (km 50)

- Ipole - Rungwa (km 172)
- Njombe (Kibena) - Lupembe - Madeke (Mfuji) Morogoro/Njombe Boarder (km 125)
- Njombe - Ndulamo - Makete - Kitulo - Isyonje(km 205)
- Itoni - Ludewa - Manda (km 211)
- Dar es Salaam - Chalinze - Morogoro express way (km 190)
- Musoma - Makojo - Busekera (km 92)
- Tabora - Mambali - Bukene - Itobo - Kahama (km 149)
- Lupilo - Malinyi - Kilosa kwa Mpepo - Londo - Kitanda (km 296)
- Ifakara - Mahenge (km 67)
- Kibondo - Mabamba (km 35)
- Kolandoto - Lalago - Mwanhuzi - Matala - Oldeani Jct (km 328)
- Mugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)
- Soni - Bumbuli - Dindira - Korogwe (km 74)
- Makofia - Mlandizi - Vikumburu (km 148)
- Handeni - Kiberashi - Kondoa - Singida (km 460)
- Pugu - Kifuru - Mbezi Mwisho - Mpiji Magoe - Bunju (km 34)
- Kisarawe - Mlandizi (km 52)
- Kiboroloni - Tsuduni - Kidia (km 10.8)
- TPC - Mabogini - Kahe (km 11.4)
- Nyamirembe Port - Katoke (km 50)
- Iringa - Ruaha National Park (km 104)
- Njombe (Ramadhani) - Iyayi (km 74)
- Mziha – Handeni (km 68)
- Kilosa – Mikumi (km 72.8)

(ii) **Kuanza Ukarabati (km 1055.12)**

- Arusha - Moshi - Himo-Holili (km 140)
- Makambako - Songea (km 295)
- Mtwara - Mingoyo - Masasi (km 200)
- Lusahunga - Rusumo (km 92)

- Nyakasanza - Kobero (km 60)
- Mlandizi - Chalinze (km 53)
- Mbeya -Tunduma (km 110)
- Igawa - Uyole (km 105.12)

(e) **Kuzifanyia upembuzi na usanifu wa kina km 6,530.7 barabara zifuatazo:-**

- Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 162)
- Mpanda - Ugala - Kaliua - Ulyankulu - Kahama (km 428)
- Arusha - Kibaya - Kongwa (km 430)
- Bugene - Kasulo (BENACO) (km 124)
- Mbeya - Igawa (km 116)
- Mbeya - Tunduma (km104)
- Murshaka – Murongo (km 125)
- Kilindoni – Ras Mkumbi (km 55) - Mafia
- Morogoro - Dodoma (km 263)
- Mwanza - Mwanza/Shinyanga (km 102)
- Mwanangwa - Misasi - Salawe - Kahama (km 149)
- Kibaoni - Majimoto - Kasansa - Muze - Kilyamatundu (km 200)
- Magu - Bukwimba - Ngudu - Jojiro (km 64)
- Tarime - Mugumu (km 87)
- Njombe - Iyayi (km 74)
- Amani - Muheza (km 34)
- Nyahunge – Sengerema (km 68)
- Mugakorongo - Rwambaizi – Murongo (km 125)
- Morogoro (Bigwa) - Mvuha (km 78)
- Morogoro Kibena -Lupembe-Mfuji (Morogoro/Njombe Boarder) (km 125)
- (Bigwa) - Kisaki (km 151)
- Kamanga - Sengerema (km 35) (Mwanza)
- Geita - Nzera - Nkome (km 54) (Geita)
- Upanuzi wa (Tegeta) - Bagamoyo (km 57)
- Kibada - Kimbiji (km 29.2)
- Murugarama - Rulenge - Nyakahura (km 85)

- Karatu - Mbulu - Haydom - Singida (km 190)
- Bariadi-Kisesa-Mwandoya-Ngoboko-Mwanhuzi-Sibiti-Mkalama-Iguguno (km 289)
- Mika - Utegi - Shirati (km 44)
- Chimala - Matamba - Kitulo (km 51)
- Upanuzi wa Kitonga Escarpment (km 10) (Iringa)
- Babati - Orkesumet - Kibaya (km 225)
- Kongwa – Mbuyuni NARCO JCT – Kibaya – Orkemet (km 340)
- Mbulu - Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63)
- Mafinga - Mgololo (km 77.6)
- Nyololo - Igowole - Mtwango (km 40.4)
- Igowole - Kasanga - Nyigo (km 54.5)
- Madaba - Mundindi (Liganga) - Mkiu (km 46) (Ruvuma)
- Kilwa - Liwale (km 258)
- Liwale - Nachingwea - Ruangwa (185)
- Kitai - Lituhi (km 93)
- Babati (Dareda) – Dongobesh (km 60)
- Mhutwe - Kamachumu - Muleba (km 53)
- Uru – Mamboleo – Materuni (km 10.2)
- Kongwa Ranch - Kiteto - Simanjiro - KIA (km 483)
- Mto wa Mbu - Longido - Karatu - Ngorongoro (km 300)
- Sanya Juu – Longido (km 65)
- Madaba – Mavanga – Ludewa (km 40)
- Likuyufusi – Mkenda (km 124)

(f) **Madaraja**

(i) **Kukamilisha ujenzi wa madaraja sita (6) yafuatayo**:-

- Kilombero na barabara za maingilio km 9
- Kigamboni na barabara za maingilio km 10
- Kavuu (Katavi)
- Sibiti (Singida)
- Lukuledi II (Lindi)
- Ruvu Chini (Pwani)

(ii) **Kuanza ujenzi / Ukarabati wa madaraja saba (7) yafuatayo**:-

- Ruhuhu (Ruvuma)
- Momba (Rukwa)
- Kirumi (Mara)
- Selander (daraja jipya) (DSM)
- Magara (Manyara)
- Wami Chini (daraja jipya) (Pwani)
- Pangani (Tanga)

(iii) **Kuanza usanifu wa madaraja matatu (3) yafuatayo**:-

- Daraja la Simiyu (Mwanza)
- Mzinga (DSM) na
- Mlalakuwa (DSM)



*Muonekano wa Daraja la Kigamboni litakapokuwa limekamilika kujengwa. Ujenzi umekamilika zaidi ya asilimia 80.*

(g)**Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar Es Salaam kwa kufanya yafuatayo**:-

**Kuanza ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara maeneo yafuatayo:-**

- TAZARA
- Ubungo
- Chang'ombe
- Uhasibu
- KAMATA

- Morocco
- Mwenge
- Magomeni
- Tabata

**Kuanza na kukamilisha ujenzi wa barabara na reli ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam:-**

(i) **Kukamilisha Ujenzi (km 80.1)**

- Mbezi - Malamba Mawili - Kinyerezi - Banana ( km 14)
- Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi/Morogoro Road (km 16.2 kati ya km 20)
- Tangi Bovu - Goba (km 5.2 kati ya km 9)
- Kimara Baruti - Msewe - Changanyikeni (km 2 kati ya 2.6)
- Kimara Kilungule - External Mandela Road (km 8.8 kati ya 9)
- Kigogo Round About - Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Jct.km(km 0.5 kati km 2.7)
- Tabata Dampo - Kigogo (km 1.6 kati ya km 2.25)
- Kibamba - Mlonganzila (km 8 kati ya km 12
- Upanuzi wa Kimara - Kibaha na Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji (km 23.8 kati ya km 25)

(ii) **Kuanza Ujenzi (km 58.8)**

- Upanuzi wa Mwai Kibaki (Morocco - Kawe Round About) na Garden Road ( km 9.1)
- Banana - Kitunda - Kivule – Msongola (km 14.7)
- Ardhi - Makongo - Goba (km 9)
- Upanuzi wa barabara ya Uwanja wa Ndege (JNIA) - Pugu (km 8)
- Upanuzi wa barabara ya Mbagala - Kongowe – Mwandege (km 4)
- Upanuzi wa barabara ya DSM Port -TAZARA - Uwanja wa Ndege (JNIA) (km 14)

(iii) **Kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT) Awamu ya Pili (II) na ya Tatu (III):-**

- Awamu ya II: Barabara ya Kilwa na Kawawa (km 19.3)
- Awamu ya III: Barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi Mohamed na

  Azikiwe (Km 23.6)

(iv) **Kuanza ujenzi wa reli ya usafirishaji wa abiria katika jiji la Dar es Salaam.**

(h) **Miradi ya kupunguza msongamano katika majiji na miji mingine yenye jumla ya km 102 kama ifuatavyo:-**

- Usagara - Kisesa (km 17) (Mwanza)
- Shabiby - Arusha road Round about (km 1.6) (Dodoma),
- Uyole - Songwe (km 40) (Mbeya)
- Iringa Bypass (km 7)
- Upanuzi wa barabara Mwanza - Mwanza Airport (km12),
- Upanuzi wa Babara ya Arusha Mjini - Kisongo (km 8.8),
- Babati Bypass (km. 12)
- Utofu - Majani Mapana - Duga Mwembeni (km 4) (Tanga)

(i) **Vivuko**

Kuimarisha usafiri wa majini katika mito, maziwa na bahari ili kufanya barabara kuwa na kiunganishi cha uhakika kwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa kivuko kipya cha Kigongo - Busisi Mkoani Mwanza;

(ii) Kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha Rugezi - Kisorya mkoani Mwanza;

(iii) Kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha Pangani - Bweni mkoani Tanga;

(iv) Upanuzi wa jengo la abiria wa kivuko cha Magogoni - Kigamboni upande wa Kigamboni; na

(v) Kuanza ujenzi wa Kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni.

**Uchukuzi**

40. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji wa reli, majini na usafiri wa anga na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) **Mashirika ya Reli**

(i) Shirika la Reli nchini (TRL) limeendelea kuimarishwa kwa kufanya yafuatayo:-

- Kununua na kukarabati vifaa mbalimbali (vichwa vya treni, mataruma, na mitambo ya kunyanyulia mabehewa);
- Kutandika reli za ratili 80 kwa yadi kutoka Kitaraka hadi Malongwe (kilometa 89);
- Ujenzi wa Madaraja makubwa matatu ya stesheni za Kilosa na Gulwe; na stesheni za Bahi na Kintinku; na

(ii) Kwa upande wa shirika la TAZARA, vichwa vya treni vya njia kuu vipya sita (6); mabehewa ya mizigo 90; vipuri vya matengenezo ya vichwa vya treni vitatu (3); na ukarabati wa mitambo ya kunyanyulia mizigo vinne (4) vimenunuliwa na ukarabati umefanyika. Aidha, mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania na Zambia yanaendelea ili kuboresha shirika hilo.

(b) **Ujenzi wa Reli Mpya**

Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Reli mpya ya Dar es Salaam-Kigali (Rwanda) na Msongati (Burundi) kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge) umekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa kutoka Isaka hadi Mwanza umekamilika.

(c) **Bandari**

(i) Huduma za uchukuzi kwenye maziwa zimeendelea kuimarishwa kwa kuboresha bandari za Kigoma, Mbamba Bay, Mwanza, Bukoba na Nansio; ikiwa ni pamoja na kuondoa mchanga katika bandari ya Kigoma, kukarabati

chelezo, kufunga maboya ya kuongozea meli, kununua Mobile Grove Crane tani 35, kununua mtambo wa kuondoa mchanga majini (dreadger) na upembuzi yakinifu wa Bandari Kavu ya Katosha. Aidha, uthamini wa eneo la Kibirizi kwa ajili ya kujenga maegesho ya vyombo vidogo vidogo vya majini umekamilika;

(ii) Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa boya la mafuta (SPM) na ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo. Aidha, upembuzi yakinifu wa kuboresha gati namba 1-7 na utafiti wa ujenzi wa gati (RoRo) kwa ajili ya kuhudumia meli za magari; ujenzi wa mfumo wa kuhamisha mizigo (conveyor system) na maghala (silo) kwa ajili ya kuhudumia shehena ya Kichele umekamilika.

(iii) Eneo la Msanga Mkuu lenye hekta 2,623 kwa ajili ya uendelezaji wa Bandari ya Mtwara na shughuli za EPZ limetengwa na kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari hiyo umekamilika; na

(iv) Ujenzi wa gati jipya la kisasa katika bandari ya Kilindoni-Mafia umekamilika.

(d) **Viwanja vya Ndege**

(i) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha na kupanua jengo la pili la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika;

(ii) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe umekamilika na kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga. Aidha, ujenzi wa jengo kubwa la abiria na uzio wa kiwanja unaendelea kukamilishwa;

(iii) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara umekamilika. Aidha, matengenezo katika jengo la abiria na barabara ya kurukia na kutua ndege umekamilika;

(iv) Mradi wa kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Kigoma awamu ya kwanza umekamilika. Aidha, upanuzi na

ukarabati wa kiwanja hicho awamu ya pili chini ya ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya umekamilika;

(v) Kazi za upanuzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba kwa kiwango cha lami kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege; barabara ya kiungo na maegesho ya magari imekamilika. Aidha, ujenzi wa jengo la abiria lipo katika hatua za mwisho za ujenzi; na

(vi) Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia kwa kiwango cha lami umekamilika.

(e) **Hali ya Hewa**

Utambuzi wa hali ya hewa ni muhimu kwa shughuli za kiuchumi zikiwemo za kilimo, uvuvi, usafiri hususan usafiri wa anga na majini. Utambuzi wa hali ya hewa ni muhimu pia kwa shughuli nyingine za kijamii ikiwa ni pamoja na kuweka tahadhari za majanga. Ili kuimarisha huduma za utambuzi wa hali ya hewa, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamefanyika mambo yafuatayo:-

(i) Rada mbili za utabiri wa hali ya hewa zenye ubora wa kimataifa zimenunuliwa na kufungwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza;

(ii) Kituo cha kutoa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa maeneo ya Ziwa Victoria kimeanzishwa mkoani Mwanza. Ili kuhakikisha kwamba taarifa za hali ya hewa zinawafikia wananchi na wadau wengine kwa wakati, taarifa za hali ya hewa sasa zinatolewa kwenye vyombo vya habari vikiwemo simu na mitandao ya kijamii; na

(iii) Vituo vitatu vya hali ya hewa (synoptic stations) vya Kilwa Masoko, Mpandeni Songwe vimeanza kufanya kazi. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Kituo Kikuu cha Hali ya Hewa umekamilika.

41. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo:-**

**Miundombinu ya Huduma za Reli**

(a) Kwa kushirikiana na sekta binafisi kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge):-
   (i) Dar es Salaam – Tabora – Kigoma/Mwanza
   (ii) Uvinza – Msongati (Burundi) na Isaka – Kigali (Rwanda)
   (iii) Mtwara – Songea – Mbamba Bay na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga
   (iv) Tanga – Arusha – Musoma
   (v) Kaliua – Mpanda – Karema

(b) Kuijengea uwezo Kampuni ya Reli Tanzania kwa kuongeza idadi ya vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na abiria ili kuimarisha utendaji wake ikiwa ni pamoja na kuimarisha karakana za Morogoro, Tabora na Dar es Salaam;

(c) Kukamilisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) itakayosaidia kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa Shirika kwa lengo la kuboresha huduma za abiria na mizigo; na

(d) Kuendelea kuboresha usafiri wa reli jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano.

**Usafiri wa Majini**

Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za uchukuzi katika Bandari za mwambao kwa kufanya yatuatayo:-

(a) Kuanza ujenzi wa gati Na. 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam;
(b) Kukamilisha uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 ili kuimarisha utoaji wa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam;
(c) Kuanza ujenzi wa gati la kushusha magari (RoRo) katika Bandari ya Dar es Salaam;
(d) Kuanza ujenzi wa bandari mpya za Bagamoyo na Mwambani Tanga;
(e) Kuanza na kukamilisha ujenzi wa magati manne (4) ya ziada katika Bandari ya Mtwara;

(f) Kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Nyamisati ili kuboresha usafirishaji wa kwenda na kutoka Mafia;

(g) Kuendelea kuboresha Bandari ya Mwanza, upanuzi wa Bandari ya Musoma na ujenzi wa magati ya Ntama, Lushamba na Kiyamkwiki;

(h) Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya bandari za Ziwa Nyasa na Tanganyika ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa kujenga magati ya Kagunga, Kasanga, Kibirizi, Itungi na Kiwira;

(i) Kuboresha mfumo wa uondoshaji mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza kiwango cha utendaji kwa kuweka mfumo wa "electronic window System" na kufunga mita za kupima mafuta; na

(j) Kujenga na kukamilisha meli mbili za abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika, meli moja ya abiria na mizigo katika Ziwa Victoria na meli nyingine ya abiria na mizigo katika Ziwa Nyasa.

**Usafiri wa Anga**

Kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kufanya yatuatayo:-

(a) Kukamilisha mpango kabambe wa usafiri wa anga;

(b) Kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya Jengo la Tatu la JNIA;

(c) Kuanza na kukamilisha ujenzi vya Viwanja vya Ndege vya Shinyanga na Sumbawanga kwa kukarabati barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha lami;

(d) Kujenga na kukamilisha awamu ya pili ya Viwanja vya Ndege vya Tabora na Kigoma;

(e) Kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato kwa kiwango cha Kimataifa;

(f) Kukamilisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza hususan jengo la abiria na kufikia kiwango cha kimataifa;

(g) Kuanza awamu ya pili ya mradi wa ujenzi, ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege kumi na moja (11) vya mikoa vilivyofanyiwa

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina vya Lindi, Kilwa Masoko, Songea, Singida, Lake Manyara, Tanga, Iringa, Njombe, Simiyu, Musoma na Moshi; na

(h) Kuhamasisha uwekezaji wa Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ili kuimarisha huduma za Shirika la Ndege la Taifa.

**Huduma za Hali ya Hewa**

Kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa kwa kufanya yatuatayo:-

(a) Kuanza ujenzi wa kituo kikuu cha utabiri wa hali ya hewa nchini; na

(b) Kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa nchini ili kufikia kiwango cha kimataifa kwa kununua rada za hali ya hewa zisizopungua tano.

**Nishati**

42. Kwa kutambua umuhimu wa nishati kwa maendeleo ya Taifa, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imechukua hatua za kuhakikisha kuwa nishati ya kutosha inapatikana kwa lengo la kukidhi mahitaji ya viwanda, taasisi zinazotoa huduma na wananchi kwa ujumla. Nguvu kubwa imeelekezwa katika kuhakikisha kwamba nishati ya umeme inasambazwa kwa gharama nafuu ili kuwaletea unafuu wa maisha wananchi hasa wale wanaoishi maeneo ya vijijini. Katika kutimiza azma hiyo:-

(a) Mipango ya kuunganisha gridi ya Taifa na nchi jirani imeendelea kutekelezwa kwa lengo la kuimarisha biashara ya umeme. Miradi muhimu ambayo utekelezaji wake unaendelea ni pamoja na:-

(i) Mradi wa Rusumo wa megawati 80 kwa ajili ya Rwanda-Burundi-Tanzania;

(ii) Mradi wa usafirishaji umeme wa gridi ya Kaskazini-Mashariki wa usafirishaji umeme kati ya Ethiopia-Kenya –Tanzania; na

(iii) Mradi wa Zambia - Tanzania-Kenya (ZTK Interconnector).

(b) Kiwango cha uunganishwaji umeme kwenye Mikoa na Wilaya ambako gridi ya Taifa haijafika nchini kimeongezeka kutoka asilimia 5 mwaka 2010 hadi asilimia 36 mwaka 2015. Aidha, kiwango cha uunganishwaji umeme vijijini kimeongezeka kutoka asilimia 5 mwaka 2010 hadi

asilimia 7 mwaka 2014 kupitia utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini wenye miradi midogo 41 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara (Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga) ambapo jumla ya wateja wapya 209,237 wameunganishiwa umeme hadi kufikia Disemba, 2014;

(c) Ukiritimba wa TANESCO wa kuwa mzalishaji na msambazaji pekee wa umeme umeondolewa na sasa sekta binafsi imeruhusiwa kushiriki katika kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme;

(d) Ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa km 542 kutoka Mnazi Bay (Mtwara) hadi Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi katika eneo la Somanga Fungu, Kinyerezi Dar es Salaam na Tegeta umefikia wastani wa asilimia 96;

(e) Jumla ya futi za ujazo trilioni 55.08 za gesi imegunduliwa nchini hadi kufikia mwaka 2015;

(f) Jumla ya nyumba za makazi 812, nyumba za ibada 27, shule 6 na zahanati 8 zimepatiwa umeme wa jua pamoja na jumla ya taa za mitaani 200 katika vijiji 10 kutoka Wilaya za Mlele, Kongwa na Uyui kupitia Mradi wa Maendeleo ya Nishati *(Tanzania Energy Development and Access Expansion – TEDAP)*; na

(g) Mradi wa usambazaji gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali umeshaanza ambapo maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi yamekamilika na kwa sasa shughuli za upanuzi zinaendelea.

43. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya 2015–2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuongeza kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa nishati ili kuendelea kukuza Sekta hiyo na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa kwa kutekeleza yafuatayo:-**

**Umeme**

(a) Kuongeza uzalishaji wa umeme ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma hii kulingana na Sera ya Nishati ya Taifa.

Kwa kutekeleza miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme *(Power System Master Plan – 2009-2033*) ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini, kipaumbele kitatolewa katika rasilimali za makaa ya mawe, maji *(hydro),* gesi asilia na nishati jadidifu *(renewable energy)* ambapo lengo ni kufikia MW 4,915 mwaka 2020 kutoka MW 1,308 mwaka 2015; na

(b) Kukamilisha na kuimarisha mtandao wa usafirishaji na usambazaji umeme (*National Grid*) unaounganisha nchi nzima kwa kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi yetu. Miradi hiyo ni pamoja na:-

(i) Mradi wa *Backbone* wa kV 400 unaounganisha mikoa ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga wenye urefu wa km 670;

(ii) Mradi wa Makambako-Songea wa kV 220, ambao unaunganisha mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma km 250; na

(iii) Mradi wa Kaskazini-Mashariki *(North-East)* unaounganisha mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, mradi mwingine muhimu ni ule wa Kaskazini-Magharibi *(North-West),* ambao unaunganisha mikoa ya Mbeya, Katavi, Rukwa na Kigoma.

(c) Kuendelea kusambaza umeme wenye uhakika mijini na vijijini kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuongeza bajeti ya Wakala wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA) ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wenye uhakika;

(ii) Kukamilisha utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango kabambe wa kupeleka umeme vijijini *(REA Turn-Key Projects Phase II)* yenye lengo la kuunganisha wateja 250,000 utakapokamilika; na

(iii) Kuanzisha REA (III) ambayo ina malengo yaafuatayo:-

- Kuongeza wigo wa usambazaji umeme kutoka REA I na II zilipoishia;
- Kufikisha umeme kwenye shule zote za sekondari, hospitali na vyanzo vya maji;
- Kuongeza idadi ya vijiji ambavyo vinafikiwa na umeme; na
- Kupeleka umeme maeneo yote ambayo si tija kwa TANESCO kuwekeza.

(iv) Kuongeza kiwango cha uunganishaji umeme *(connection level)* kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 60 ifikapo mwaka 2020; na

(v) Kutekeleza miradi ya kuunganisha gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani ambapo miradi ya Zambia-Tanzania-Kenya, Burundi-Rwanda-Tanzania na Tanzania-Kenya-Ethiopia itahusika.

**Mafuta na Gesi Asilia**

44. **Kwa kuzingatia ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi asilia na matarajio ya upatikanaji wa mafuta, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuielekeza Serikali kusimamia sekta hii kwa kuzingatia Sera na Sheria mbalimbali zilizopo zitakazowezesha nchi kunufaika na rasilimali hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na kutekeleza Sera na Sheria hizo, malengo muhimu katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 ni pamoja na:-**

(a) Kuwezesha na kusimamia ujenzi wa miundombinu muhimu ya gesi asilia na mafuta nchini pamoja na kukamilisha Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia *(Natural Gas Utilisation Master Plan*);

(b) Kuhakikisha wananchi wanaopakana na miundombinu ya gesi na ambako bomba la gesi linapita wanashiriki na kunufaika na gesi;

(c) Kuwawezesha wananchi kwa ujumla washiriki na wanufaike na fursa zinazotokana na uchumi wa gesi;

(d) Kuendeleza mradi wa kugeuza gesi kuwa katika hali ya vimiminika *(Liquefied Natural Gas - LNG)* ili kuwezesha mauzo ya gesi asilia ndani na nje ya nchi;

(e) Kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kushiriki katika sekta ndogo ya mafuta na gesi kwa kuzingatia Sera na Sheria zilizopo;

(f) Kuendelea kuhamasisha utafutaji wa mafuta na gesi asilia;

(g) Kuendelea kusomesha vijana wa Kitanzania katika ngazi mbalimbali za vyuo vikuu, VETA, kulingana na mahitaji ya rasilimali watu katika Sekta ya Mafuta na Gesi; na

(h) Kuendelea kusimamia ujenzi wa miundombinu muhimu ya mafuta na gesi nchini ili kuleta ufanisi na tija katika kuvuna na kutumia mafuta na gesi asilia.

(i) Kwa kutambua umuhimu wa nishati ya mafuta, Serikali:-

    (i) Itahakikisha hifadhi za kimkakati zenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya mafuta kwa nchi yetu na nchi jirani zinajengwa Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar;

    (ii) Itahamasisha sekta binafsi kutumia fursa ya kijiografia kuigeuza Dar es Salaam kuwa soko kubwa la mafuta ya jamii ya petroli kwa ukanda wa Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara;

    (iii) Itahakikisha wakati wote sehemu zote za nchi zinapata mafuta yenye ubora unaokidhi viwango na kwa bei inayoakisi gharama halisi kupitia Taasisi zake (TPDC, EWURA na Wizara ya Nishati na Madini); na

    (iv) Itahimiza matumizi ya gesi ya Petroli *(Liquefied Pretroleum Gas -LPG)* na gesi asilia katika matumizi ya nyumbani na viwandani ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kuhifadhi mazingira.

**Nishati Jadidifu na Matumizi Bora ya Nishati**

45. **Kwa kuzingatia kwamba gesi asilia na makaa ya mawe ni rasilimali zinazoisha *(depletable),* na kwa kuzingatia madhara ya mabadiliko ya tabianchi, Chama Chama Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuwekeza nguvu kubwa katika kuzalisha nishati jadidifu kwa kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuzalisha umeme wa jua usiopungua MW 180; Joto ardhi MW 200 kwa kuzigatia uwezo uliopo wa kuzalisha hadi MW 5000;

(b) Kuzalisha umeme MW 100 kwa kutumia nguvu za upepo kufikia mwaka 2020; na

(c) Kufanya tafiti ili kubaini na kupanga vyanzo mbadala kwa miaka ijayo ili kuepusha Taifa kukosa nishati ya umeme.

**Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

46. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imekuwa katika jitihada za kuendeleza utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuinua Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ili kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika kipindi hicho, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Kuimarisha Utendaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kuhakikisha:-

(i) Sheria ya Tume imepitiwa upya ili kuipa COSTECH mamlaka ya kiudhibiti pamoja na kutambua mchango wa ubunifu; na

(ii) COSTECH imeanzisha taasisi za kuwakuza wajasiriamali wa TEHAMA ikiwemo ya *Dar Teknohama Incubator* (DTBi) ambapo matokeo yake yamechangia kuanzishwa kwa mfumo wa MAXMALIPO.

(b) Jumla ya watafiti 517 wamesomeshwa katika ngazi ya shahada ya Uzamili na Uzamivu katika vyuo vikuu vya hapa nchini katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2014;

(c) Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 wagunduzi 11 walipewa Tuzo ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (TASTA). Aidha, Taasisi nane (8) zilipewa Tuzo za Utafiti wa Sayansi na

Teknolojia (NARST) na Taasisi mbili (2) zimepatiwa Tuzo za Mazingira (NAEM);

(d) Ujenzi wa awamu ya I na II ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu kilometa 7,560 umekamilika na umesaidia watoa huduma kufikisha huduma za mawasilianao kwa wananchi kwa uharaka zaidi, uhakika na kwa gharama nafuu. Kuwepo kwa mkongo mmoja unaomilikiwa na Serikali umepunguza gharama za huduma ya mawasiliano ambapo:-

   (i) Gharama kwa mtumiaji wa mwisho zimeshuka kutoka Shilingi 147 kwa dakika mwaka 2009 hadi Shilingi 67 kwa dakika mwaka 2014; na

   (ii) Ada ya kuunganisha simu za mikononi imeshuka kutoka Shilingi 115 kwa dakika mwaka 2009 hadi Shilingi 34.92 kwa dakika mwaka 2014.

(e) Mfumo wa kusimamia mawasiliano umewekwa ili kubaini takwimu zinazopita katika mitandao ya mawasiliano kwa kutambua mapato na miamala ya fedha, kufuatilia na kugundua mawasiliano ya ulaghai na kutambua taarifa za laini za simu na za kifaa cha mawasiliano;

(f) Zoezi la kuhamisha matangazo kutoka mfumo wa analojia kwenda katika utangazaji wa Digiti awamu ya kwanza limekamilika; na

(g) Idadi ya wananchi wanaomiliki simu za kiganjani imeongezeka kutoka milioni 2.9 mwaka 2005 hadi milioni 32.01 mwaka 2015.

47. **Mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda ambavyo Taifa linataka yafanyike ili kuleta mageuzi ya uchumi, yatawezekana kwa kuwekeza vema katika ujenzi wa msingi imara wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika sekta mbalimbali yatasaidia uchumi wetu kukua kwa kasi na kuwapunguzia wananchi umasikini pamoja na kuongeza ajira.**

**Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha miaka mitano ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015-2020, itaweka msisitizo mkubwa wa vipaumbele kama ifuatavyo:-**

(a) Kuanzisha vituo vya ubunifu ili kukuza makampuni ya TEHAMA yanayoibukia kwa lengo la kuongeza ajira kwa vijana;

(b) Kuandaa mazingira bora ya kusambaza matokeo ya utafiti na teknolojia kwa watumiaji katika sekta za uzalishaji hususan kilimo, mifugo, uvuvi na afya;

(c) Kuendeleza matumizi ya teknolojia ya nyuklia katika tiba ya saratani na kuongeza vituo kutoka vituo viwili (2) vya sasa hadi sita (6) vitakavyohudumia kanda mbalimbali nchini, vituo vinne vitakavyoongezwa ni: Hospitali ya Rufaa Mbeya, Mnazi Mmoja (Zanzibar), KCMC pamoja na Dodoma;

(d) Kuunganisha katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano baadhi ya shule za msingi, shule zote za sekondari, ofisi zote za wakuu wa wilaya/polisi (OCD), hospitali zote za wilaya, vyuo vikuu vyote na vituo vya posta 65 ili kuweza kutumia fursa za TEHAMA hususan Elimu Mtandao, Maktaba Mtandao na Afya Mtandao;

(e) Kuanzisha kituo mahiri cha huduma za TEHAMA kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kuhawilisha teknolojia na kutoa ajira kwa Watanzania;

(f) Kufikisha huduma za mawasiliano ya simu za viganjani kwa wananchi wote kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) katika vijiji vyote vya Tanzania Bara na Zanzibar;

(g) Kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye Sekta ya Mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za mawasiliano ya simu;

(h) Kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya Pato Ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya utafiti, maendeleo na maonyesho ya matokeo ya utafiti;

(i) Kuwalinda watumiaji wa simu za mikononi dhidi ya dhuluma, wizi na uhalifu wa mitandao; na

(j) Kuongeza idadi ya watumiaji mitandao (internet) kutoka milioni 9.0 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 20.0 mwaka 2020.

## SURA YA NNE
## SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

48. Huduma bora za jamii kama afya, elimu, maji na nyinginezo ni nyenzo muhimu katika kuondoa umasikini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali chini ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi imeendeleza jitihada za kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kunufaika na huduma hizo. Kwa hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi kilichopita ili wananchi waendelee kunufaika na huduma za jamii ambazo ni za msingi katika jitihada za kuboresha maisha yao.

### Afya

49. Ili kujenga Taifa lenye watu wenye afya bora inayowawezesha kuzalisha mali na kutoa huduma mbalimbali, katika kipindi cha mwaka 2010-2015, Serikali iliendelea kuyapa kipaumbele maeneo yaliyoainishwa katika MKUKUTA na Malengo ya Milenia ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Vituo vya kutolea huduma ya Afya vimeongezeka kutoka 6,260 mwaka 2010 hadi vituo 7,014 mwaka 2015. Pia kuna kliniki 89 zinazohamishika (huduma za mkoba) katika mfumo wa utoaji wa huduma za wazazi, meno, macho, moyo na sukari ambazo huendeshwa na madaktari bingwa;

(b) Udahili wa wanafunzi watarajali umeongezeka kutoka 7,013 mwaka 2010 hadi wanafunzi 11,192 mwaka 2015 katika Vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii;

(c) Waajiriwa wapya wa kada za afya wameongezeka kutoka 7,471 mwaka 2010 hadi waajiriwa 9,345 mwaka 2014;

(d) Kupitia mpango wa hati punguzo, vyandarua 8,753,438 vyenye viuatilifu kwa ajili ya kaya zenye watoto chini ya miaka mitano, vyandarua 7,785,787 kwa ajili ya wajawazito na vyandarua 4,960,111 kwa ajili ya watoto chini ya umri wa mwaka mmoja

vimesambazwa bure kwa lengo la kuboresha tiba ya malaria, kudhibiti mbu na kutoa kinga. Aidha, vyandarua 26,371,329 viligawiwa kwa wananchi bila malipo kupitia kampeni zilizolenga watoto chini ya miaka mitano na ngazi ya Kaya. Matokeo yake ni:-

(i) Vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kutoka 33 mwaka 2010 hadi 12 kwa kila watu 1,000 mwaka 2014; na

(ii) Idadi ya watu waliopatikana na malaria imepungua kutoka watu 310 mwaka 2010 hadi 161 kwa kila watu 1,000 mwaka 2014.

(e) Mpango wa Upuliziaji wa viuatilifu ukoko katika kuta ndani ya nyumba ili kuua mbu wanaoeneza malaria umetekelezwa kwa mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na Geita ambapo zaidi ya kaya 1,440,000 zenye watu 6,500,000 zilinufaika;

(f) Ujenzi wa kiwanda cha viuadudu (bio-larvicides) katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa lengo la kuzalisha viuadudu kwa ajili ya kudhibiti viluwiluwi vya mbu nchini umekamilika ambapo Kata za Jiji la Dar es Salaam zimeanza kunufaika;

(g) Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) ilitoa huduma za kibingwa za mkoba kwa wagonjwa 513 ambapo wagonjwa 116 walifanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro;

(h) Hospitali za Rufaa za Mikoa 24 zimeunganishwa kwenye mtandao wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano ili kutoa huduma za afya kwa njia ya mtandao;

(i) Vifaa vya kujimudu kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na shime sikio, viti mwendo, mashine za nukta nundu na fimbo nyeupe kwa ajili ya makazi 17 ya wazee, wasiojiweza na vyuo viwili vya ufundi vimenunuliwa. Jumla ya wazee 1,750 walipatiwa huduma katika makazi 17 yanayomilikiwa na Serikali na 24 yanayomilikiwa na wakala wa hiari;

(j) Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuhakikisha kuwa dawa na vifaa tiba vinapokosekana

katika bohari zake, Mshitiri/Mnunuzi wa Sekta Binafsi anakuwa tayari kuwezesha upatikanaji wa dawa hizo kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini;

(k) MSD imeanza kupeleka shehena za dawa moja kwa moja hadi vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili kuboresha usambazaji dawa na kupunguza gharama;

(l) Jumla ya Wataalamu 1,553 wa Sekta ya Afya katika ngazi ya Halmashauri wamepata mafunzo ya uingizaji na utumiaji wa taarifa kupitia mfumo wa elektroniki ili kufanikisha upatikanaji wa takwimu za afya ambapo jumla ya kompyuta 133 kwa ajili ya Halmashauri na Mikoa; na kompyuta 189 kwa ajili ya matumizi ya mfumo wa hospitali za Mikoa na Wilaya zilitolewa;

(m) Watanzania 4,010,844 sawa na asilimia 9.2 wamejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kufikia mwaka 2015. Aidha, asilimia 19.2 ya Watanzania wamefikiwa na huduma za bima kwa kujumuisha mifuko yote ya Bima za Afya;

(n) Huduma za matibabu ya kibingwa na uchunguzi zimeimarishwa. Huduma hizo ni pamoja na upasuaji mkubwa wa moyo; upasuaji wa mgongo na ubongo; kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo; kuanzishwa kwa huduma ya matibabu ya dharura katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (Emergency Medicine); na kununua mashine za mionzi. Aidha, hadi sasa jumla ya wagonjwa 671 walipata huduma ya upasuaji mkubwa wa moyo; wagonjwa 211 walifanyiwa upasuaji maalumu: ubongo 29, mgongo 107, 56 waliwekewa viungo bandia vya nyonga na 19 viungo bandia vya goti; na

(o) Mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto umeanzishwa. Hadi sasa akina Mama walioanzishiwa tiba ya maisha ni 72,207 kati ya mama wajawazito wa VVU watarajiwa 97,908. Mpango huu umewezesha kiwango cha maambukizi kupungua kutoka asilimia 8 mwaka 2010 hadi asilimia 5 mwaka 2015.




*Moja ya ghala la Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya kuhifadhi Dawa katika Kanda*

50. **Kwa kuzingatia dhamira ya kuwa na wananchi wenye afya bora watakaoweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kutoa huduma katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya kwa kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendeleza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) wenye lengo la kuimarisha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kuhakikisha kwamba:-

(i) Lengo la kila kijiji kuwa na Zahanati, Kata kuwa na Kituo cha Afya na Wilaya kuwa na Hospitali linaendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo huduma hizi hazijakamilika pamoja na kujenga hospitali za wilaya katika wilaya zote mpya;

(ii) Hospitali za Rufaa za Mikoa zinaendelea kuimarishwa na kukamilisha ujenzi kwa mikoa mipya na ile ambayo haina hospitali hizi;
(iii) Kujenga hospitali katika wilaya mpya;
(iv) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Afya kwa kupitia sera ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP);
(v) Hospitali za Rufaa za Kanda zitaendelea kuimarishwa na kujenga hospitali nyingine tatu kwa ajili ya Kanda ya Kusini, Kati na Magharibi;
(vi) Kudahili wanafunzi 15,000 katika Vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii ifikapo mwaka 2020 ikiwa ni jitihada za kutosheleza mahitaji ya rasilimali watu katika sekta hii;
(vii) Kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu katika vyuo vya mafunzo ya afya na kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji wa vyuo;
(viii) Kuajiri wataalamu zaidi wa afya kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma za afya. Aidha, hospitali za wilaya zitaendelea kuimarishwa kwa kuzipatia madaktari, wauguzi, dawa na vifaa tiba vya kutosha;
(ix) Kutoa motisha kwa watumishi ambao wanafanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwajengea ushawishi wa kuendelea kutoa huduma za afya katika maeneo hayo; na
(x) Kujenga nyumba za watumishi karibu na vituo vya kutolea huduma.

(b) Kuimarisha mapambano dhidi ya malaria kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwagawia wananchi vyandarua vyenye viuatilifu 22,360,386 bila malipo;
(ii) Kutekeleza mpango wa upuliziaji wa viuatilifu ukoko katika kuta za nyumba ili kuua mbu wanaoeneza malaria katika mikoa ya Kigoma na Lindi;

(xi) Kuendelea kutekeleza mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwa kutumia viuadudu vya kibailojia katika Kata za Jiji la Dar es Salaam; na

(xii) Kununua na kusambaza dawa za malaria katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini.

(c) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za dharura na za kawaida kwa wagonjwa kupitia vituo vya huduma za afya hapa nchini. Huduma hizi ni pamoja na magonjwa ya saratani, mishipa ya fahamu, mapafu, figo, huduma za magonjwa ya moyo, upasuaji mbalilmbali ikiwamo upasuaji wa mifupa;

(d) Hospitali ya Taifa Muhimbili itaendelea kutoa huduma za kibingwa za mkoba katika Hospitali za Rufaa za Kanda;

(e) Kuunganisha hospitali za rufaa za Mikoa na Wilaya na hospitali nyinginezo kwenye mfumo wa matibabu mtandao (telemedicine);

(f) Halmashauri za Wilaya zitaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kununulia vifaa vya kujimudu kwa lengo la kuwawezesha watu wenye ulemavu;

(g) Bohari ya Dawa itakamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika mikoa ya Tanga, Tabora, Mtwara na Dar es Salaam. Aidha, Serikali itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi kuwezesha upatikanaji wa dawa pale zinapokosekana katika Bohari ya Dawa;

(h) Kuongeza Washitiri Binafsi 17 katika mikoa tisa kwa ajili ya ununuzi wa dawa pale ambapo hazipo Bohari ya Dawa;

(i) Kuunganisha mifumo ya ukusanyaji na utoaji taarifa za afya ili kufikia lengo la kuwa na mfumo mmoja unaokusanya na kutoa taarifa za afya nchini. Aidha, mfumo wa ukusanyaji taarifa kwa njia ya simu za mkononi utasambazwa nchi nzima;

(j) Kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kuwa na Bima ya Afya ili kumudu gharama za matibabu;

(k) Kuimarisha huduma za matibabu ili kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kununua mashine za mionzi (LINAC machine) kwa ajili ya tiba ya saratani;

(ii) Kununua vifaa vya kisasa na kuwajengea uwezo wataalam ili kuhudumia wagonjwa wengi wa moyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na hospitali za rufaa za Kanda;

(iii) Kununua mashine za mionzi (CT-Scan, MRI) kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji wa mgongo na ubongo; na

(iv) Kuimarisha mtandao wa Hospitali za Taifa pamoja na Huduma za Ubingwa wa Juu zikiwemo zile za upasuaji wa moyo; huduma kwa wagonjwa wa saratani; upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu na upasuaji kupitia tundu dogo kwa kutumia kifaa maalumu ikiwa ni pamoja na kuchuja damu na kupandikiza figo kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo.

(l) Kupanua huduma za matibabu mtandao (telemedicine) pamoja na zile za kutumia mtandao wa simu pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi yatakayowawezesha kutoa huduma za kibingwa. Aidha, vituo vingine vya saratani vitaongezwa katika hospitali ya KCMC na hospitali ya rufaa ya Mbeya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi;

(m) Kukamilisha ujenzi wa hospitali za Mloganzila, Mtwara na Chuo Kikuu cha Dodoma;

(n) Kukarabati na kuimarisha huduma za kibinadamu katika vituo vya kutolea huduma za ustawi wa jamii vikiwemo makazi 17 ya wazee, mahabusi saba za watoto walio katika mkinzano na sheria pamoja na shule moja ya maadilisho;

(o) Kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za makundi maalumu wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi (albinism) na watoto wanaoishi mitaani ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Mtoto katika Halmashauri zote;

(p) Kukamilisha Sera ya Huduma za Ustawi wa Jamii pamoja na Mkakati wake wa Utekelezaji. Aidha, Halmashauri zitahakikisha wazee wanatambuliwa na kupewa matibabu bure katika hospitali za Serikali;

(q) Kuimarisha Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto kwa kuzingatia vipaumbele vya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuzijengea uwezo Hospitali na Vituo vya Afya ili kutoa huduma kamili ya Afya ya Uzazi na Mtoto pamoja na upasuaji kwa mama wajawazito;

(ii) Kuanzisha Benki za Damu katika Mikoa itakayoanza kutekeleza mpango wa kutoa huduma kamili ya afya ya uzazi na mtoto. Vilevile, huduma za uzazi wa mpango zitapewa kipaumbele;

(iii) Kuzijengea uwezo Zahanati na Vituo vya Afya katika mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Kigoma kutoa huduma ya msingi ya dharura ya Afya ya Uzazi na Mtoto;

(iv) Kutoa huduma za mkoba (mobile clinic) hasa maeneo ya vijijini; na

(v) Kuendelea kutekeleza mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto.

**Elimu**

51. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha, kuimarisha na hata kupanua Elimu ya Awali hadi ya Chuo Kikuu kwa lengo la kuhakikisha kwamba elimu katika ngazi zote inakuwa na ubora unaostahili ili kuwawezesha vijana na makundi mengine kumudu ushindani wa soko la ajira ambalo wigo wake umepanuka ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) **Elimu ya Awali**

(i) Idadi ya shule za msingi zenye madarasa ya Elimu ya Awali imeongezeka kutoka shule 10,612 mwaka 2010

hadi shule 14,783 ambayo yana walimu 13,600 mwaka 2015;

(ii) Stashahada ya Elimu ya Awali ya miaka miwili katika vyuo 19 vya serikali imeanzishwa kwa lengo la kupata walimu wenye weledi wa juu katika ngazi ya Elimu ya Awali; na

(iii) Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka 128,847 mwaka 2006 hadi 157,162 mwaka 2013.

(b) **Elimu ya Msingi**

(i) Katika kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa walimu wa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi, vigezo vya kujiunga na mafunzo ya ualimu vimepandishwa hadhi kutoka ufaulu wa daraja la nne hadi kuanzia ufaulu wa daraja la kwanza mpaka daraja la tatu kwa waliofaulu masomo hayo;

(ii) Kupitia mpango wa kuwajengea uwezo walimu na mwanafunzi, jumla ya walimu 9,814 katika Halmashauri 40 wakiwemo walimu 3,272 wa somo la Hisabati na 3,272 wa somo la Kiingereza wamejengewa uwezo wa kuyamudu masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha. Aidha, Stashahada ya Elimu ya Msingi imeanzishwa katika vyuo vinne (4) UDOM, Morogoro, Bustani na Marangu vyenye uwezo wa kudahili walimu tarajali 713 kwa mwaka ili kuandaa walimu mahiri watakaofundisha Elimu ya Msingi;

(iii) Maslahi ya walimu yameendelea kuboreshwa kulingana na ukuaji wa uchumi;

(iv) Madai mbalimbali ya walimu yameendelea kulipwa baada ya kuhakikiwa;

(v) Ruzuku ya Wanafunzi (Capitation Grants) imeendelea kutolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zote za Serikali nchini;

(vi) Stashahada ya Elimu ya Msingi katika vyuo vitatu (3), Stashahada ya Juu ya Elimu masomo ya Sayansi katika vyuo vitatu (3), Stashahada ya Juu ya Elimu masomo la Lugha katika chuo kimoja (1) na Stashahada ya Elimu ya Michezo katika chuo kimoja (1) zimeanzishwa ili kuweza kuandaa walimu mahiri watakaofundisha Elimu ya Msingi kwa kuwajengea uwezo wa kumudu maarifa na stadi muhimu katika kutekeleza mitaala kwa ufanisi;

(vii) Uandikishaji wa watoto wa miaka 7-13 umeongezeka kutoka wanafunzi 6,499,581 mwaka 2005 hadi wanafunzi 7,679,877 mwaka 2013;

(viii) Idadi ya uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu imeongezeka kutoka wanafunzi 27,422 mwaka 2009 hadi wanafunzi 31,488 mwaka 2013;

(ix) Jumla ya shule za msingi 7,165 sawa na asilimia 37.4 zilikaguliwa mwaka 2013 kwa lengo la kuboresha kiwango cha elimu;

(x) Idadi ya walimu walioajiriwa imeongezeka kutoka 135,013 mwaka 2005 hadi 189,487 mwaka 2013;

(xi) Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi umeimarika kutoka uwiano mwalimu mmoja wanafunzi 56 (1:56) mwaka 2005 hadi uwiano wa mwalimu mmoja wanafunzi 43 (1:43) mwaka 2013;

(xii) Uwiano wa kitabu kwa wanafunzi umeboreshwa kutoka kitabu kimoja wanafunzi saba (1:7) mwaka 2010 kufikia wastani wa kitabu kimoja wanafunzi watatu (1:3) mwaka 2014;

(xiii) Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka kutoka 38,448 mwaka 2006 hadi 161,007 mwaka 2013; na

(xiv) Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na Elimu ya Sekondari (Kidato cha Kwanza) imeongezeka kutoka wanafunzi 403,873 sawa na aslimia 84.3 mwaka

2010 hadi 451,392 mwaka 2015 sawa na asilimia 100.

(c) **Elimu ya Sekondari**


(i) Idadi ya walimu wa sekondari imeongezeka kutoka 40,517 mwaka 2010 hadi walimu 80,529 mwaka 2014 na hivyo kufikia uwiano Kitaifa wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 22 (1:22);

(ii) Walimu wa masomo ya Sayansi za Jamii wameongezeka hadi kufikia 52,816 mwaka 2014 na hivyo kuwa na ziada ya walimu 2,960 ikilinganishwa na mahitaji ya walimu 49,856 wa fani hizo;

(iii) Walimu wa Sayansi na Hisabati wameendelea kupatiwa mafunzo ili kuboresha fani hizo ambapo vifaa vya maabara na kemikali vyenye thamani ya Shilingi milioni 327.7 vimenunuliwa na kusambazwa. Aidha, jumla ya vitabu milioni 4,485,530 vya sayansi vimenunuliwa na kusambazwa katika shule mbali mbali nchini;

(iv) Hadi kufikia mwaka 2014, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari awamu ya pili (MMES II), mafunzo ya Sayansi na Hisabati yametolewa kwa walimu 9,004 katika mzunguko wa mada za mwanzo na walimu 7,863 kwa mzunguko wa mada za pili na walimu 182 wameanza mzunguko wa mada za tatu; na

(v) Idadi ya maabara imeongezeka kutoka 1,478 mwaka 2005 hadi 4,237 mwaka 2015 na maabara 5,974 zipo katika hatua mbalimali za ujenzi.




*Mwenyekiti wa CCM, Rais Jakaya Mrisho Kikwete akisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa wanafunzi wa shule za Sekondari wakati wa uzinduzi wa moja ya Maabara zilizokamilika kujengwa.*

(d) **Elimu ya Ualimu**

(i) Mafunzo tarajali ya walimu wa Shule za Msingi watakaofundisha masomo mawili yameanza kutolewa ambapo wanachuo 1,964 wa Diploma ya Juu ya Elimu ya Sekondari na wanachuo 178 wa Diploma ya Sayansi wa Shule za Msingi wamedahiliwa kwa mwaka 2014/15 katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(ii) Kati ya mwaka 2010 na 2015, wakufunzi 331 wa Vyuo vya Ualimu walipatiwa mafunzo ya namna ya kutumia

TEHAMA katika kufundisha na kujifunza. Aidha, vyuo vyote vya ualimu (34) vimepatiwa kompyuta na hivyo kuwapatia fursa wakufunzi kuandaa mada zao na maandiko mengine kwa kutumia teknolijia hiyo;

(iii) Jumla ya Shilingi bilioni 4.3 zimetumika kukarabati miundombinu ya vyuo vya Ualimu Patandi, Bustani na Vikindu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia; na

(iv) Maabara za Vyuo vya Ualimu vyenye mchepuo wa Sayansi zimeboreshwa kwa kuzinunulia vifaa vyenye thamani ya Shilingi milioni 379.8 katika maabara na kemikali za masomo ya Sayansi (Fizikia, Kemia na Biolojia) katika vyuo saba vya Ualimu vya Korogwe, Kleruu, Butimba, Songea, Tukuyu, Monduli na Morogoro.

(e) **Elimu ya Juu**

(i) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu wa mwaka 2010 umeandaliwa na utekelezaji wake umechangia wanafunzi wa kidato cha sita wanaojiunga na Vyuo Vikuu kuongezeka kutoka wanafunzi 34,564 mwaka 2009/2010 hadi wanafunzi 40,452 mwaka 2014/2015 sawa na asilimia 14.6;

(ii) Utaratibu wa utoaji na urejeshwaji mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu umeboreshwa ambapo:-

- Dawati la Mikopo limeanzishwa katika kila Chuo;
- Idadi ya wanafunzi ambao wamepata mikopo imeongezeka kutoka wanafunzi 72,035 mwaka 2009/2010 hadi kufikia 99,928 Mwezi Machi, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 27.9; na
- Utaratibu wa urejeshaji wa makopo umeendelea kuboresha ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 jumla ya Shilingi bilioni 75.57 zemerejeshwa kati ya Shilingi bilioni 165.0 ya mikupuo inayopaswa kuwa imerejeshwa.

Makusanyo haya ni asilimia 45.4 ya kiwango kinachopaswa kuwa kimekusanywa.

(iii) Bajeti kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu imeendelea kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 186.48 mwaka 2010 hadi Shilingi bilioni 328.313,44 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asimia 43.2;

(iv) Ujenzi na ukarabati wa majengo mapya 25 kwa ajili ya kumbi za mihadhara, maabara na ofisi za wafanyakazi katika vyuo vikuu vya UDSM, OUT, DUCE, MUCE, SUA, DIT na ARU umekamilika na utaongeza nafasi za kusomea wanafunzi hadi kufikia 47,622;

(v) Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika Vyuo Vikuu imeongezeka kutoka wanafunzi 139,638 mwaka 2010 hadi kufikia wanafunzi 218,959 mwaka 2014 sawa na asilimia 36.2;

(vi) Idadi ya wanafunzi wa kike wanaosoma Elimu ya Juu imeongezeka kutoka wanafunzi 53,376 kati ya wanafunzi 141,671 waliodahiliwa mwaka 2010/11 hadi kufikia wanafunzi 78,800 kati ya wanafunzi 218,959 waliodahiliwa mwaka 2014/2015;

(vii) Taasisi 23 za Elimu ya Juu kati ya 32 zimeunganishwa katika Mkongo wa Taifa ili kuimarisha ufundishaji na uendeshaji wa elimu kwa njia ya mtandao hadi kufikia mwaka 2015;

(viii) Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vimeanza kutoa mafunzo kwa njia ya masafa baada ya kuunganishwa na Mkongo wa Taifa na kuwezesha wahadhiri kutoa elimu kwa njia ya masafa na kuweza kuwafikia wanafunzi wengi mikoani; na

(ix) Idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vimeongezeka kutoka 19 mwaka 2010 hadi 49 mwaka 2015.

(f) **Elimu ya Mafunzo ya Ufundi**

(i) Vyuo vya Ufundi Stadi vimeongezeka kutoka vyuo 672 mwaka 2010 hadi kufikia vyuo 755 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la aslimia 12.35;

(ii) Vyuo vya Elimu ya Ufundi vimeongezeka kutoka 240 mwaka 2010 hadi 473 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 97.08;

(iii) Udahili wa wanachuo katika Vyuo vya Ufundi Stadi umeongezeka kutoka wanachuo 78,586 mwaka 2010 hadi kufikia wanachuo 145,511 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 85.16;

(iv) Udahili katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo umeongezeka kutoka wanachuo 85,040 mwaka 2010 hadi wanachuo 113,080 mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 33.81; na

(v) Udahili wa wasichana katika Vyuo vya Ufundi Stadi umeongezeka kutoka 52,154 mwaka 2010 hadi 56,849 mwaka 2014. Aidha, udahili wa wasichana katika vyuo vya Elimu ya Ufundi umeongezeka kutoka 38,698 mwaka 2010 kufikia 53,891 mwaka 2014.

(g) **Elimu ya Watu Wazima yenye Manufaa**

(i) Idadi ya wanafunzi wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana (ODL) imeongezeka kutoka wanafunzi 5,767 mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi 9,399 mwaka 2013; na

(ii) Jumla ya watu wazima 907,771 (wanaume 434,466 na wanawake 473,305) wamejiunga na Elimu ya Watu Wazima na kujifunza Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK), na kujifunza fani nyingine za kilimo, ufundi, ufugaji na usindikaji wa bidhaa mbalimbali ambapo wameweza kuongeza fursa za kujiajiri.

52. **Elimu ya kisasa na hasa yenye mwelekeo wa Sayansi na Teknolojia ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Kwa kutambua ukweli huu, CCM inaipa kipaumbele Sekta ya Elimu**

**umuhimu wa kipekee ili kuiendeleza sekta hii. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha Serikali inasimamia Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuandaa mfumo, muundo na taratibu nyumbufu za kutoa Elimu ya Awali na Elimumsingi (1+6+4) bila malipo ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Uandikishwaji rika lengwa la watoto wa darasa la Elimu ya Awali unaongezeka kutoka asilimia 45 mwaka 2015 hadi asilimia 100 mwaka 2020;

(ii) Uandikishwaji rika lengwa la watoto wa Darasa la Kwanza unaongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2015 hadi asilimia 100 mwaka 2020; na

(iii) Uandikishwaji rika lengwa la Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza unaongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi asilimia 80 mwaka 2020.

(b) Kuhuisha taratibu za kujiunga na taasisi zinazotoa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa kutambua sifa zinazopatikana katika mifumo na taasisi tofauti ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Asilimia 20 ya wahitimu wa Elimumsingi wanaendelea na masomo katika ngazi za Sekondari ya Juu na asilimia 80 kuendelea na elimu au mafunzo ya ufundi katika ngazi ya cheti, stashahada au shahada kulingana na sifa, vipaji au vipawa;

(ii) Asilimia 80 ya wahitimu wa Elimu ya Sekondari ya Juu kujiunga na Elimu ya Juu ya Taaluma na asilimia 20 kuendelea na Elimu ya Ufundi, katika ngazi ya cheti, stashahada au shahada kulingana na sifa; na

(iii) Asilimia 70 ya wahitimu wa Elimu au Mafunzo ya Ufundi na Taaluma wanapata ajira kwa kujiajiri au kuajiriwa.

(c) Kudurusu na kuhuisha muundo wa mitaala ili elimu katika ngazi mbalimbali ikamilike kwa muda wenye tija na itilie maanani

matokeo ya kusoma yenye kujenga ujuzi, maarifa ya kujitegemea, weledi na kuwawezesha wahitimu kumudu na kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa au kujiajiri;

(d) Kuhuisha vigezo na utaratibu wa kuhakiki, kusimamia na kupima utekelezaji wa mitaala katika shule na taasisi za elimu na mafunzo katika ngazi zote ili kuhakikisha kwamba:-

- (i) Ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi unaongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 90 mwaka 2020 na asilimia ya wanafunzi wanaoendelea na Kidato cha Kwanza kuongezeka kutoka asilimia 55.5 hadi asilimia 100;
- (ii) Ufaulu wa mtihani wa Kidato cha Nne unaongezeka kutoka wastani wa asilimia 69.8 mwaka 2015 hadi asilimia 90.0 mwaka 2020 na ufaulu wa daraja la I – III unaongezeka kutoka wastani wa asilimia 30.8 hadi asilimia 50.0; na
- (iii) Idadi ya wataalamu wenye ujuzi wa juu wanaongezeka kutoka asilimia 3 hadi asimilia 10 mwaka 2020, ujuzi wa kati kutoka asilimia 13 hadi 30 na ujuzi wa chini kupungua kutoka asilimia 84 hadi 60.

(e) Kuimarisha ithibati na udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo ili kuhakikisha kwamba:-

- (i) Asilimia 60 ya wanafunzi wanahitimu shahada kwenye sekta ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa uchumi;
- (ii) Programu tatu (3) au zaidi za mafunzo zinaanzishwa zenye kukidhi mahitaji na kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa;
- (iii) Asilimia 70 ya wahitimu katika ngazi zote wawe katika mrengo wa sayansi, ufundi, hisabati na teknolojia;

(f) Kuandaa na kutumia utaratibu wa upatikanaji na usambazaji wa vitabu vya kiada na ziada kwa ngazi zote za elimu na mafunzo ili kuhakikisha kwamba:-

   (i) Uwiano wa kitabu cha kiada kwa mwanafunzi katika Elimumsingi unaongezeka kutoka 1:3 mwaka 2015 hadi 1:1 mwaka 2020;
   (ii) Asilimia 50 ya fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule zinatumika kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada; na
   (iii) Uwiano wa vitabu vya ziada kwa kila somo kwa mwanafunzi katika Elimumsingi kuwa 1:10.

(g) Kuandaa utaratibu, kuimarisha mfumo wa udahili na kutumia fursa za elimu na mafunzo ndani na nje ya nchi kwa makundi yote ya jamii kwa usawa katika ngazi zote hususan katika ufundi, hisabati, sayansi na teknolojia ili kuhakikisha kwamba:-

   (i) Asilimia 100 ya wahitaji wa mikopo kwa ajili ya kusomea fani ya udaktari wanapata mikopo;
   (ii) Ufadhili wa nafasi 500 za masomo ya fani ya udaktari zinapatikana kila mwaka ili kupunguza pengo la uhaba wa madaktari nchini;
   (iii) Asilimia 100 ya wale wenye mahitaji maalumu, vipaji na vipawa wataotambulika watapata fursa za kuendelea na masomo katika ngazi mbalimbali; na
   (iv) Shule moja maalumu ya Ufundi (Specialized Technical Schools) au zaidi inaanzishwa kila mkoa ambayo itadahili wanafunzi wenye vipaji mbalimbali na kuwaendeleza kwenye fani mbalimbali zenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

(h) Kuandaa mpango wa kuwawezesha walimu na wanafunzi kutumia TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia ili kuhakikisha kwamba:-

   (i) Asilimia 80 ya walimu wanaandaliwa na kutumia TEHAMA kufundishia katika ngazi zote; na

(ii) Asilimia 70 ya taasisi zote zinazotoa elimu na mafunzo zinaunganishwa katika Mkongo wa Taifa.

(i) Kuhuisha miongozo ya Elimu na Mafunzo ili kuondoa vikwazo vinavyosababisha mwanafunzi kushindwa kukamilisha mzunguko wa elimu au mafunzo ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Mdondoko katika Elimumsingi unapungua kutoka wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2015 hadi asilimia 2 mwaka 2020;

(ii) Wasichana wote wa Elimumsingi wanaoacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito wataendelea na masomo; na

(iii) Wanafunzi wanaomaliza mzunguko wa elimu katika ngazi ya Elimumsingi wanaongezeka kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 95 mwaka 2020.

(j) Kuandaa walimu, wakufunzi na wahadhiri mahiri hususan katika masomo ya hisabati, lugha, sayansi, teknolojia na ufundi ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Uondokaji wa walimu, wakufunzi na wahadhiri unapungua kutoka wastani wa asilimia 0.8 mwaka 2015 hadi asilimia 0.2 mwaka 2020;

(ii) Tatizo la uhaba wa walimu wapato 24,000 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za Sekondari linapungua kwa kutoa mafunzo kwa walimu 5,000 wa masomo hayo kila mwaka; na

(iii) Idadi ya wahadhiri wanaongezeka kutoka wahadhiri 6,880 mwaka 2015 hadi wahadhiri 10,000 mwaka 2020.

(k) Kuandaa mpango kabambe wa kuongeza udahili katika taasisi za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya rasilimali watu na ujuzi kwa maendeleo ya Taifa na soko la ajira hususan ujuzi unaohitajika au kuhusiana na sekta zinazokua haraka na zinazojitokeza mfano mafuta, gesi na madini ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Sayansi Shirikishi cha Mwalimu J.K. Nyerere (Butiama) unakamilika na

kuanzisha na kukamilisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi za Madini Shinyanga;

(ii) Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha Mkoa wa Kagera utafanyika;

(iii) Udahili katika vyuo vya Ufundi Stadi unaongezeka kutoka wastani wa wanafunzi 150,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 700,000 mwaka 2020;

(iv) Udahili katika vyuo vya Ufundi vya Kati unaongezeka kutoka wastani wa wanafunzi 30,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 285,600 mwaka 2020; na

(v) Udahili katika ngazi ya shahada unaongezeka katika vyuo vya elimu ya Juu kutoka wastani wa wanafunzi 60,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 117,000 mwaka 2020.

(l) Kushirikiana na wadau katika kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wa elimu ya mafunzo ikiwemo mikopo na ruzuku ili uwe endelelevu na wenye vyanzo anuai;

(m) Kuweka utaratibu wa ada na michango mbalimbali katika shule na vyuo binafsi ili kusimamia kwa ufanisi masuala ya ada na michango;

(n) Kuandaa utaratibu wa ushirikiano baina ya Sekta ya Umma, Binafsi na Jamii katika ugharamiaji wa maendeleo ya elimu na mafunzo katika ngazi zote ili kuhakikisha kwamba:-

(i) Mchango wa Sekta Binafsi katika kudahili wanafunzi katika vyuo vya Ufundi ngazi ya kati unaongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 2015 hadi asilimia 25 mwaka 2020; na

(ii) Mchango wa Sekta Binafsi kudahili wanafunzi katika ngazi ya shahada unaongezeka kutoka asilimia 35 mwaka 2015 hadi asilimia 40 mwaka 2020.

(iii) Bajeti ya Sekta ya Elimu na Mafunzo inaongezeka kutoka asilimia 17.6 mwaka 2015 hadi asilimia 25 ya bajeti ya Serikali mwaka 2020;

(iv) Bajeti ya Elimumsingi inaongezeka kutoka asilimia 71 mwaka 2015 hadi asilima 75 ya Bajeti ya Sekta ya Elimu na Mafunzo mwaka 2020;

(v) Bajeti ya Elimu ya Ufundi na Elimu ya Juu inaongezeka hadi kufikia asilimia 25 ya Bajeti ya Sekta ya Elimu na Mafunzo ifikapo mwaka 2020; na

(vi) Kuendelea kusimamia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2015 ambayo inaifanya elimu ya Msingi hadi Sekondari kuwa ya lazima na bila ya malipo.

(o) Kuanzisha Tume ya Walimu itakayosimamia Maendeleo na Maslahi ya Walimu wote Nchini.

**Maji**

53. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote hususan wale ambao wanaishi maeneo ya vijijini. Katika kipindi hicho yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana:-

(a) Serikali imeendelea kuimarisha huduma za maji Vijijini kwa kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu ya maji, hali iliyochangia upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Vijijini kuongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 67.7 mwaka 2015;

(b) Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma ya maji safi na salama Mijini. Kutokana na jitihada hizo, kiwango cha upatikanaji maji kwa wakazi wa Miji Mikuu ya Mikoa kimeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2005 hadi asilimia 86 mwaka 2014. Aidha, katika jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji ya Bagamoyo na Kibaha, kiwango cha upatikanaji maji kimeongezeka kutoka asilimia 55 hadi asilimia 68 katika kipindi hicho.

(c) Maabara za maji 16 na Kituo cha Utafiti cha kuondoa madini ya *fluoride* cha Ngurdoto kilichoko Arusha zimejengewa uwezo kwa kuzipatia dawa za kufanyia uchunguzi, mashine pamoja na

usafiri. Aidha, maabara za maji katika mikoa ya Kigoma, Singida, Shinyanga na Bukoba zimekarabatiwa;

(d) Wananchi wameendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini ambapo vyombo vya watumiaji maji (COWSOs) 520 vimeundwa katika Halmashauri mbalimbali nchini; na

(e) Usimamizi wa rasilimali za maji umeendelea kuimarishwa na yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

  (i) Jumuiya 91 za Watumiaji Maji zimeundwa; na

  (ii) Maeneo 26 ya vyanzo vya maji yametathminiwa na kuzungushiwa uzio pamoja na maeneo ya maji chini ya ardhi ya Maisaka na Makutupora.

(f) Ujenzi wa mabwawa manne ya Nyambele (Bunda), Kinyambwiga (Bunda) Nyashitanda (Misungwi) na New Sola (Maswa) umekamilika na yamekabidhiwa kwa wananchi;

(g) Mradi wa maji wa Kahama/Shinyanga umekamilika ambapo upanuzi wa mradi unaendelea katika maeneo ya Vijiji vilivyoainishwa pamoja na Miji iliyopo katika Wilaya hiyo. Aidha, Mji wa Ngudu, wilayani Kwimba tayari umeunganishwa kwenye mradi huo na wananchi wanapata maji; na

(h) Upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka umefanyika katika Miji ya Moshi, Tanga, Arusha, Mbeya, Iringa, Songea, Tabora, Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma.



*Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa Nachingwea mara baada ya kuzindua mradi wa maji wenye thamani ya Shilingi Bilioni 34.6 unaojumuisha Wilaya za Nachingwea na Masasi Mkoani Mtwara.*

54. **Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi kilichopita, bado zipo changamoto mbalimbali katika kutekeleza miradi ya maji nchini. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kukabiliana na changamoto hizo kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuboresha huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 67.7 mwaka 2015 hadi asilimia 85 mwaka 2020 kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutekeleza lengo la kuwapatia wananchi waishio vijijini huduma ya maji safi, salama na ya kutosha kama yalivyo Malengo ya Milenia;

(ii) Kujenga vituo vya kuchotea maji 93,051 vitakavyohudumia watu 23,262,876 ambavyo vitaongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka 20,022,283 mwaka 2015 hadi kufikia 43,285,159 mwaka 2020 sawa na asilimia 53.7; na

(iii) Kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika majengo ya Serikali, asasi za umma na binafsi na nyumba za watu binafsi.

(b) Kuboresha huduma ya Maji Mijini kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 95 mwaka 2020;

(ii) Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika miji mikuu ya mikoa kutoka asilimia 86 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 95 mwaka 2020;

(iii) Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo ya miradi ya Kitaifa kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 90 mwaka 2020; na

(iv) Kujenga Bwawa la Kidunda ili kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam.

(c) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji na kuhakikisha vijiji vyote vilivyopo kando kando ya miradi hiyo mikubwa vinanufaika. Miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Nzega, Tabora na Igunga;

(ii) Mradi wa Maji wa Chalinze awamu ya tatu;

(iii) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe; na

(iv) Miradi ya Maji katika miji mikuu ya mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe na Katavi.

(d) Kupanua na kuboresha miradi ya maji ya kitaifa ifuatayo:-

(i) Mradi wa Wanging'ombe, Maswa, Mugango-Kiabakari, Handeni Trunk Main (HTM), Chalinze, Makonde na Kahama-Shinyanga; na

(ii) Mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kwenda Mji wa Mtwara ili kukidhi mahitaji ya maji katika ukanda huo kutokana na ongezeko la watu na shughuli za uwekezaji baada ya kugundulika kwa gesi asilia.

(e) Kuanzisha miradi ya ujenzi wa mabwawa katika mikoa yenye ukame kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na kilimo katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara, Simiyu, Arusha, Shinyanga, Manyara na maeneo mengine yenye ukame;

(ii) Ujenzi wa mabwawa manane ya kimkakati kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, kuzuia mafuriko na matumizi mengine; na

(iii) Kukamilisha ukarabati wa mabwawa ambayo tayari yamekwisha jengwa.

55. **Shughuli nyingine zitakazofanyika ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini ni kama ifuatavyo:-**

(a) Kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwenye vijiji vinavyozunguka maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria;

(b) Kuendelea na uchimbaji wa visima vya maji na kutumia pampu za maji zinazotumia nishati ya jua;

(c) Kuiwezesha Sekta Binafsi kutoa huduma ya maji safi kwa mfumo wa ubia na Sekta ya Umma;

(d) Kuendelea kuhamasisha wananchi kuunda Jumuiya za Watumia Maji Vijijini katika Mabonde yote ya maji nchini

ifikapo mwaka 2020 ili kuwashirikisha wananchi kikamilifu katika kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji;

(e) Kujenga na kukarabati Maabara za Maji kwa ajili ya kusimamia ubora wa maji nchini na kutoa taarifa za hali ya ubora wa maji kila mwaka;

(f) Kuziongezea uwezo wa kiutendaji taasisi zinazoshughulika na Sekta ya Maji ambazo ni Chuo cha Maji, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na Bohari Kuu ya Maji ili kuongeza ufanisi wa taasisi hizo;

(g) Kuendelea kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika matumizi endelevu na usimamizi bora wa rasilimali za maji shirikishi;

(h) Kuweka mfumo madhubuti na endelevu wa utunzaji wa vyanzo vya maji na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo hivyo;

(i) Kufanya tafiti za upatikanaji maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuendeleza rasilimali hiyo kwa matumizi mbalimbali;

(j) Kuimarisha mtandao wa ukusanyaji takwimu za rasilimali za maji kwa ajili ya kupata taarifa sahihi za hali ya rasilimali za maji nchini ili kuwezesha mgawanyo mzuri wa maji na kupunguza migogoro baina ya watumia maji; na

(k) Kuanzisha Mfuko wa Maji wa Taifa (National Water Investment Fund) kwa ajili ya kuharakisha ujenzi wa miradi nchini.

**Majitaka**

(a) Kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji majitaka nchini.

(b) Kuiwezesha Sekta Binafsi kutoa huduma ya majitaka kwa mfumo wa ubia na Sekta ya Umma.

## SURA YA TANO
## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

56. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuanzisha na kuendesha programu za kukabiliana na changamoto za umasikini kwa wananchi na ukosefu wa ajira hususan kwa vijana ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Dhamana ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 10.5 imetolewa na kuwanufaisha wananchi 10,646 katika vikundi 300 kutoka mikoa mbalimbali ikiwemo Mwanza, Mtwara, Mbeya, Rukwa, Singida, Dodoma, Manyara, Ruvuma, Tanga, Kagera na Lindi;

(b) Kuanzishwa kwa mafunzo ya ujasirimali kwa vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu yenye lengo la kuwawezesha kujiajiri kwa kutumia fursa zilizopo badala ya kutegemea ajira za sekta rasmi;

(c) Kampuni 1,728 zimesajiliwa kwa ushirikiano na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ambapo Kampuni 786 zilipata kiasi cha shilingi bilioni 7.8 kama mitaji kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya kiuchumi;

(d) Mfuko wa Ufundi na Utafiti umeanzishwa kwa ushirikiano na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 16.5 zilitolewa kwa vyuo tisa vya Elimu ya Juu kati ya vyuo 49 vilivyotuma maombi kwa ajili ya vifaa vya kufundishia;

(e) Uhamasishaji wa kuanzisha Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS na VICOBA) umewezesha SACCOS kuongezeka kutoka 1,875 mwaka 2005 hadi 9,468 mwaka 2013. Idadi ya VICOBA imeongezeka hadi kufikia 23,000 mwaka 2015 vyenye wanachama 700,000 na mtaji wa Shilingi bilioni 86. Aidha, wanachama wa SACCOS na vikundi vingine vya kijamii milioni 1.6 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali. Kati ya hao, wanawake ni asilimia 53 na wanaume ni asilimia 47.

(f) Shirikisho la Mafundi Seremala limeanzishwa kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa samani ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje;

(g) Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo umeboreshwa na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

   (i) Mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 25.1 mwaka 2010 hadi kufikia bilioni 57.7 mwaka 2014 na kunufaisha wajasiriamali 95,336. Aidha, urejeshaji wa mikopo umefikia asilimia 93.8; na

   (ii) Mfuko umeongeza ajira 650,000 na kuzijengea uwezo asasi ndogo ndogo za kifedha 590. Aidha, wajasiriamali 8,665 wamepatiwa ujuzi wa kuendesha biashara zao.

(h) Mfuko wa Udhamini wa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati kupitia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Bidhaa Nje, umeongezewa mtaji kutoka Shilingi bilioni 6 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 30.81 mwaka 2014. Aidha, mfuko umetoa dhamana ya Shilingi milioni 448.59 ambapo asilimia 80 ya dhamana imetumika kuwezesha shughuli za kilimo, kuhamasisha uundaji wa mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na kuchochea watu wengi kufanya biashara ya mauzo ya nje; na

(i) Mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 50.03 imetolewa kwa wajasiriliamali chini ya mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira. Mikopo hiyo imetolewa kupitia Benki za CRDB na NMB na kuwanufaisha wajasiriamali 74,701.

57. **Kwa kutambua kwamba kuwawezesha wananchi kiuchumi ni hatua ya msingi katika kujenga Taifa lililoimarika kiuchumi na lenye lengo la kujitegemea, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuhakikisha kuwa shughuli zote zenye mwelekeo wa ushirika zinapewa msukumo stahiki kwa kuhamasisha na kusimamia kwa nguvu uanzishaji wa vikundi vya ushirika kama vile SACCOS na VICOBA; Vyama vya Mazao, Ufugaji na Uvuvi

hasa ikizingatiwa kuwa ushirika ndiyo silaha kuu ya wanyonge na nguzo kuu ya ujenzi wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea;

(b) Kuweka mfumo wa kuvitambua, kuvisajili na kuviwezesha vikundi vyote vyenye mwelekeo wa ushirika na ujasiriamali;

(c) Kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuhakikisha kwamba fursa ya mikopo kwa ajili ya mitaji inapatikana bila ya urasimu na kwa masharti nafuu na kuwafikia wananchi wengi mijini na vijijini;

(d) Kutenga kiasi cha shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji kama Mfuko wa Mzunguko (Revolving Fund) kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika;

(e) Kusaidia wafanyabiashara wadogo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutenga maeneo mahsusi katika kila Halmashauri kwa ajili ya biashara ndogo ndogo;

(ii) Kuondoa kero na malalamiko kuhusu ushuru na kodi zinazotozwa na Halmashauri ambazo zinakwamisha jitihada za wafanyabiashara wadogo kujikwamua kimaisha;

(iii) Kuwarasimisha wafanyabiashara wadogo ili biashara zao zitambuliwe kisheria kwa kuwapatia leseni, mafunzo ya ujasiriamali na kuwaunganisha na asasi za fedha ili wapate mikopo yenye masharti nafuu;

(iv) Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Biashara Ndogo na za Kati;

(v) Kuanzisha mfuko mkubwa wa kitaifa wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na asasi nyingine za fedha;

(vi) Kuweka utaratibu utakaozitaka Halmashauri kutenga asilimia 30 ya thamani ya manunuzi yake kwa ajili ya biashara, kampuni au vikundi vinavyomilikiwa na vijana/wanawake; na

(vii) Kuhakikisha kazi za ujenzi unaogharamiwa na Serikali katika maeneo ya vijijini kwa mfano ujenzi wa barabara, shule na zahanati zinatolewa kwa vikundi vya vijana na wanawake katika maeneo husika.

(f) Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kukamilisha marekebisho ya Sera na Sheria ya Uwekezaji na pia kuandaa Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi;

(ii) Kuondoa vikwazo vya kuanzisha na kuendesha biashara kwa kupitia upya Sheria, Kanuni na Taratibu za biashara ili kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi; na

(iii) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika miradi ya ubia na sekta ya umma pamoja na kuandaa mazingira rafiki ya biashara kwa lengo la kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

**Urasimishaji Mali za Wanyonge:**

58. **Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi na kuwapa nguvu ya kiuchumi hasa wanyonge mijini na vijijini kwa kuwawezesha kumiliki ardhi na kufanya biashara katika mfumo rasmi wa kisasa unaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, kupitia urasimishaji rasilimali na biashara, MKURABITA ni nyenzo muhimu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kupunguza umasikini na kuongeza ajira nchini. Katika kipindi cha miaka mitano ya Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuongeza kasi ya utambuzi, usajili na umiliki wa ardhi pamoja na kuendeleza urasimishaji wa rasilimali za wananchi,

kuwashirikisha na kuwawezesha kutumia rasilimali zao kama dhamana ya kupata mitaji;

(b) Kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ardhi wakiwemo Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Halmashauri za Miji, Majiji na Wilaya ili kukamilisha kazi ya upimaji wa mipaka ya vijiji vyote na kuwahamasisha wananchi kuchangia upimaji wa mashamba yao na kuwapatia hati miliki za kimila;

(c) Kuanzisha chombo cheye nguvu ya kisheria kitakachoratibu shughuli za urasimishaji rasilimali za wananchi; na

(d) Kuanzisha Mfuko Maalumu wa kugharamia shughuli za urasimishaji ambao utaziwezesha Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji kukopeshwa kwa masharti nafuu. Mfuko huu utaendeshwa kwa utaratibu wa Dhamana ya Benki (Bank Guarantee Scheme).

**Kuwawezesha Vijana Kujiajiri**

59. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuongeza ajira kwa vijana kwa kuanzisha na kuendesha programu za kukabiliana na ongezeko kubwa la vijana wanaofuzu Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu kila mwaka wanaohitaji ajira ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Takriban vijana milioni 16 wameajiriwa katika sekta mbalimbali nchini katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2015;

(ii) Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.8 imetolewa kwa SACCOS 244 na vikundi vya vijana 667 katika kipindi cha 2014/15;

(iii) Jumla ya vijana 35,000 wamepewa mafunzo ya ujasiriamali ambapo kati yao, vijana 11,500 walikuwa wahitimu wa elimu ya juu; na

(iv) Wahitimu 325 wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali pamoja na kuwezeshwa

kupata mitaji kupitia ushirikiano wa Serikali na Umoja wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUGECO).

60. **Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa vijana ambao ni kundi kubwa la nguvukazi. Changamoto zinazowakabili ni pamoja na ukosefu wa ajira, elimu na maarifa ya kisasa katika uzalishaji mali, mitaji, biashara na ujasiriamali. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga, kurasimisha, kupima na kuyawekea miundombinu maeneo maalumu ya vijana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo, ufugaji, madini, viwanda vidogo, uvuvi, mawasiliano na biashara;

(b) Kuziwezesha SACCOS za vijana katika Halmashauri zote nchini kupata mikopo kutoka kwenye benki na taasisi nyingine za fedha;

(c) Kuwajengea uwezo vijana kutumia TEHAMA katika kuboresha uzalishaji mali, ufanisi, viwango na kutafuta masoko katika shughuli zao za uchumi;

(d) Kuwawezesha vijana wanaohitimu Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi kuunda makampuni kulingana na fani zao kwa lengo la kuwapatia mitaji na nyenzo kupitia taasisi za fedha na mifuko mingine ya uwezeshaji;

(e) Kuhamasisha na kuweka mazingira yatakayowezesha vijana wajasiriamali wadogo kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuweza kupata mikopo na kunufaika na mafao mengineyo yatolewayo na mifuko hiyo;

(f) Kuviwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) ili viweze kutoa mafunzo ya ujasiriamali, stadi za maisha, ujasiri, uongozi na TEHAMA kwa vijana;

(g) Kuhakikisha Halmashauri zote nchini zinaanzisha vituo maalumu ili kuwawezesha vijana kupata sehemu ya kujifunza

kwa vitendo shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kupata taarifa mbalimbali za maendeleo;

(h) Kuwawezesha vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati kufanya kazi kwa kujitolea katika asasi mbalimbali kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ya kazi ili waweze kuajirika au kujiajiri wenyewe; na

(i) Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu.

**Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi**

61. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, jitihada za kuwaendeleza wanawake zimeendelea kuchukuliwa kwa kutunga Sera, Sheria na Programu mbalimbali zenye lengo la kuongeza fursa za kiuchumi na kuwajengea uwezo wa kitaaluma, kibiashara, mbinu za kupata mitaji, masoko pamoja na mikopo.

62. Fursa hizo zimewawezesha wanawake kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na hivyo kuinua vipato vyao na vya familia.

63. **Kwa kutambua kuwa uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi umeleta maendeleo na mabadiliko makubwa kwa wanawake, familia na Taifa kwa ujumla na kwa kutambua kuwa wanawake ndio wazalishaji wakuu wa chakula na walezi wa familia, Chama Cha Mapinduzi, katika miaka mitano ijayo, kitaielekeza Serikali kuendelea kuwaendeleza wanawake kiuchumi kwa kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, elimu ya ujasiriamali na biashara ili kuwawezesha kuongeza ajira, ujuzi wa kujiajiri, fursa za kipato na kujikimu;

(b) Kuwahamasisha kuanzisha na kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali, vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS na

VICOBA) na kuwawezesha kimtaji ili kupanua shughuli zao za uzalishaji mali;

(c) Kuwahamasisha kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuweza kupata mikopo na kunufaika na mafao mengineyo yatolewayo na mifuko hiyo hasa mafao ya uzazi na elimu;

(d) Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mujibu wa Sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu; na

(e) Kuondoa kero na malalamiko ya wanawake wajasiriamali hasa mama lishe, wauza mbogamboga, wauza maandazi/vitumbua kuhusu maeneo ya kufanyia biashara, ushuru na kodi zinazotozwa na Halmashauri ambazo zinakwamisha jitihada zao za kujikwamua kimaisha.

# SURA YA SITA

## MAZINGATIO MAALUMU YA ILANI KUHUSU ZANZIBAR




*Mwenyekiti wa CCM Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete (katikati) akiwatambulisha Mgombea wa CCM wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu John Pombe Magufuli (kulia) na Mgombea wa CCM wa Urais wa Zanzibar Ndugu Mohamed Shein*

**Utangulizi**

64. Katika Sura hii, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 - 2020, inaelezea na kuainisha maeneo muhimu ya Sera za CCM, kwa kuzingatia mazingira maalumu ya Zanzibar (SMZ). Kwa kutambua na kuridhika na Sera hizo ambazo zinazingatia maslahi mapana ya Taifa letu yaani haki, umoja, mshikamano, uwazi na uwajibikaji, Wazanzibari wameendelea kuiunga mkono CCM na kuipa ridhaa ya kuongoza Serikali ya Mapinduzi kwa kuichagua katika chaguzi zote zilizopita.

65. Katika kipindi cha mwaka 2010 - 2015 cha Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Zanzibar imeendelea kupiga hatua kubwa ya maendeleo kisiasa, kiuchumi na kijamii.

**MAFANIKIO NA MALENGO YA KIUCHUMI**

66. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein imeweza kutekeleza kwa mafanikio makubwa, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 - 2015 na kuendelea kuimarisha umoja wa kitaifa na utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya mafanikio hayo ya kujivunia ni kama yafuatayo:-

**Hali ya Uchumi**

67. Katika miaka mitano iliyopita Sekta ya Uchumi imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) **Kukuza Uchumi:**

(i) Pato la Taifa limeongezeka kutoka thamani ya Shilingi bilioni 1,050.8 mwaka 2010 hadi kufikia thamani ya Shilingi bilioni 2,138.5 mwaka 2014. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kiliongezeka kutoka asilimia 4.3 mwaka 2010 hadi asilimia 7.0 mwaka 2014;

(ii) Mfumuko wa bei umeshuka kutoka asilimia 6.1 mwaka 2010 hadi asilimia 5.6 mwaka 2014;

(iii) Pato la kila mwananchi limeongezeka kutoka shilingi 856,000 sawa na dola za Kimarekani 613 mwaka 2010 na kufikia shilingi milioni 1.56 sawa na Dola 939 mwaka 2014;

(iv) Kiwango cha thamani ya bidhaa zilizosafirishwa nje, kiliongezeka kutoka shilingi bilioni 18 mwaka 2010 hadi kufikia shilingi bilioni 133.6 mwaka 2014; na

(v) Kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani kimeongezeka kutoka shilingi bilioni 181.379 mwaka 2010/2011 hadi shilingi bilioni 330.7 mwaka 2013/2014.

(b) **Maeneo Huru ya Kiuchumi**

(i) Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi (Land Use Plan) wa eneo Huru la Kiuchumi la Fumba, umekamilika. Jumla ya hekta 3,000 zimewekewa mipaka na kugawanywa katika eneo la vijiji vya asili (hekta 1,310), eneo la uwekezaji (hekta 743) na eneo la akiba (hekta 947). Aidha, maandalizi ya kulifungua kiuchumi Eneo Huru la Kiuchumi la Micheweni, yanaendelea.

(ii) Hadi kufikia mwaka 2014, jumla ya miradi 165, yenye mtaji wa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 526.7 imeidhinishwa kuwekezwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) ikilinganishwa na miradi 33 mwaka 2010 yenye mtaji wa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 115.2. Miradi 63 kati ya hiyo, ni ya wawekezaji Wazalendo, na 90 ni ya wageni. Miradi hiyo yote inazalisha ajira zipatazo 6,658 kwa wananchi.

(c) **Uwakilishi wa Sekta Binafsi:**

Baraza la Biashara la Zanzibar limeanzishwa na kushiriki katika majadiliano ya ubia wa uwekezaji kwa maendeleo ya viwanda na mashirikiano kwa ajili ya wote(*Smart Partneship Dialogue*). Miongoni mwa yaliyojadiliwa katika vikao hivyo ni

pamoja na kuimarisha mapato, kukuza Pato la Taifa na Faharisi ya Bei ya mtumiaji.

(d) **Mazingira Bora ya Kiuchumi:**

Sheria ya Fedha na Uwekezaji imefanyiwa mapitio ili iendane na mazingira halisi ya kiuchumi na kutoa nafasi zaidi ya kuzitangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Kutokana na hatua hizo, wawekezaji kutoka nje wameweza kujitokeza na kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

(e) **Kupambana na Umasikini:**

(i) Mifuko ya mikopo kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo wadogo, yaani Mfuko wa Kujitegemea na Mfuko wa JK & AK imeunganishwa pamoja na kuanzishwa mfuko mmoja tu (Mfuko wa Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi). Mfuko huo umezinduliwa ukiwa na mtaji wa shilingi bilioni 2.31. Aidha, mikopo 1,603 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.45, imetolewa katika shehia 305 Unguja na Pemba na kutoa ajira za moja kwa moja 20,614, zilizowahusisha wanawake 11,873 na wanaume 8,741;

(ii) Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF II) umekamilika ambapo miradi 656 yenye thamani ya Shilingi bilioni 9.4 imetekelezwa. Kati yake miradi 324 ni ya Unguja na 332 ni ya Pemba. Miradi hiyo inahusu shughuli za kijamii, uvuvi (ununuzi wa boti na zana za kuvulia) pamoja na mapambano dhidi ya UKIMWI.

(iii) Utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) umeanza katika Shehia 40 za Unguja na Pemba (Unguja 20 na Pemba 20) ambapo miradi 103 (Unguja 68 na Pemba 35) yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.1 imeanzishwa. Miradi hiyo inahusu ujenzi wa skuli za maandalizi, ujenzi wa matuta ya kuzuia maji ya bahari, hifadhi ya

mazingira na ukarabati wa njia za ndani. Jumla ya kaya masikini 6,598 zimenufaika na miradi hiyo.

(iv) Vikundi vya kiuchumi 250 na wajasiriamali 6,000 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, wakiwemo wahitimu wa vyuo vikuu 250, ili kubadili mitazamo yao na kuwajengea uwezo wa kujiajiri wao wenyewe; na

(v) Kituo cha kulelea wajasiriamali kimeanzishwa. Kituo hicho ni cha kwanza na cha aina yake katika ukanda wa Afrika Mashariki, na kinatoa mafunzo katika fani za Uchumi, TEHAMA, Utalii na Usindikaji wa Mazao ya Biashara.

**Kukuza Uchumi**

68. **Katika kipindi kilichopita (2010 -2015), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi na kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaendeleza mafanikio hayo na kuandaa Mipango ya kipaumbele ili kufanikisha huduma za kilimo, utalii endelevu pamoja na kujenga mazingira bora ya biashara na kuimarisha huduma za jamii kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kufanya mapitio ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA) na kuandaa mkakati mpya wa utekelezaji wa Mpango huo (MKUZA III) na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Vision 2020);

(b) Kujenga mazingira yatakayowezesha uchumi wa Zanzibar kufikia kiwango cha uchumi wa nchi zenye kipato cha kati, kiwango cha ukuaji wa uchumi kufikia wastani wa asilimia 10, mfumuko wa bei kubaki katika tarakimu moja na wastani wa pato la kila mwananchi kuongezeka kutoka kiwango cha sasa cha wastani wa dola za Kimarekani 939 (shilingi 1,340,000) hadi dola 1950 (shilingi 3,500,000) ifikapo mwaka 2020;

(c) Kuendeleza udhibiti wa mapato na nidhamu katika matumizi ya Serikali, kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali na kuanzisha Msimamizi wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu; na

(d) Kupunguza utegemezi kwa Wahisani wa Maendeleo, misamaha ya kodi isiyo na tija kwa Taifa na kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka Shilingi bilioni 330.7 mwaka 2013/2014 hadi kufikia Shilingi bilioni 800 ifikapo mwaka 2020/21 na kushusha kiwango cha nakisi ya Bajeti ya Serikali kutoka uwiano wa asilimia 8 ya Pato la Taifa mwaka 2014/2015 hadi kufikia asilimia 7 ifikapo mwaka 2019/2020.

**Mchango wa Sekta Binafsi**

69. Sekta Binafsi hutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), iliidhinisha jumla ya miradi 35 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 1.06 na kutengeneza ajira 1,365. Ili kuongeza mchango wa Sekta Binafsi katika kukuza Uchumi wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Mwongozo na Sheria ya Ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kuharakisha utekelezaji wa miradi yenye tija inayopendekezwa kufanyika;

(b) Kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa uendelezaji wa mji mpya wa kisasa katika Maeneo Huru ya Uchumi ya Fumba na Micheweni, na kuweka vivutio kwa wawekezaji wa Sekta ya Viwanda; na

(c) Kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha kimtaji wawekezaji wa ndani na kuwaunganisha na wawekezaji wa nje pamoja na kuvishawishi Vyombo na Taasisi za Fedha nchini, kuwapatia mikopo yenye riba na masharti nafuu na kupunguza

urasimu na vikwazo katika biashara, ukiwemo mlolongo wa leseni na kodi.

**Kupambana na Umasikini**

70. Ili kuongeza nguvu na kasi ya kupambana na umasikini katika kipindi kilichopita (2010-2015), Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umeanzishwa. Kwa kupitia mfuko huo wananchi wengi hususan vijana, wanawake na wafanyabishara wadogo wadogo wameweza kupatiwa mitaji (mikopo) na kujikwamua kiuchumi. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaendeleza jitihada hizo na kuielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ili kuongeza uwezo wake wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo, kuimarisha Kituo cha Kulelea Wajasiriamali na kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuondokana na umasikini;

(b) Kuendelea kuwahamasisha wananchi kuunda vikundi vya ushirika na hasa ushirika wa uzalishaji mali, vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS), VICOBA pamoja na BENKI NDOGO vyenye wanachama wengi na kuleta tija kwa jamii;

(c) Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kukamilisha Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) na kubuni programu nyingine za kusaidia jamii kupambana na umasikini; na

(d) Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na kuhakikisha kwamba, fedha za mfuko huo zinatumika kwa lengo lililokusudiwa na hususan kuimarisha huduma za jamii.

(e) Kuzihamasisha asasi za kifedha nchini kuanzisha dirisha maalumu kwa ajili ya kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu wanawake na vijana. Aidha, idara maalumu ya mikopo itaanzishwa ili kusimamia majukumu yafuatayo:-

    (i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Asasi za Mikopo Nafuu (Micro-Finance Policy) ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kunufaika na huduma za kifedha kwa masharti nafuu;

(ii) Kutoa mikopo 5,000 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 itakayowanufaisha jumla ya wananchi 50,000 kutoka makundi mbalimbali ya jamii hususan wanawake, vijana na walemavu Unguja na Pemba;

(iii) Kuimarisha huduma za mikopo kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo teknolojia ya mitandao ya simu ili kupunguza gharama na muda wa upatikanaji na urejeshaji wa fedha za mikopo; na

(iv) Kuongeza kiwango cha dhamana ya Serikali katika benki kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 500 ili ziweze kuwahudumia wajasiriamali 50,000.

(f) Kuanzisha jumla ya vituo kumi vya huduma za biashara, kimoja kwa kila Wilaya ili kuongeza tija katika shughuli za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo.

**Sekta za Uzalishaji Mali**

**Kilimo**

71. Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 31 katika Pato la Taifa (GDP) na kuwawezesha wananchi walio wengi kujikimu kimaisha na kuwapatia uhakika wa chakula na lishe bora. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Sekta ya Kilimo imepata mafaniko yafuatayo:-

(a) Sera ya Masoko na Bidhaa za Kilimo imepitishwa na kuanza kutumika. Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea, Sheria ya Uhifadhi na Utibabu wa Mimea na Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe zimepitishwa;

(b) Mashamba darasa 1,200 ya wakulima yameanzishwa. Wakulima 2,800 wa zao la mpunga na 1,500 wa zao la muhogo na mboga mboga wamepatiwa mafunzo. Jumla ya tani 674,334 za mazao ya chakula zimezalishwa mwaka 2014 ikilinganishwa na tani 346,535 zilizovunwa mwaka 2013. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 95;

(c) Jumla ya matrekta mapya 45 yamenunuliwa, matrekta makongwe 37 yamefanyiwa matengenezo na mashine za kuvunia mpunga 14 zimenunuliwa. Eneo la uzalishaji wa zao la

mpunga limeongezeka kutoka hekta 10,000 mwaka 2010 hadi hekta 34,000 mwaka 2015. Kiwango cha uzalishaji wa zao hilo kimeongezeka kutoka tani 20,000 hadi tani 33,655. Idadi ya kaya zinazojishughulisha na kilimo imeongezeka kutoka 10,000 mwaka 2010 hadi 70,000 mwaka 2014;

(d) Mafunzo ya nadharia na vitendo yametolewa kwa wakulima 400 juu ya mbinu za kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji. Wakulima 2,000 (700 Pemba na 1,300 Unguja) walipatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za uzalishaji mpunga;

(e) Eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 600 mwaka 2010, hadi hekta 800 mwaka 2014. Jumla ya hekta 200 za miundombinu ya umwagiliaji maji zimeimarishwa. Kiwango cha uzalishaji wa mpunga wa kumwagilia maji kimeongezeka kutoka tani 2 mwaka 2010 hadi tani 4 kwa hekta mwaka 2014;

(f) Matumizi ya pembejeo kati ya mwaka 2010 hadi 2015 yameongezeka kutoka tani 13 hadi 750 za mbegu tani 203 hadi 1,500 za mbolea na lita 10,000 hadi 30,000 za dawa ya kuulia magugu. Wakulima 61,500 wa mpunga wa kumwagilia maji na wa kutegemea mvua wamepatiwa ruzuku ya bei za pembejeo (asilimia 75);

(g) Vikundi 33 vya wakulima 652 (wanawake 345 na wanaume 307) vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo ya kilimo cha mbogamboga na matunda;

(h) Chuo cha Kilimo cha Kizimbani kimeimarishwa. Idadi ya wanafunzi wa ngazi ya cheti imeongezeka kutoka 300 mwaka 2010 hadi 741 mwaka 2014. Mafunzo ya Stashahada katika fani ya uzalishaji mifugo na uzalishaji wa mazao na kilimo mjumuisho yameanza kufundishwa;

(i) Kituo cha Utafiti cha Kizimbani kimepandishwa hadhi kuwa Taasisi kamili ya Utafiti wa Kilimo. Ujenzi wa maabara mpya ya utafiti wa zao la mpunga na ukarabati wa maabara ya udongo na maabara ya usarifu wa mazao umekamilika. Mbegu nne mpya za muhogo na mbili za viazi vitamu vyenye viini lishe na kustahamili ukame zimegunduliwa;

(j) Jumla ya miche 3,500,000 ya mikarafuu imeoteshwa katika vitalu mbalimbali vya Serikali. Kati ya hiyo miche 2,216,328 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.4 imetolewa kwa wakulima bila ya malipo. Kiwango cha uzalishaji wa karafuu kimeongezeka kutoka tani 2,673 mwaka 2010 hadi kufikia tani 5,340 mwaka 2014. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 50;

(k) Jumla ya tani 11,477 za karafuu zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 130.82 zimesafirishwa na kuuzwa nje ya nchi. Bei ya kuuzia karafuu kwa wakulima imeongezeka kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 14,000 kwa kilo moja. Bei hiyo ni sawa na asilimia 80 ya bei ya karafuu katika soko la dunia; na

(l) Jumla ya miche ya minazi mirefu 89,200 (Unguja 52,900 na Pemba 36,300) imeoteshwa na kupandwa katika kipindi cha 2010 hadi 2014.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akiangalia zao la karafuu alipotembelea katika shamba la Bw.Said Sinani (hayupo pichani) Chumbageni - Kusini Pemba akiwa katika ziara maalum*

72. **Kwa kutambua kwamba bado zipo changamoto zinazowakabili wakulima walio wengi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015 - 2020), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wa CCM itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za kilimo bora kwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji pamoja na programu ya mapinduzi ya kilimo na usimamizi wa raslimali za misitu;

(b) Kuongeza idadi ya Mabwana/Mabibi shamba kutoka 172 mwaka 2014 hadi kufikia mmoja kwa kila Shehia ifikapo mwaka 2020 na kuendeleza mafunzo kwa wakulima na kutilia mkazo matumizi ya Kanuni za Kilimo Bora katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na matumizi ya zana za kisasa;

(c) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Kilimo cha Umwagiliaji maji na kuimarisha eneo la hekta 2,105 za miundombinu ya umwagiliaji maji katika bonde la Cheju, Kilombero, Chaani, Mlemele na Makwararani;

(d) Kuongeza uzalishaji na ubora wa zao la karafuu pamoja na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hususan manjano, hiliki, tangawizi, pilipilimanga, kungumanga, kilimo cha alizeti na kuanzisha mazao mapya ya biashara;

(e) Kuimarisha vituo vya huduma na udhibiti wa maradhi ya mazao, wadudu waharibifu pamoja na ukaguzi na karantini dhidi ya maradhi na wadudu waharibifu wa mimea na mifugo ili kudhibiti maradhi ya mimea na mifugo nchini;

(f) Kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula, biashara, mboga mboga na matunda na kuhakikisha kwamba, matumizi ya takwimu na matokeo ya utafiti huo yanawafikia wakulima na kutumika kufanya maamuzi;

(g) Kukiimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani ili kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo na mifugo nchini kwa kukifanya kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA);

(h) Kuhamasisha Sekta Binafsi kujenga viwanda vya usarifu wa mazao ili kuongeza thamani na ubora wa mazao ya mboga na matunda, nazi na karafuu ili kukuza kipato cha wakulima na kurahisisha upatikanaji wa soko;

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula ili kujikinga na balaa la njaa na ukosefu wa chakula na lishe; na

(j) Kuwawezesha wakulima kumudu gharama za matumizi ya teknolojia katika kuongeza ufanisi wa matumizi ya ardhi na uzalishaji wenye tija kupitia utekelezaji wa programu ya kuwawezesha wakulima wa vijijini.

**Ufugaji**

73. Umuhimu wa ufugaji bora na wa kisasa unazingatia haja ya kuongeza tija na ubora wa mazao ya mifugo kutokana na uhaba wa ardhi, ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Sekta ya Mifugo imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Wafugaji 23,393 wa ng'ombe, mbuzi na kuku wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu pamoja na mbinu za ufugaji wa kisasa. Pia vituo vya wafugaji 570 vimeanzishwa ili kutoa mafunzo kwa wafugaji;

(b) Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 4,343,351 mwaka 2010 hadi 27,243,351 mwaka 2014. Aidha, jumla ya wafugaji 40 wamepatiwa mafunzo ya usindikaji wa mazao ya maziwa. Uzalishaji wa mayai umeongezeka kwa asilimia 14 kutoka 164,270,132 mwaka 2010 hadi 186,870,292 mwaka 2014;

(c) Huduma za upandishaji wa ng'ombe kwa sindano zimeimarishwa. Jumla ya ng'ombe 6,400 wamepandishwa kwa kutumia mbegu za kisasa;

(d) Vituo vya huduma za utibabu wa mifugo vimefanyiwa ukarabati na kupatiwa madawa. Watoa huduma za msingi 42 na madaktari wasaidizi 90, wamepatiwa mafunzo Unguja na Pemba;

(e) Kiwanda kikubwa cha usarifu maziwa cha Azam Dairy kimeanzishwa huko Fumba na tayari kimeanza uzalishaji. Kiwanda hicho kitatoa ajira 200. Aidha, kiwanda kingine cha kusarifu kuku kimeanzishwa huko Maruhubi; na

(f) Wafugaji wameshajiishwa na kupatiwa mafunzo juu ya matumizi ya samadi kama chanzo cha nishati mbadala na kupatiwa utaalamu wa kutumia na kutunza mitambo ya Biogesi. Jumla ya mitambo 32 imejengwa Unguja na Pemba.

74. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), SMZ chini ya uongozi wa CCM itaendelea kuhimiza ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa na nyama, mbuzi pamoja na kuku wa nyama na mayai ili kuongeza tija na kipato cha wafugaji kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Programu mbalimbali za elimu kwa wafugaji ili kuwawezesha wafugaji wadogo kutekeleza kanuni za ufugaji wa kisasa na kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na kukidhi mahitaji na viwango vya soko la ndani na nje;

(b) Kuimarisha vituo vya utafiti na huduma za kinga na tiba za mifugo na kuwapatia wafugaji huduma ya upandishaji wa ng'ombe kwa sindano ili kupata mbegu bora pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kutoa huduma za afya na pembejeo za mifugo;

(c) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ili kuwekeza katika sekta ya mifugo na viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo; na

(d) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa sekta ya mifugo.

**Uvuvi na Mazao ya Baharini**

75. Uvuvi na uzalishaji wa mazao ya bahari ni moja ya shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Uvuvi imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Vikundi 167 vya wavuvi wadogo wadogo na vikundi 48 vya Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo pamoja na msaada wa vifaa mbalimbali vya uvuvi. Leseni za uvuvi 32,500 zimetolewa na vyombo 10,210 vimesajiliwa ambapo tani 148,535 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 572.5 zimevuliwa;

(b) Vikundi 144 vya Uvuvi na Ufugaji wa Viumbe vya Baharini (samaki, kaa na majongoo) vikiwemo vile vya ufugaji wa chaza na lulu vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo, vitendea kazi pamoja na vifaranga vya samaki 33,081. Mabwawa sita (6) ya mfano (mashamba darasa) ya kufugia samaki yamejengwa Unguja na Pemba na wajasiriamali 59 wa mazao ya baharini walipelekwa China ili kupata mafunzo ya ufugaji wa mazao ya baharini;

(c) Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi zimeandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kanuni hizo zinahusu maeneo ya zamani ya MENAI, MIMCA na PECCA pamoja na maeneo mapya ya Tumbatu na Changuu - Bawe. Pia ulinzi shirikishi umeimarishwa kwa kuanzisha kitengo cha kusimamia maeneo yote ya hifadhi za baharini na kuanzisha Kamati za Doria Vijijini;

(d) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Bahari (IMS) na Kampuni ya ununuzi wa mwani ya Birr, utafiti umefanywa juu ya uwezekano wa kulima mwani aina ya *"cottonii"* kwenye kina kirefu cha maji huko Fundo, Shumba Mjini, Mkia wa Ng'ombe, Tumbe na Makangale Pemba na kubaini mafanikio

mazuri. Jumla ya tani 51,687 zenye thamani ya shilingi bilioni 18.7 zimezalishwa na kusafirishwa nje ya nchi;

(e) Ili kuwaendeleza wakulima wa mwani, jumla ya vihori 100 vimetolewa kwa njia ya mkopo. Vihori hivyo vimetolewa kwa vikundi 50 vya Wanawake wanaolima mwani kwa wingi katika vijiji 10 vya Unguja ili kurahisisha usafirishaji wa mwani kutoka baharini. Vile vile, mashine za kukaushia mwani na matunda kwa nguvu za jua baada zimeanza kutumika; na

(f) Idadi ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu imeongezeka kutoka 23 mwaka 2009/2010 hadi 77 mwaka 2013/2014. Mapato yatokanayo na leseni hizo, nayo yameongezeka kutoka shilingi billion 1.12 mwaka 2009/2010 hadi kufikia shilingi bilioni 3.30 mwaka 2013/2014.



*Kilimo cha Mwani ni moja ya kilimo kinacholimwa na Wananchi walio kando ya bahari kutokana na kipato chake husaidia wakulima wa Zao hilo, Kama wanavyoonekana Wakinamama wa Kijiji cha Kojani wakiwa katika eneo lao la kilimo hicho kattiba bahari ya kujani wakipanda mwani. kilimo hicho katika bahari ya kujani wakipanda mwani.*

76. **Kwa kutambua mchango mkubwa wa uvuvi na mazao ya baharini katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar na kipato cha mwananchi, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020) kitaielekeza SMZ kuendeleza uvuvi na mazao ya baharini kwa kasi zaidi kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Uvuvi ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na uhifadhi wa mazingira na kuendeleza jitihada za kuwahamasisha wavuvi wadogo kuanzisha vikundi vya ushirika na kuwapatia mafunzo na mikopo nafuu ya zana za kisasa ili kuongeza mapato yao;

(b) Kuandaa Mpango na mazingira ya kuvutia Sekta Binafsi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu, utengenezaji wa boti za uvuvi, ujenzi wa vyumba vya baridi (cold rooms) pamoja na viwanda vya kusindika samaki. Aidha, wavuvi hasa vijana watahamasishwa na kupatiwa mafunzo na zana za kisasa zitakazowawezesha kuvua katika kina kirefu cha maji;

(c) Kuendelea kununua vihori 500 vya kubebea mwani na kuvisambaza kwa wakulima wa mwani 3,000 Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa mwani na kuhamasisha wafugaji wa samaki, chaza, kaa, kamba na majongoo ili kuendeleza uzalishaji wa mazao hayo na kusimamia utafutaji wa masoko;

(d) Kuendelea kusimamia mpango shirikishi wa maeneo ya hifadhi ya bahari yakiwemo maeneo ya Tumbatu, Chumbe-Bawe, Menai na MIMCA kwa Unguja na Kisiwa Panza, Kokota na Mwambe kwa PECCA-Pemba; na kuhakikisha kwamba, jamii inayozunguka maeneo hayo inanufaika na uhifadhi huo; na

(e) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa pamoja zitaandaa Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu ili kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi wa bahari kuu, kujenga

viwanda vya kusindika samaki, kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Uvuvi na kujenga Bandari ya Uvuvi.

**Maliasili**

77. Visiwa vya Unguja na Pemba vimesheheni utajiri wa maliasili ambazo ni kivutio kikubwa cha watalii. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Sekta ya Maliasili imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Mpango wa Matumizi ya Misitu, Sera ya Misitu na Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Rasilimali za Misitu umeandaliwa ili kuimarisha udhibiti na uhifadhi wa maliasili zikiwemo rasilimali za misitu, maliasili zisizorejesheka, wanyama pori pamoja na bayoanuai. Aidha, wananchi wameshirikishwa kikamilifu katika usimamizi na uhifadhi wa maeneo tengefu ya Jozani na Ngezi pamoja na misitu ya asili ya Masingini, Msitu Mkuu na Kiwengwa.

(b) Ushirikishwaji wa wananchi umefanyika katika utunzaji na uhifadhi wa wanyama adimu walio katika hatari ya kutoweka hususan Kima Punju, Popo wa Pemba na Paa Nunga. Maeneo mapya ya hifadhi ya Kima Punju huko Muyuni na Jambiani yameanzishwa. Jumla ya mikataba 50 ya usimamizi wa misitu ya jamii na matumizi endelevu ya maliasili imefikiwa kati ya Serikali na wananchi. Chini ya mikataba hiyo, kaya 4,500 zimepatiwa majiko ya gesi bila ya malipo; na

(c) Wananchi wamehamasishwa kuanzisha miradi ya ufugaji wa nyuki ambapo jumla ya mizinga ya kisasa 3,000 imesambazwa kwa wafugaji na kupatiwa fursa ya soko la ndani na nje ya nchi.

78. **Ili kuendeleza zaidi sekta ya maliasili, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu na Uhifadhi wa Raslimali zisizorejesheka na kutoa taaluma ya udhibiti wa raslimali hizo kwa jamii;

(b) Kuimarisha maeneo ya hifadhi na usimamizi wa wanyama pori walio katika hatari ya kutoweka wakiwemo Paa Nunga, Kima

Punju na Popo wa Pemba ili kuongeza idadi ya wanyama hao na kuimarisha utalii wa kimaumbile *(eco-tourism)*;

(c) Kusimamia matumizi endelevu ya rasimali za misitu ya jamii na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali kutoka tani 5 mwaka 2014, hadi kufikia tani 10 mwaka 2020; na

(d) Kuendeleza kazi ya uatikaji na usambazaji wa miche ya misitu na kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti.



*Katibu Mkuu wa CCM Ndg. Abrahaman Kinana akijumuika na wananchi wa kikundi cha kuhifadhi Mazingira Fuoni Kibondeni katika upandaji wa miti ya mikoko ili kutunza mazingira ya eneo hilo, akiwa katika ziara yake kukagua miradi ya maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM*

**Mazingira na Mabadiliko Tabianchi**

79. Mazingira ni suala mtambuka ambalo linagusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, upo uhusiano tegemezi kati ya mazingira na maendeleo na kwamba uharibifu wa mazingira si tu husababisha umasikini, bali umasikini nao husababisha uharibifu wa mazingira. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamepatikana mafanikio kutokana na utunzaji na uhifadhi wa mazingira kama ifuatavyo:-

   (a) Sera ya Mazingira ya mwaka 1992 imefanyiwa mapitio na Sera Mpya ya Mwaka 2013 imezinduliwa. Ili kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 1996 imefanyiwa marekebisho na Sheria Mpya ya Mazingira ya Mwaka 2015 pamoja na Kanuni ya Usimamizi wa Maliasili zisiorejesheka na Kanuni ya Marufuku ya Mifuko ya Plastiki zimepitishwa;

   (b) Jumla ya miradi 221 imefanyiwa ukaguzi wa kimazingira na kupatiwa ushauri wa kitaalamu. Miradi mingine 32 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini ya kimazingira na kupatiwa vyeti vya mazingira;

   (c) Jumla ya miche 6,020,861 ya misitu na miti ya matunda imesambazwa na kupandwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo yaliyoathirika kwa uchimbaji wa mchanga, uchimbaji wa kifusi na matofali ya mawe; na

   (d) Utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi umefanyika. Maeneo 148 (Unguja 25 na Pemba 123) yamebainika kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwa kuingiwa na maji ya chumvi kutokana na kupanda kwa kina cha bahari.

80. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kuendeleza udhibiti wa hifadhi ya mazingira kwa kutekeleza yafuatayo:-**

   (a) Kuendelea kusimamia Sera na Sheria ya Mazingira na ushirikishwaji wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwenye maeneo yao;

(b) Kufanya tathmini za athari za Kimazingira, ukaguzi wa Kimazingira na ufuatiliaji wa Kimazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi;
(c) Kusimamia mabadiliko ya tabianchi na elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira;
(d) Kuanzisha vituo viwili vya usarifu wa taka ngumu (Unguja 1 na Pemba 1) kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kuzalisha ajira kwa vijana; na
(e) Kukamilisha ujenzi wa ukuta katika kingo za barabara ya Mizingani ili kuzuia athari za mmomonyoko wa ardhi unaosababishwa na bahari.

**Utalii**

81. Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vyenye historia na vivutio mbalimbali vya utalii zikiwemo fukwe za kuvutia, misitu ya asili, wanyama adimu, magofu na urithi wa kimataifa wa Mji Mkongwe. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Sekta ya Utalii imepata mafanikio yafuatayo:-
(a) Sheria ya Kamisheni ya Utalii imefanyiwa marekebisho na Kanuni za Sheria ya Kamisheni ya Utalii na ile ya Chuo cha Utalii zimepitishwa na kuanza kutumika. Chini ya sheria hio mpya (Sheria Na. 7/2012) Kamati za Utalii za wilaya zimeanzishwa;
(b) Ofisi ya Uwakala wa Utangazaji Utalii nchini India imeanzishwa na masoko mapya ya utalii ya India, China, Uturuki na Urusi yameibuliwa. Kutokana na hatua hizo, watalii 1,863 kutoka India, 2001 kutoka China na 840 kutoka Uturuki walipokelewa;
(c) Idadi ya watalii walioingia Zanzibar imeongezeka kutoka 132,836 mwaka 2010 hadi 310,500 mwaka 2014. Kukamilika kwa ujenzi wa chumba cha chini ya bahari katika hoteli ya Manta Reef huko Makangale Pemba ni moja ya kivutio kikubwa cha watalii;
(d) Utafiti wa kiikolojia kwenye Ngome ya Mazrui – Chwaka na Tumbe (Pemba) na Ngome Kongwe na Forodhani (Unguja) umefanyika. Maeneo mapya manane (8) ya kihistoria yakiwemo Kiumbi, Kiwengwa, Muyuni, Dimani, Mwanampambe, Mwana wa Mwana, Tazari na kijiji kilichozama Mkumbuu yameibuliwa. Jengo la

Makumbusho ya Hamamni Baths yamefanyiwa ukarabati ili kulirudisha katika hali yake ya awali;

(e) Uhakiki wa hoteli na kuzipangia madaraja umefanyika. Hoteli 71 zilifikia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki zikiwemo hoteli za nyota tano 16, nyota nne tisa, nyota tatu 43 na nyota mbili sita; na

(f) Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimeimarishwa. Jumla ya wahitimu 983 (wanawake 386 na wanaume 597) wamehitimu masomo yao katika ngazi ya Shahada na Stashahada. Walimu sita wamepatiwa mafunzo ya juu.




*Watalii wanaotembelea katika Visiwa vya Zanzibar hupata fursa za kutembelea maeneo ya Historia na vivutio vya Utalii ndani ya Zanzibar na vitongoji vyake. Kama wanavyoonekana Watalii hawa waliofika Zanzibar wakipata historia ya Nyumba ya Marcury ilioko*

*katika mtaa wa shangani ndani ya mji mkongwe wa Unguja.Wageni wengi wanaotembelea Zanzibar hufika katika nyumba hii ikiwa katika medali ya historia ya Zanzibar*

82. **Ili kuendeleza Sekta ya Utalii na kuifanya iwe endelevu na kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kufanya mapitio ya Sera ya Utalii na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazohusiana na sekta hii pamoja na kuandaa mpango wa kukusanya taarifa na takwimu za idadi ya hoteli na taarifa nyingine ili kufahamu thamani halisi ya mchango wa sekta kwenye Pato la Taifa;

(b) Kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha miradi ya ujenzi wa hoteli za kitalii hususan hoteli za daraja la kwanza na kuongeza idadi ya watalii wanaoingia Zanziabr kutoka 310,500 mwaka 2014 hadi 500,000 mwaka 2020;

(c) Kuimarisha kikosi maalumu cha ulinzi na ushirikishwaji wa wananchi kwa kuanzisha vituo vitatu vya utoaji taarifa zikiwemo za uhalifu ili kuimarisha usalama wa watalii wanaotembelea Zanzibar;

(d) Kuendeleza utalii wa kumbukumbu za kihistoria, kiutamaduni na kimaumbile wenye kutunza mazingira na kuibua maeneo mapya likiwemo jengo la "Living Stone House"(Kinazini), jengo la Tip Tip (Forodhani), jengo la Baraza la Kutunga Sheria "Legislative Council" (Mnazi Mmoja) na jengo la Mwinyimkuu (Dunga) ili kuongeza idadi ya watalii na muda wa kukaa nchini;

(e) Kuendeleza jitihada ya kuvitangaza vivutio vya utalii kwa kuanzisha Kitengo cha Masoko, Ofisi tatu za kutangaza utalii, kuanzisha masoko kwa njia shirikishi na mtandao na kufanya utafiti ili kuibua masoko mapya hasa katika Bara la Asia na Mashariki ya Kati;

(f) Kuimarisha bidhaa na huduma za utalii kwa kuanzisha vituo 10 vya huduma na bidhaa za utalii zinazotokana na asili ya Mzanzibari sambamba na utoaji wa huduma kwa watalii katika bustani nane za kimaumbile zitakazozalisha ajira 1,000;

(g) Kuihamasisha jamii kushiriki katika utalii wa ndani na kutoa mafunzo kwa vijana 680 ili kuwawezesha kujiajiri wenyewe kupitia Sekta ya Utalii na kutengeneza ajira 100,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja; na

(h) Kukiunganisha Chuo cha Utalii na SUZA ili kutoa mafunzo ya Shahada ya Utalii.

**Viwanda na Biashara**

83. Uchumi wa viwanda una nguvu kubwa ya kuziwezesha sekta nyingine za uchumi kuingia katika mkondo wa uchumi wa kisasa. Aidha, Sekta ya Biashara ina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Viwanda na Biashara imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Sera ya Biashara imefanyiwa mapitio na Sheria Mpya ya Utoaji Leseni za Biashara na Usajili imepitishwa. Aidha, sheria ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji, sheria ya mizani na vipimo na sheria ya biashara zimefanyiwa mapitio;

(b) Miradi 817 ya viwanda na ya wajasiriamali imekaguliwa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu. Wazalishaji wadogo wadogo 189 (Unguja 119 na Pemba 70) wamepatiwa mafunzo juu usindikaji mazao, ujasiriamali, kuongeza thamani ya mazao na mbinu za kuendeleza biashara zao. Vikundi 500 vya wajasiriamali vimeweza kushiriki katika maonesho ya Kikanda na Kimataifa;

(c) Sheria mpya ya Biashara imepitishwa. Chini ya Sheria hiyo, Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) na Alama ya Utambulisho (logo) na Alama ya Ubora wa Bidhaa (Standard Mark) ambayo itaonesha ubora wa bidhaa hizo pia imeanzishwa ili kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa nchini na kukuza masoko ya ndani na nje;

(d) Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kimepatiwa mwekezaji na kimefanyiwa ukarabati mkubwa pamoja na kupatiwa mashine mpya na kuimarisha mashamba ya miwa. Jumla ya wafanyakazi 350 wameajiriwa na usindikaji wa sukari tayari umeanza;

(e) Kiwanda cha Makonyo huko Pemba kimeimarishwa kwa kupatiwa mashine mpya ya kupimia ubora wa mafuta ya mimea *(Gas Chromolography)* na mashine ya kuwekea mafuta kwenye ujazo mdogo. Kiwanda pia kimeingia makubaliano ya kibiashara na Kampuni ya Land ya Japan ili kuuza mafuta ya mimea katika soko la Japan;

(f) Mradi wa Tasnia Chapa *(Branding)* umeanzishwa ili kuilinda na kuipa hadhi zaidi karafuu ya Zanzibar na kuitangaza Zanzibar kupitia bidhaa nyingine za viungo zikiwemo mdalasini, pilipili hoho na pilipili manga; na

(g) Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC) limefanyiwa mabadiliko makumbwa ambapo:-

(i) Zao la karafuu halikubinafishwa na mpango wa kuliendeleza umetayarishwa;

(ii) Magendo ya karafuu yamepungua sana kutokana na ushirikishwaji wa wananchi; na

(iii) Sheria ya maendeleo ya karafuu na Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu umeanzishwa.

84. **Ili kuendeleza shughuli za viwanda na biashara na kuinua Uchumi wa Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati na kuandaa vivutio kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vikubwa;

(b) Kuandaa mkakati wa kuendeleza Sekta Binafsi pamoja na programu ya kuwakuza wawekezaji wa ndani na wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati (SME’s) kwa kuwapatia mafunzo,

mitaji na huduma za kiufundi ili kuzalisha bidhaa bora zenye kukabili ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi;

(c) Kuendeleza viwanda chini ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ) na kuwavutia wawekezaji wenye mitaji mikubwa kuwekeza katika miundombinu ya viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi, vikiwemo viwanda vya kushona nguo, usindikaji mazao, usindikaji samaki na viwanda vya kusarifu (kuchakata) mazao ya kilimo na mifugo;

(d) Kufanya mapitio ya Sera ya Biashara ya Mwaka 2006, kuandaa Sera Mpya ya Biashara na kuanzisha chombo maalumu cha kuwaendeleza wajasiriamali wadogo na kufanya utafiti juu ya gharama za biashara kwa lengo la kuchochea ukuaji wa biashara na kuondosha urasimu katika utoaji wa leseni;

(e) Kuimarisha utengamano wa kikanda (EAC, SADC, IOR, ACP) na kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya EAC, SADC na AGOA na kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Nje (Zanzibar National Export Strategy);

(f) Kuanzisha na kuendeleza ujenzi wa Kiwanja cha Maonyesho ya Biashara cha Kimataifa na kuhamasisha ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ndani na nje ya nchi;

(g) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko na kufanya utafiti wa masoko na bei ili kupanua wigo wa mahitaji ya masoko mbalimbali. Aidha, wajasiriamali watapatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo na mbinu za kuweza kuyafikia masoko hayo; na

(h) Kusimamia utekelezaji wa Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) na kukamilisha mkakati wa utambulisho wa karafuu ya Zanzibar na uhamasishaji matumizi ya tasnia malibunifu *(Intellectual Property Right)* ili kuendeleza tija.

**Vyama vya Ushirika**

85. Vyama vya Ushirika bado vina nafasi muhimu katika kuwaunganisha na kuwawezesha wananchi kubadili maisha yao na kujiendeleza kiuchumi. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) ni nyenzo ya kuwapatia wananchi mitaji kutokana na michango yao na mikopo kutoka katika vyombo na taasisi za fedha. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), utekelezaji wa Sera na Sheria ya Vyama vya Ushirika imefanyika na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Vyama vipya vya Ushirika 749 vimesajiliwa zikiwemo SACCOS 16, na vyama vya uzalishaji mali na huduma 826. Idadi ya vyama vya ushirika imefikia 2,493 vikiwa na jumla ya wanachama 39,664 Unguja na Pemba;

(b) Vyama vya ushirika 485 vimefanyiwa ukaguzi wa hesabu na ripoti za ukaguzi huo kuwasilishwa kwenye Mikutano Mikuu ya vyama hivyo. Aidha, Vyama vya Ushirika 2,243 vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida ili kutathmini hali ya uendeshaji, utekelezaji wa sheria na uandishi wa vitabu vya hesabu;

(c) SACCOS 203 zimefanyiwa uthamini na kupangiwa madaraja ya ubora. Mtaji wa SACCOS hizo umefikia shilingi bilioni 3.5. Jumla ya SACCOS 17 zimeunganishwa na taasisi mbalimbali za fedha na kuweza kupatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3 ili kuimarisha mitaji katika biashara zao; na

(d) Jumla ya wanachama 13,953 wakiwemo wanawake 8,923 na wanaume 5,030 wamepatiwa mafunzo ya aina mbalimbali juu ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Aidha, Sekta ya Ushirika imeweza kutoa ajira binafsi 6,835 (wanawake 2,948 na wanaume 3,887) kutokana na Vyama vya Ushirika 88.

86. **Ili kuendeleza Sekta ya Ushirika, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuifanyia mapitio Sera ya Vyama vya Ushirika na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na upatikanaji wa takwimu zitakazosaidia kuandaa mipango na kuleta

mageuzi katika Sekta ya Ushirika na kuimarisha uchumi wa Taifa;

(b) Kufanya usajili wa vyama vipya vya ushirika 600 vya uzalishaji (kilimo, mifugo, viwanda vidogo vidogo, uvuvi na huduma) pamoja na SACCOS 50 kubwa;

(c) Kuziimarisha SACCOS na Asasi Ndogo za Fedha kwa kuzipatia mafunzo ya kitaaluma, uongozi na kuwaongezea mitaji ili ziweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi kwa lengo la kuongeza ajira;

(d) Kuwapatia mafunzo ya uongozi na uendeshaji wanachama 15,000 wakiwemo viongozi 3,000 na wanachama 12,000 wa vyama vya ushirika na kuvifanyia ukaguzi vyama 3,000 vya ushirika; na

(e) Kusimamia uanzishaji na kuviimarisha vyama vikuu vitatu vya kisekta (kilimo na masoko, kazi za mikono na huduma) ili kujenga sauti ya pamoja na utoaji wa huduma muhimu za kisekta katika kuendeleza Vyama vya Ushirika vya Msingi.

**Sekta za Miundombinu ya Kiuchumi**

87. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Miundombinu imepata mafanikio yafuatayo:-

**Barabara**

(a) Jumla ya Kilomita 656 (Unguja Km. 430 na Pemba 226) za barabara za lami zilizokwishajengwa zimefanyiwa matengenezo;

(b) Ujenzi wa barabara ya Mfenesini hadi Bumbwini (Km.13) na barabara ya Welezo hadi Dunga (Km. 12.75) kwa kiwango cha lami umekamilika. Vile vile, Kilomita 108.9 za barabara za Pemba zimejengwa kwa kiwango cha lami;

(c) Jumla ya Kilomita 124.7 za barabara za Unguja zimejengwa kwa viwango mbalimbali. Kilomita 18 zimejengwa kwa kiwango cha lami Km. 14 kwa kiwango cha changarawe, Km. 12 ujenzi bado unaendelea na km 80.7 zimefanyiwa upembuzi yakinifu na ubunifu wa michoro; na

(d) Kwa upande wa Pemba, jumla ya Km. 203.4 za barabara zimejengwa kwa viwango mbalimbali. Kilomita 103.0 zimejengwa kwa kiwango cha lami, Km. 60.3. kwa kiwango cha changarawe na Km. 40.1 zimefanyiwa upembuzi yakinifu pamoja na michoro.




*Barabara mpya ya Amani – Mtoni ambayo ilifunguliwa rasmi na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi wakati wa maadhimisho ya kutimiza miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar.*

88. **Ili kuendeleza kazi ya kuimarisha miundombinu ya barabara, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa SMZ inatekeleza kazi zifuatazo:-**

(a) Kuendeleza kazi ya utunzaji na matengenezo ya barabara zilizokwisha kujengwa na kufanya marekebisho katika maeneo yanayotuama maji ya mvua na kuathiri ubora wa barabara hizo;

(b) Kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Jendele–Cheju–Kaebona (km 11.7) na Koani –Jumbi (km 6.3)

kwa Unguja na barabara ya Ole – Kengeja (Km 35), Mkanyageni – Kangani (Km 6.5), Finya – Kicha (Km 8.8) na Mgagadu - Kiwani (Km 7.6) kwa Pemba;

(c) Kujenga jumla ya kilomita 160.8 za barabara kwa kiwango cha lami Unguja na kilomita 51.1 za barabara kwa kiwango cha lami huko Pemba kwa mpango ufuatao:-

(i) **Unguja**

- Matemwe – Muyuni (Km 7.6)
- Kichwele – Pangeni (Km 4.8)
- Kinduni – Kichungwani – Kitope (Km 3.5)
- Umbuji – Uroa (Km 6.9)
- Fuoni – Kombeni (Km 8.6)
- Jozani – Charawe – Ukongoroni – Bwejuu (Km 23.3)
- Mkwajuni – Kijini (Km 9.4)
- Pale – Kiongole (Km 4.6)
- Malindi Port – Kinazini – Mtoni – Bububu (Km 11.2)
- Creek road – Mkunazini – Mnazimoja (Km 1.3)
- Tunguu – Fuoni – Magomeni – Kariakoo – Mkunazini (Km 16.3)
- Welezo – Amani - Ng'ambo (Km 2.9)
- Mtoni – Amani – Kiembesamaki (Km 8.5)
- Airport – Kiembesamaki – Kilimani - Mnazimmoja (Km 6.6)
- Bububu – Mahonda – Mkokotoni (Km 31)
- Kizimbani – Kiboje (Km 7.2)
- Melitano - Kwarara (Km 1)
- Kijitoupele – Fuoni – Mambosasa (Km 2.5)
- Sharifumsa – Mwanyanya - Bububu Skuli (Km 3.6)

(ii) **Pemba**

- Chake – Wete (Km 22.1)
- Mkoani – Chake (Km 27)
- Mji wa Wete (Km 2)

(d)Kuendeleza kazi ya uwekaji wa taa za kuongoza magari kwa kuweka taa sita (Unguja nne (4) na Pemba mbili (2) ili kupunguza

msongamano wa magari katika baadhi ya maeneo ya miji hususan Zanzibar, Wete na Chake Chake Pemba; na

(e) Kuimarisha Karakana Kuu ya Serikali kwa mashirikiano na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi na utoaji wa huduma bora za kiufundi kwa Taasisi mbalimbali za Serikali na watu binafsi.

**Bandari**

89. Bandari ni mlango mkuu wa biashara na chachu ya ukuaji wa uchumi wa Taifa na wananchi kwa jumla. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), mafanikio yaliyofikiwa kwenye eneo la bandari ni kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Bandari kwa kushirikiana na Kampuni ya *AZAM MARINE* limejenga majengo ya kuhudumia abiria likiwemo jengo la Watu Mashuhuri *(VIP)* katika Bandari ya Malindi, pamoja na kuimarisha huduma nyingine za abiria;

(b) Eneo la kuhifadhia makontena lenye ukubwa wa kilomita za mraba 6,000 katika Bandari ya Malindi limefanyiwa matengenezo ili kuongeza ufanisi. Aidha, vifaa na mitambo mipya ya kisasa imenunuliwa;

(c) Matengenezo makubwa yamefanyika katika gati ya Mkoani Pemba. Kiungo cha gati hiyo ambacho kiliathirika kutokana na nguvu za mawimbi ya meli pia kimefanyiwa matengenezo;

(d) Ili kuimarisha gati ndogo ya Mkokotoni, kazi ya uchunguzi wa athari za kimazingira imekamilika. Aidha, mpango wa ujenzi wa gati hiyo tayari umeandaliwa; na

(e) Kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri imekamilika. Mjenzi wa Bandari hiyo, Kampuni ya China *(Harbour Engineering Company)* ameteuliwa na fedha kwa ajili ya ujenzi huo tayari zimepatikana.

90. **Ili kuendeleza na kuimarisha bandari katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kwamba, SMZ inatekeleza kazi zifuatazo:-**

(a) Kukamilisha ujenzi wa bandari mpya ya kuhudumia mizigo katika eneo la Mpigaduri na kuiendeleza Bandari ya Malindi kwa kuongeza vifaa vya huduma kwa abiria pamoja na mizigo;

(b) Kuimarisha na kuendeleza Bandari ya Mkoani-Pemba kwa kuipatia vifaa vya kisasa vya kuhudumia abiria na mizigo. Aidha, kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, gati ya Wete itaimarishwa;

(c) Kuimarisha gati ya Mkokotoni kwa kukamilisha kazi ya ujenzi wa jeti kwa ajili ya huduma za usafiri wa wananchi wa Tumbatu na usafirishaji wa mizigo kwa majahazi; na

(d) Kuliimarisha Shirika la Meli ili lijiendeshe kibiashara na kununua meli nyingine mpya ya abiria na moja ya mafuta.

**Usafiri wa Baharini**

91. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Sheria ya kuanzisha Shirika la Meli la Zanzibar imefanyiwa mapitio na sheria mpya imepitishwa. Mpango wa mageuzi ya kimuundo na uendeshaji umeanza kutekelezwa. Jumla ya meli mbili za Shirika hilo; M V. Maendeleo na M V.Ukombozi zimefanyiwa matengenezo makubwa;

(b) Serikali imenunua meli mpya ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 200 za mizigo ili kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi hususan kati ya Kisiwa cha Unguja na Pemba;

(c) Ofisi ya Mrajisi wa Meli na Mamlaka ya Usafiri wa *Baharini "Zanzibar Maritime Authority"* (ZMA) imeimarishwa. Kwa kushirikiana na SUMATRA na mamlaka hiyo imeweza kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya baharini na kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za mara kwa mara za vyombo vya baharini; na

(d) Wawekezaji wa ndani na nje wameendelea kushajiishwa ili kuwekeza katika sekta ya usafiri wa baharini. Jumla ya

kampuni 23 tayari zimewekeza katika sekta ya usafiri wa baharini.

92. **Ili kuendeleza na kuimarisha usafiri wa baharini, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itahakikisha kwamba, SMZ inaendelea kusimamia Utekelezaji wa Sheria na Kanuni za usafiri wa baharini ili kupunguza ajali za vyombo vya baharini kwa kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA).**

**Usafiri wa Anga**

93. Uimara wa Sekta ya Usafiri wa Anga huchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Sekta ya Utalii, biashara na kukuza uchumi wa nchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Ujenzi wa jengo jipya na eneo la maegesho ya ndege umeanzishwa ili kukiimarisha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume. Kazi ya ujenzi wa maegesho na njia za kurukia ndege umekamilika;

(b) Ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilomita 8.59 unaozunguka Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume umekamilika; na

(c) Hali ya usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume imeimarishwa. Vifaa vya ukaguzi vikiwemo *"walk through doors, x - ray machine, hand held metal na under search mirrors"* vimenunuliwa. Pia wafanyakazi wa kada mbalimbali wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na kazi zao.

94. **Ili kuiendeleza Sekta ya Usafiri wa Anga katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020) CCM itahakikisha kwamba, SMZ inatekeleza kazi zifuatazo:-**

(a) Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume (AAKIA) ili

kuongeza idadi ya abiria wanaotumia kiwanja hicho, kiwango cha mizigo na kuongeza mapato ya Serikali;

(b) Kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za abiria, ndege na mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Karume-Pemba ikiwemo kuongeza urefu na uwekaji wa taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege, huduma za umeme na kukamilisha ujenzi wa uzio; na

(c) Kuendelea kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa wafanyakazi wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba pamoja na kuimarisha huduma za zimamoto na usalama wa viwanja vya ndege.

**Nishati**

95. Sekta ya Nishati hususan umeme, ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Aidha, matumizi ya nishati ya umeme hurahisisha shughuli nyingi za kiuchumi, kuongeza kasi ya uzalishajimali na kuwawezesha wananchi kujiajiri wao wenyewe. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Sera ya Nishati imeanzishwa na Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo umeandaliwa. Aidha, Sheria ya Udhibsiti wa huduma za Maji na Nishati (ZURA) imepitishwa;

(b) Mradi wa ujenzi wa njia ya pili ya umeme inayopita chini ya bahari kutoka Ras Kiromoni-Tanzania Bara hadi Fumba-Unguja (Mradi wa MCC) umekamilika na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme kutoka Megawati 45 hadi kufikia Megawati 145 kwa Unguja;

(c) Kazi ya ujenzi wa njia ya umeme ya megawati 20 inayopita chini ya bahari kutoka Tanga hadi Pemba (Mradi wa NORAD) imetekelezwa na kumaliza kabisa tatizo la umeme katika kisiwa hicho;

(d) Njia kubwa ya Umeme yenye urefu wa kilomita 5.2 imejengwa katika vijiji vya Kibonde Maji na Pongwe kwa Unguja na Kivugo na Kichuwani kwa Pemba. Aidha, vijiji 129 vimefikishiwa huduma ya umeme Unguja na Pemba sawa na asilimia 105 ya lengo lililowekwa (vijiji 123);

(e) Vyanzo vya nishati mbadala ya umeme ukiwemo umeme wa jua, mawimbi ya bahari, upepo na gesi asilia vimefanyiwa uhakiki. Kampuni kutoka Italia imeteuliwa kuanza utafiti katika maeneo hayo; na

(f) Vijana 32 wanaendelea kupatiwa mafunzo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwatayarisha kwa ajili ya kuendeleza sekta ya mafuta na gesi asilia.

96. **Ili kuimarisha Sekta ya Nishati ambayo inajumuisha umeme, nishati mbadala, mafuta na gesi asilia katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), SMZ chini ya uongozi wa CCM itatekeleza kazi zifuatazo:-**

(a) **Umeme na nishati mbadala:**

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Nishati ya Mwaka 2009 na kuendeleza juhudi za upatikanaji wa umeme na nishati mbadala;

(ii) Kuimarisha shughuli za usimamizi wa huduma za umeme na usambazaji wa nishati hiyo mijini na vijijini vikiwemo visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu; na

(iii) Kuimarisha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa lengo la kuliwezesha kujiendesha kibiashara.

(b) **Mafuta na Gesi Asilia:**

(i) Kuandaa Sera na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia;

(ii) Kuendeleza jitihada za kuwajengea uwezo watendaji pamoja na kuhamasisha vijana kujiunga na masomo ya fani ya Mafuta na Gesi Asilia; na

(iii) Kuandaa mpango shirikishi utakaohakikisha kwamba wananchi wananufaika na kupata fursa za kiuchumi na kijamii kutokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

**Ardhi**

97. Ardhi ni raslimali muhimu katika ujenzi wa uchumi wa Taifa. Aidha, moja ya malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, ni kuondoa umiliki wa ardhi mikononi mwa wachache na kuhakikisha

kwamba ardhi yote ya Zanzibar inamilikiwa na wananchi wenyewe na kuwawezesha kuondokana na umasikini, dhuluma na ubaguzi wa kitabaka. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Sera Mpya ya Ardhi imeandaliwa na utoaji wa Hati Mpya za Matumizi ya Ardhi na kuzibadilisha zile za zamani imetekelezwa katika Shehia 20 Unguja na Pemba;

(b) Jumla ya maeneo 3,541 katika Shehia 22 za Unguja na Pemba yamesajiliwa na Mrajis wa Ardhi. Vile vile, nyumba, viwanja na mashamba 22,746 yametambuliwa Unguja na Pemba. Hati Mpya za Ardhi 1,310 na viwanja 1,691 zimetolewa kwa ajili ya matumizi mbalimbali na mikataba 223 ya ardhi imetolewa kwa wawekezaji;

(c) Mapitio na utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi *(National Land Use Plan)* na utayarishaji wa Mpango Kabambe *(Master Plan)* ya Mji wa Zanzibar imetekelezwa;

(d) Kazi ya kufanya mapitio na marekebisho ya ramani ya Zanzibar pamoja na miji ya Zanzibar, Chake Chake, Wete na Mkoani pamoja na visiwa vidogo vidogo imetekelezwa. Ramani mpya ya Kisiwa cha Unguja na Pemba tayari zimechapishwa na kuanza kutumika;

(e) Kazi ya utambuzi wa umiliki wa ardhi katika maeneo ya ukanda wa pwani na fukwe imetekelezwa. Jumla ya wamiliki 1,600 wametambuliwa katika Kijiji cha Nungwi na 1,000 katika Kijiji cha Paje. Maeneo ya Chwaka kwa Unguja na Michenzani kwa Pemba pia yamepimwa. Kazi ya utambuzi wa umiliki wa ardhi katika maeneo ya miji kwa majaribio *(Pilot)* pia imefanyika. Jumla ya wamiliki 6,000 wametambuliwa na kusajiliwa; na

(f) Idadi ya Mahakimu katika Mahakama za Ardhi imeongezeka kutoka watatu (3) hadi sita (6) na Washauri *(Assessors)* kutoka 19 hadi 27. Hatua hiyo imeongeza ufanisi na kasi ya kusikiliza mashauri yanayohusiana na migogoro ya ardhi na

kuyatolea uamuzi. Mahakama ya Ardhi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kusini Pemba pia zimeanzishwa.

98. **Ili kuendeleza Sekta ya Ardhi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa, SMZ inatekeleza malengo yafuatayo:**

(a) Kuendeleza kazi ya Usajili wa Ardhi katika maeneo yote ya Unguja na Pemba kwa mujibu wa Sera na Sheria ya Ardhi. Aidha, ramani zote za visiwa vya Unguja na Pemba zitaendelea kufanyiwa mapitio na marekebisho kwa mujibu wa mahitaji na mabadiliko yatakayojitokeza;

(b) Kuendeleza kazi ya upimaji wa viwanja na utoaji wa Hati kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi *(National Land Use Plan)* pamoja na ramani ya mji na za miji; na

(c) Kuendeleza jitihada za kupunguza migogoro ya ardhi kwa kuimarisha huduma za Mahakama za Ardhi katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Aidha, jamii itaelimishwa juu ya umuhimu wa kutambua na kufuata Sheria mbalimbali za ardhi ikiwemo utambuzi, upimaji na usajili.

## Sekta za Huduma za Jamii

### Elimu

99. Elimu ni moja ya haki ya msingi kwa kila mwananchi na nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya elimu imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) **Elimu ya Maandalizi:**

(i) Idadi ya Skuli za Maandalizi zimeongezeka kutoka 238 mwaka 2010 hadi 279 mwaka 2015. Ujenzi wa Skuli za Maandalizi za Tunduni, Kama, Potoa, Jongowe na Konde umekamilika na skuli ya maandalizi ya Machomane-Pemba imefanyiwa ukarabati mkubwa; na

(ii) Idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 29,732 (15,216 wasichana na 14,516 wavulana) mwaka 2010 hadi 38,808 (19,654 wasichana na 19,154 wavulana) mwaka 2015. Idadi ya walimu 382 wamepatiwa mafunzo ya kusomesha ngazi ya Elimu ya Maandalizi.

(b) **Elimu ya Msingi:**

(i) Ujenzi wa Skuli ya Msingi ya Mwanakwerekwe umekamilika. Idadi ya skuli imeongezeka kutoka 299 mwaka 2010 hadi 359 mwaka 2015. Madarasa mapya 563 yamejengwa, madawati 7,955, viti 2,371 na meza 2,329 zimechongwa na kusambazwa katika madarasa hayo Unguja na Pemba;

(ii) Idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza imeongezeka kutoka 38,743 (19,163 wasichana na 19,580 wavulana) mwaka 2010 na kufikia 43,062 (21,129 wasichana na 21,933 wavulana) mwaka 2015. Walimu wa ngazi ya cheti 949 wameajiriwa na kupelekwa katika skuli za msingi Unguja na Pemba;

(iii) Mazingira ya skuli za msingi yameimarishwa kwa kukarabatiwa na kujengwa njia rafiki ili kuwezesha wanafunzi wenye ulemavu kuingia madarasani kwa urahisi. Jumla ya wanafunzi 203 wenye mahitaji maalumu wameandikishwa na kuanza Elimu ya Msingi; na

(iv) Jumla ya skuli 248 za msingi zimepatiwa kompyuta mbili kila moja kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na skuli 20 zimepatiwa maabara za kuhamishika *(mobile lab)* na pia skuli 25 zimepatiwa vifaa vya kuunganisha mawasiliano *(bridge IT)* Unguja na Pemba.

(c) **Elimu ya Sekondari:**

(i) Idadi ya wanafunzi wa Sekondari (kidato cha 1-4) imeongezeka kutoka 78,165 (41,804 wasichana na

36,361 wavulana) mwaka 2012 hadi 79,662 (43,544 wasichana 36,118 wavulana) mwaka 2014;

(ii) Idadi ya Skuli za Sekondari imeongezeka kutoka 194 mwaka 2010 hadi 213 mwaka 2014. Skuli mpya 19 zimejengwa na madarasa mapya 263 yamejengwa katika skuli mbalimbali za Sekondari Unguja na Pemba;

(iii) Skuli kongwe 6 za Sekondari zimefanyiwa ukarabati mkubwa. Skuli hizo ni Hamamni, Forodhani na Tumekuja kwa Unguja na Utaani, Fidel-Casro na Uweleni kwa Pemba. Ujenzi wa ghorofa ya pili ya Skuli ya Sekondari ya Donge unaendelea. Aidha, nyumba za walimu 27 zimejengwa katika skuli mbalimbali Unguja na Pemba; na

(iv) Jumla ya walimu 10 wamepatiwa mafunzo nje ya nchi, 450 wamepatiwa mafunzo ya kuinua uwezo wao wa kufundisha masomo ya Hisabati na Sayansi na wafanyakazi wa kada nyingine za elimu 2,867 wameendelezwa kwa kupatiwa mafunzo katika vyuo mbalimbali katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada ya uzamili na uzamivu.




*Jengo la Skuli ya Secondary ya  Faraja lililofunguliwa na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Idi Kwamtipura Mjini Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa shamra shamra za Maadhimisho ya miaka 51ya Mapinduzi ya Zanzibar.*

(d) **Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima:**

(i) Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo kimeendelea kutoa mafunzo katika fani tofauti. Idadi ya wanafunzi katika kituo hicho imeongezeka kutoka 246 (wanawake 67 na wanaume 179) mwaka 2011 hadi 305 (wanawake 73 na wanaume 232) mwaka 2015; na

(ii) Jumla ya vikundi vya kiuchumi 250 na wajasiriamali 6,000 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kupitia madarasa ya Elimu ya Watu Wazima, Unguja na Pemba.

(e) **Kuimarisha Huduma za Maktaba:**

(i) Ujenzi wa Maktaba Kuu ya Zanzibar umekamilika. Zabuni ya ujenzi wa Maktaba Kuu, Tawi la Pemba, pia imetangazwa na Shirika la Huduma za Maktaba limeanzishwa; na

(ii) Jumla ya maktaba nane (8) za jamii zimeanzishwa katika maeneo ya Chumbuni, Welezo, Kiembesamaki, Mpapa, Uzini, Fumba, Bweleo na Tumbatu kwa upande wa Unguja kwa mashirikiano na jumuiya isiyo ya kiserikali (MJUKIZA). Aidha, wananchi wamehamasishwa kuanzisha Maktaba za Jamii katika maeneo wanayoishi.

(f) **Vyuo vya Elimu ya Juu:**

(i) Idadi ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Zanzibar University (ZU) na Univesity Collage of Education Zanzibar (UCEZ) imeongezeka kutoka 3,624 mwaka 2010 hadi 6,038 mwaka 2014. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 67;

(ii) Ujenzi wa Chuo Kikuu cha SUZA huko Tunguu umekamilika. Majengo mapya manne (4) yamejengwa na kuwekewa samani, kompyuta na vifaa vya maabara. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imeongezeka kutoka 1,972 (wanawake 853 na wanaume 1119) mwaka 2010 hadi 2,078 (wanawake 1,244 na wanaume 834) mwaka 2015. Wahitimu wa fani mbalimbali nao wameongezeka kutoka 524 (wanawake 347 na wanaume 177) mwaka 2010 hadi 749 (418 wanawake na wanaume 331) mwaka 2015; na

(iii) Idadi ya wanafunzi wanaodhaminiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeongezeka kutoka 1,022 (wanawake 534 na wanaume 488) mwaka 2010 hadi 2,658 (wanawake 1,372 na wanaume 1,286) mwaka 2015.

(g) **Kuimarisha Mafunzo ya Ualimu:**

(i) Ujenzi wa Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa, kilichopo Mchangamdogo, Wete Pemba umekamilika. Mafunzo ya ualimu yametolewa katika Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja, Chuo cha Kiislamu Kiuyu na Chuo cha Benjamin William Mkapa huko Pemba;

(ii) Jumla ya walimu 4,031 wamemaliza mafunzo kati yao 238 wamemaliza mafunzo ya ngazi ya Cheti cha Elimu Jumuisho, 951 wamemaliza ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Sekondari, 1,823 wamemaliza ngazi ya stashahada ya Elimu ya Msingi na walimu 1,019 wamemaliza Mafunzo ya Ualimu wa Dini na Kiarabu;

(iii) Chuo Kikuu cha SUZA kimeanzisha Diploma ya Sayansi ya Ualimu yenye wanafunzi 102 na Diploma ya Uongozi yenye wanafunzi 100. Aidha, hatua za awali za kutayarisha mtaala wa ualimu Cheti ngazi ya Maandalizi zimeanza;

(iv) Kitivo cha Tiba *(Faculty of Medicine)* kimeanzishwa na sasa wanafunzi 66 wa mwaka wa kwanza na wa pili wanendelea na masomo;

(v) Jumla ya walimu 2,481 wamepatiwa mafunzo ya ualimu kwa njia ya Elimu Masafa kwa kupitia Vituo vya Walimu (TCs) na kuweza kupandishwa daraja na kukidhi vigezo vya kufundisha ngazi ya Elimu ya Msingi; na

(vi) Mradi maalumu umeanzishwa ili kuendeleza mafunzo ya walimu wa sayansi na hisabati. Programu ya Maendeleo ya Walimu *(Teachers Advancement Programme - TAP)* imeanzishwa na kufanikiwa kutoa mafunzo kwa walimu Unguja na Pemba. Pia vituo vya ualimu vya Dunga na Kiembesamaki vimepatiwa kompyuta kwa ajili ya kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu kupitia mradi huu.

(h) **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali:**

(i) Ujenzi wa Vituo vya Elimu ya Amali vya Mkokotoni-Unguja na Vitongoji-Pemba umekamilika. Mafunzo ya Amali yametolewa katika Kituo cha Mkokotoni na Mwanakwerekwe-Unguja na Vitongoji-Pemba. Jumla ya wanafunzi 3,130 (936 wanawake na 2,194 wanaume) wamepatiwa mafunzo ya Elimu ya Amali katika vyuo hivyo;

(ii) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, ambayo hutoa mafunzo ya fani mbalimbali za ufundi imeimarishwa. Ukarabati wa miundombinu ya maji na umeme pamoja na karakana ya uhunzi umefanyika. Idadi ya wanafunzi katika Taasisi hiyo imeongezeka kutoka 237 (wanawake 55 na wanaume 182) mwaka 2010 hadi 1,308 (wanawake 250 na wanaume 1,058) mwaka 2015; na

(iii) Ujenzi wa madarasa manne (4) katika Skuli ya Ufundi ya Kengeja-Pemba umekamilika na kupatiwa huduma ya umeme na vifaa vya kisasa vya kufundishia pamoja na karakana.

100. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), SMZ chini ya uongozi wa CCM itaendeleza jitihada za kusimamia ukaguzi ili kuendeleza ubora wa elimu katika ngazi zote pamoja na kutekeleza yafuatayo:-**

(a) **Elimu ya Maandalizi**

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Makuzi na Malezi ya Mtoto na kuongeza kiwango cha uandikishaji kutoka asilimia 31 Mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 50 mwaka 2020;

(ii) Kuwahamasisha wananchi na Sekta Binafsi kuongeza idadi ya madarasa pamoja na kujenga skuli za Maandalizi hususan katika maeneo ya vijijini; na

(iii) Kuimarisha mazingira rafiki ya skuli kwa mtoto kujifunza kwa kutekeleza Programu ya Lishe katika skuli 40 za Maandalizi na kuanzisha vituo 150 vya Tucheze Tujifunze katika Wilaya ya Kaskazini "A" na Kaskazini "B" Unguja na Micheweni na Mkoani-Pemba.

(b) **Elimu ya Msingi**

(i) Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi kutoka asilimia 83.7 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2020;

(ii) Kujenga Skuli za Msingi 10 za ghorofa (Unguja 6 na Pemba 4) katika maeneo yenye upungufu na msongamano mkubwa wa wanafunzi;

(iii) Kuimarisha Programu ya Lishe katika Skuli za Msingi zilizo katika mazingira magumu; na

(iv) Kutekeleza lengo la kutoa elimu bila malipo katika elimu ya msingi kwa kutowachangisha wazee michango yoyote.

(c) **Elimu ya Sekondari**

(i) Kuongeza kiwango cha uandikishaji kutoka asilimia 60 mwaka 2014 hadi asilimia 80 mwaka 2020;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Kibuteni na Donge Unguja; na Mkanyageni, Pemba. Aidha, mabweni (dakhalia) ya kulala wanafunzi katika skuli zilizo mbali na makaazi ya wananchi hususan Skuli ya Sekondari ya Mtule, Matemwe na Chwaka-Tumbe yatajengwa;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa skuli 20 na ujenzi wa madarasa 500 na kuimarisha Elimu ya Sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wa Sekondari; na

(iv) Kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (**TEHAMA)** na ufundishaji wa somo la kompyuta katika Skuli zote za Sekondari sambamba na kuzipatia idadi ya kompyuta za kutosha.

(d) **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali**

(i) Kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na kujenga Kituo cha Mafunzo ya Amali huko Makunduchi Unguja na Daya Mtambwe-Pemba;

(ii) Kuviimarisha vituo vya Mafunzo ya Amali kwa kuvipatia vifaa vya kisasa ili viweze kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo na nadharia ikiwa pamoja na kuimarisha mitaala ya mafunzo kwa kuanzisha fani zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira ili kuwawezesha vijana wengi zaidi kujiajiri hususan Sekta ya Utalii, Uvuvi na Kilimo; na

(iii) Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la madarasa katika Taasisi ya Sayansi ya Karume ili kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na Taasisi hiyo na kupatiwa stadi mbalimbali za maisha.

(e) **Mafunzo ya Ualimu**

(i) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ualimu kazini na vyuoni kwa ngazi ya Cheti na Diploma kwa walimu 5,000 ifikapo mwaka 2020;

(ii) Kuviimarisha Vituo vya Walimu (TCs) vilivyopo sasa kwa kuvipatia vifaa vya kujifunzia, kufundishia na TEHAMA; na kuendeleza mashirikiano kati ya vituo hivyo na taasisi mbalimbali zinazotoa mafunzo ya ualimu; na

(iii) Kutoa motisha kwa walimu wanaofanya kazi, kuhamasisha walimu kujiendeleza kielimu kwa kuwapatia ruzuku za masomo na kuwapandisha daraja kazini.

(f) **Elimu ya Juu**

(i) Kuanzisha Awamu ya Pili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa **(SUZA)**; kujenga Chuo Kikuu kipya katika eneo la Dole; na kuimarisha mashirikiano na Vyuo Vikuu mbali mbali vya ndani na nje ya nchi na kutoa fursa za masomo ya Elimu ya Juu nje ya Zanzibar;

(ii) Kuongeza nafasi za masomo katika Elimu ya Juu na kuimarisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo ili kuongeza idadi ya wanafunzi watakaonufaika kutoka 2,658 mwaka 2015 hadi kufikia 22,404 mwaka 2020; na

(iii) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na Elimu ya Juu hususan katika fani za sayansi, ufundi, udaktari na teknolojia.

(g) **Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima**

(i) Kuendeleza jitihada za kuhamasisha vijana kujiunga na madarasa ya Elimu Mbadala ili kuwawezesha kujiajiri; na

(ii) Kuimarisha utoaji wa Elimu Endelevu kwa watu wazima na kuongeza idadi ya watu wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu kutoka asilimia 85.7 na kufikia asilimia 90 mwaka 2020.

(h) **Elimu Mjumuisho**

(i) Kukamilisha Sera ya Elimu Mjumuisho na kuimarisha miundombinu na mazingira ya skuli ili kukidhi mahitaji ya utoaji wa Elimu Mjumuisho na stadi za maisha; na

(ii) Kuimarisha uwezo wa walimu wa Elimu Mjumuisho kwa kuwapatia mafunzo jumla ya walimu 500 na kuandaa Kamusi ya Lugha ya Alama.

(i) **Michezo na Utamaduni katika Skuli**

Kufufua na kuendeleza Michezo na Utamaduni kwa wanafunzi wa skuli za Msingi na Sekondari na kuanzisha somo la michezo katika Skuli teule sita za Sekondari nne (4) Unguja na Pemba mbili (2).

(j) **Uhifadhi wa Kumbukumbu za Kihistoria na Mambo ya Kale**

(i) Kuendeleza utekelezaji wa Mpango wa Uhifadhi wa Mambo ya Kale na kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kale pamoja na vituo vya kuhifadhia kumbukumbu katika kila Mkoa; na

(ii) Kusimamia uendeshaji, utunzaji na matengenezo ya Makumbusho ya Mnazi Mmoja, Beit-Ajab, Kasri ya Forodhani, Jengo la Kale la Mtoni pamoja na kuendeleza ukusanyaji wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali na kuzihifadhi katika mfumo wa komputa.

(k) **Nyumba za Walimu**

Kujenga jumla ya nyumba 40 za Walimu, Unguja (24) na Pemba (16) na kukamilisha nyumba zote ambazo ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

(l) **Huduma za Maktaba**

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maktaba ya Zanzibar na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba Kuu Pemba, kuanzisha Maktaba za Jamii katika maeneo wanayoishi pamoja na kuendeleza uhamasishaji wa wananchi kupenda kutumia maktaba; na

(ii) Kuendeleza mafunzo ya Ukutubi na kuongeza idadi ya vitabu katika maktaba zote.

**Afya**

101. Kwa kutambua umuhimu wa afya kwa wananchi, CCM imeendelea kusimamia Utekelezaji wa lengo la kufikisha huduma za afya karibu na wananchi wote mijini na vijijini. Huduma za afya zinapatikana katika kila sehemu isiyozidi kilomiti 5 Unguja na Pemba. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Afya imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) **Utekelezaji wa Sera ya Afya:**

Sera ya Afya ya mwaka 1999 imefanyiwa mapitio na Sera mpya ya mwaka 2011 imeandaliwa na kuanza kutumika. Aidha, Sheria ya Afya ya Jamii na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepitishwa. Chini ya sheria hii, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeimarishwa na kupewa nguvu za kisheria.

(b) **Kuimarisha Huduma za Hospitali Kuu ya Mnazimmoja:**

Ili kufikia lengo la kuifanya Hospitali Kuu ya Mnazimmoja kuwa Hospitali ya Rufaa, hatua mbalimbali za kuimarisha huduma katika Hospitali hiyo zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Idadi ya madaktari (MD) imeongezeka hadi kufikia 82 wakiwemo madaktari bingwa sita. Mashine ya uchunguzi wa moyo *(ECG na Echocardiography)*

imenunuliwa na daktari bingwa mzalendo wa maradhi ya moyo amepatikana;

(ii) Kwa mashirikiano na taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Upasuaji wa Ubongo (*Neurosurgical Education and Development)* ya Spain, jengo jipya la Kitengo cha Upasuaji wa Uti wa Mgongo (*Neorosurgical Unit)* limejengwa pamoja na ununuzi wa vifaa vipya vya upasuaji wa mgongo na vichwa maji. Aidha, tiba kwa njia ya mawasiliano ya mtandao *(telemedicine)* imeanzishwa;

(iii) Idara zote muhimu za maabara *(microbiology, parasitology, aematology, biochemistry, histopathology and blood trasfusion)* zimefanyiwa matengenezo makubwa na kufikia kiwango cha utendaji kinacholingana na maabara nyingine za Afrika Mashariki. Jumla ya vipimo 67 vinafanyika ikilinganishwa na vipimo 30 vya hapo awali;

(iv) Huduma ya uchunguzi wa maradhi ya Kifua Kikuu kwa kutumia mashine ya kisasa *(Gene expert)* yenye uwezo mkubwa wa kugundua vimelea vya maradhi hayo kwa haraka zimeanza kutolewa;

(v) Sehemu ya matibabu ya meno na macho zimeimarishwa na kuweka vifaa vipya vya matibabu;

(vi) Ukarabati mkubwa umefanyika katika Kitengo cha Wagonjwa Mahututi (ICU), Chumba cha Upasuaji *(theatre)* na Wodi ya Wazazi pamoja na kuwekewa vifaa vya kisasa; na

(vii) Ujenzi wa ghala jipya la kuhifadhia dawa (Bohari Kuu ya Dawa) huko Maruhubi na Kituo cha Damu Salama huko Sebleni umekamilika.

(c) **Hospitali ya Kivunge:**

Jumla ya nyumba 12 za wafanyakazi zimejengwa, Chumba cha Upasuaji, Wodi za Watoto na Sehemu ya Wagonjwa wa Nje (OPD) zimejengwa. Aidha, mashine za upasuaji na mashine ya

mionzi *(Utra Sound)* zimenunuliwa na Kitengo cha Huduma za Dharura kimeanzishwa.

(d) **Hospitali ya Wete:**

Ili kuipandisha hadhi Hospitali ya Wete kuwa Hospitali ya Mkoa, maabara mpya, wodi ya akina mama na sehemu ya kuhifadhia maiti zimejengwa. Aidha, wodi ya wanaume, kliniki ya watoto, vyoo na ghala ya kuhifadhia dawa zimefanyiwa ukarabati mkubwa na mashine ya mionzi *(Utra Sound)* pamoja na mashine ya kupimia moyo zimenunuliwa.

(e) **Hospitali ya Mkoani:**

Ili kuipandisha daraja Hospitali ya Abdalla Mzee-Mkoani na kuwa Hospitali ya Mkoa, mpango wa kuijenga upya hospitali hiyo umeandaliwa. Katika kutekeleza mpango huo, malipo ya fidia kwa wananchi wote waliyobomolewa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa majengo mapya tayari yamefanyika na kazi ya ujenzi wa hospitali hiyo unaendelea.

(f) **Hospitali ya Micheweni:**

Kazi ya utanuzi na matengenezo ya majengo ikiwemo Wodi ya Wazazi, Chumba cha Upasuaji na Chumba cha Maabara mpya ya kisasa umekamilika. Aidha, ujenzi wa Chumba cha Upasuaji unaendelea.

(g) **Kuimarisha Huduma za Kinga na Tiba:**

(i) Uwiano wa daktari kwa kutoa huduma kwa wananchi sasa umefikia daktari mmoja anahudumia watu 9,093 (1:9093) badala ya watu 31,836 (1:31,836);

(ii) Jumla ya madaktari wazalendo 37 wameajiriwa. Idadi ya madaktari na wataalamu wa afya imeongezeka kutoka 3,634 mwaka 2010 hadi 4,618 mwaka 2014. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 26;

(iii) Elimu ya Afya kwa Umma imeendelea kutolewa kwa njia mbalimbali. Mkazo mkubwa umewekwa katika kuelimisha wananchi kuhusu maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Jitihada maalumu zimechukuliwa

juu ya kinga na tahadhari kuhusu maradhi ya EBOLA; na

(iv) Jumla ya wafanyakazi 142 wa kada mbali mbali wamepelekwa masomoni ndani na nje ya nchi wakiwemo Madaktari 9, Wasaidizi Madaktari 12, Wauguzi 96 na wengiene wasiokuwa wa kada za afya.

(h) **Mapambano dhidi ya Malaria:**

(i) Ili kuendeleza mapambano dhidi ya malaria, mradi wa "Maliza Malaria Zanzibar" umeendelea kutekelezwa. Kupitia mradi huo, nyumba 57,385 sawa na asilimia 96 ya lengo lililowekwa zilipulizwa dawa ya kuua mbu wa malaria. Zoezi hilo limefanyika katika Wilaya zote za Unguja na Pemba;

(ii) Vyandarua 717,000 viligawiwa kwa wananchi (vitatu kwa kila kaya) na vingine 30,474 vilisambazwa kwa kupitia katika vituo vinavyotoa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto Unguja na Pemba; na

(iii) Jumla ya wagonjwa 28,982 (7,618 wakiwa chini ya umri wa miaka 5 na 21,364 wakiwa zaidi ya miaka 5) walichunguzwa katika vituo mbalimbali vya afya na asilimia 1.4 waligundulika kuwa na vimelea vya malaria na kutibiwa. Jitihada hizo zimewezesha kiwango cha ugonjwa wa malaria kuendelea kushuka kutoka asilimia 0.06 mwaka 2010 hadi asilimia 0.03 mwaka 2014.

(i) **Mapambano dhidi ya UKIMWI:**

(i) Jitihada za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kupima afya zao na kupiga vita unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) zimeendelezwa. Ili kuendeleza jitihada hizo, jumla ya shilingi 51,471,765 zimetolewa kwa Jumuiya ya Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (ZAPHA+);

(ii) Wahudumu wa afya 150 na waelimishaji rika 40 wamepatiwa mafunzo ya kuelimisha jamii mbinu za kujikinga na UKIMWI, kupiga vita unyanyapaa na udhalilishaji wa kijinsia. Jumla ya wananchi 3,881

kutoka katika Shehia 118 za Unguja na Pemba wamefikiwa na kupatiwa elimu hiyo. Vile vile vijana 300 wamepatiwa mafunzo ya Stadi za Maisha;

(iii) Jumla ya wananchi 61,921 wamejitokeza kupima afya zao (wanawake 32,477 na wanaume 29,444). Kati yao 966, sawa na asilimia 1.56 waligundulika kuwa wanaishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) wanawake 520 (asilimia 54) na wanaume 446 (asilimia 46);

(iv) Idadi ya wagonjwa wanaopata huduma ya dawa za ARVs, imeongezeka kutoka 2,341 mwaka 2010 hadi 4,669 mwaka 2014 sawa na asilimia 99;

(v) Huduma za tiba na kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto zimetekelezwa. Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU imeongezeka kutoka 87 mwaka 2012, hadi 91 mwaka 2014; na

(vi) Matokeo ya jitihada hizo, kiwango cha maambukizi ya VVU bado kimeendelea kuwa asilimia 0.6.

(j) **Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma:**

(i) Ili kudhibiti ugonjwa wa Kifua Kikuu na Ukoma, matibabu ya maradhi hayo kwa wananchi yameendelea kutolewa na kampeni maalumu ya ulishaji dawa kwa jamii imeendelea kutekelezwa. Vijiji 24 vya Unguja na Pemba vimefikiwa kwa njia ya mikutano na wananchi 314 waligunduliwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kati yao 223 (asilimia 71) wanapatiwa dawa wakiwa nyumbani kwao na chini ya uangalizi wa familia zao; na

(ii) Jumla ya wananchi 97 waligundulika kuwa na maradhi ya Ukoma kati yao sita (6) wakiwa na ulemavu wa daraja la pili. Hatua ya kuwapatia mafunzo juu ya ugonjwa wa Ukoma wananchi 169 ambao ni jamaa za wagonjwa hao imetekelezwa.

(k) **Huduma za Afya ya Mama na Mtoto:**

(i) Jumla ya Vituo vya Afya 84 vinatoa huduma za ziada ikiwemo kuzalisha, maabara na huduma za meno. Huduma ya Afya ya Uzazi (kwa njia ya kawaida au upasuaji) na Afya ya Mama na Mtoto hutolewa bila ya malipo katika hospitali zote na Vituo vya Afya. Vituo vyote hivyo vinafaidika na upatikanaji wa dawa chini ya mpango maalumu (Zanzibar Integrated Logistic System); na

(ii) Juhudi za kuwapatia watoto chanjo zimeendelea kutekelezwa ili kupunguza idadi ya vifo vya watoto ambapo asilimia 96.75 ya watoto wote wenye umri chini ya miaka 15 wamepatiwa chanjo hizo. Chanjo ya BCG imefikia asilimia 148, Polio 95, Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda na Uti wa mgongo asilimia 101 na Surua asimilia 77.

(l) **Kuendeleza Huduma ya Tiba Asili**

Baraza la Tiba Asili limeanzishwa na waganga 193 wamesajiliwa. Jumla ya maduka ya dawa za asili 39, kliniki za tiba asili na tiba mbadala 18 zimeanzishwa na wasaidizi waganga 125 wamesajiliwa.

(m) **Chuo cha Sayansi ya Afya:**

(i) Jumla ya wanafunzi 821 wa taaluma mbalimbali za afya wamehitimu mafunzo. Aidha, kwa kushirikiana na Chuo cha MATANZAS cha Cuba, wanafunzi 38 (19 wanaume na 19 wanawake) wa kada ya udaktari wamehitimu na kuongeza idadi ya madaktari wazalendo wanaotoa huduma katika hospitali za Unguja na Pemba. Aidha, masomo ya kujiendeleza kwa wafanyakazi wenye cheti kwa muda mrefu na ambao hawakupata fursa ya kujiendeleza kielimu katika fani zao yameanzishwa; na

(ii) Jumla ya wanafunzi 183 wamejiunga na mafunzo hayo kwa mwaka 2013/2014 na wanafunzi 11 wanaendelea na mafunzo ya Elimu Masafa kupitia AMREF.

102. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza SMZ kuiendeleza zaidi Sekta ya Afya kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuendeleza ushirikishwaji wa wananchi na Sekta Binafsi ili kuchangia maendeleo ya afya kwa kuzingatia MKUZA na Dira ya 2020;

(b) Kuendelea kuifanya Hospitali ya Mnazimoja kuwa ya Rufaa kwa kuongeza huduma za matibabu ya saratani na kuimarisha huduma za uchunguzi na ununuzi wa vifaa kama *"Magnetic Resonance Imaging"* (MRI), DNA na kuongeza idadi ya madaktari bingwa wa fani mbalimbali;

(c) Kujenga Hospitali ya kisasa ya Rufaa katika eneo la Binguni Unguja, kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee na kuimarisha Hospitali ya Wete-Pemba ili zifikie daraja na kiwango cha Hospitali za Mkoa. Aidha, Hospitali za Vijiji *(Cottage Hospitals*) za Micheweni na Vitongoji (Pemba) na Makunduchi na Kivunge (Unguja) zitaendelea kuimarishwa ili zifikie daraja na kiwango cha Hospitali za Wilaya;

(d) Kuendeleza jitihada za kuimarisha Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto kwa kujenga majengo mapya ya Wodi ya Wazazi na Wodi ya Watoto katika Hospitali Kuu ya Mnazimoja pamoja na kuvifanyia ukarabati vituo 19 vya Afya ya Msingi na kuvipatia vifaa vya kisasa Unguja na Pemba ili kupunguza kiwango cha vifo vya mama na mtoto;

(e) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma na maradhi mengine ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza pamoja na kuimarisha jitihada za utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi ili kupunguza ongezeko la maradhi ya Saratani, Kisukari na Shinikizo la Damu;

(f) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya na watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi wakiwemo madaktari wa fani ya Udaktari Bingwa katika fani ya maradhi ya wanawake, mifupa, watoto, maradhi ya moyo na usingizi;

(g) Kuendelea kutambua umuhimu wa tiba asili na tiba mbadala katika jamii na kuimarisha ushirikiano na Baraza la Tiba Asili katika utendaji wake wa kazi;

(h) Kuhamasisha upatikanaji wa chakula na lishe bora katika kila kaya ili kupunguza utapiamlo mkali kwa watoto kutoka asilimia 24 mwaka 2014 hadi asilimia 12 mwaka 2020;

(i) Kuendeleza tafiti mbalimbali katika maeneo ya Afya ya Mama na Mtoto, maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza pamoja na mifumo ya utoaji wa huduma za afya;

(j) Kuimarisha huduma za matibabu kwa wagonjwa walioathirika na madawa ya kulevya na afya ya akili na kujenga kituo maalumu kwa waathirika wa madawa ya kulevya;

(k) Kuimarisha upatikanaji, ugawaji, usambazaji na udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi *(Reagents)* vyenye ubora na usalama katika ngazi zote;

(l) Kuandaa Sheria ya Uanzishaji wa Mfuko wa Bima ya Afya na kusimamia utekelezaji wa mfuko huo; na

(m) Kuimarisha na kusimamia mfumo wa taarifa za Afya ili ziweze kutumika katika kutoa maamuzi katika ngazi zote.

**Maji**

103. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ chini ya uongozi wa CCM imeimarisha huduma za usambazaji na ugawaji wa maji safi na salama kwa wananchi ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Mradi wa maji Mkoa wa Mjini Magharibi, Awamu ya Pili umetekelezwa. Ujenzi wa matangi makubwa mawili huko Kinuni na Dole na uchimbaji wa visima vitano (Kizimbani (3) na Msikiti Mzuri (2) pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 21 umekamilika. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kimefikia asilimia 87.7;

(b) Katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, kazi ya ujenzi wa matangi ya maji Matemwe (lita 3,000,000) na Nungwi (lita 3,000,000)

pamoja na ulazaji wa mabomba kwenye maeneo yote ya mradi imekamilika. Kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika mkoa huo kimefikia asilimia 71.68;

(c) Kwa Mkoa wa Kusini Unguja, kazi ya ujenzi wa matangi ya maji ya Machui (lita 1,500,000) na Tunguu (lita 1,200,000) pamoja na ulazaji wa mabomba kwenye maeneo ya mradi imekamilika. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mkoa huo kimefika asilimia 76.45;

(d) Kazi ya ujenzi wa matangi ya maji ya Ndagoni (lita 1,000,000), Vikunguni (lita 300,000), Vitongoji-Ali Khamis Camp (lita 300,000), Kambini Bahanasa (lita 1,000,000) na Wambaa (lita 500,000) pamoja na ulazaji wa mabomba katika maeneo yote ya miradi ya Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba imekamilika. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kimefikia asilimia 56.42 na Mkoa wa Kusini Pemba asilimia 74.08; na

(e) Jumla ya mita 3,007 zimefungwa katika nyumba za makazi na maeneo ya biashara Unguja na Pemba ili kupunguza kiwango cha upotevu wa maji.

104. **Ili kuendeleza sekta ya maji na kuimarisha huduma za usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kufanikisha yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kuimarisha usambazaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 87 mwaka 2015 hadi asilimia 97 mwaka 2020 kwa Mijini na kutoka asilimia 70 mwaka 2015 hadi asilimia 85 kwa vijijini;

(b) Kuendeleza utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa miundombinu ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi na ufungaji wa mita kwa wateja ili kudhibiti upotevu wa maji;

(c) Kuendeleza jitihada za kuhuisha miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji, kuhifadhi, kutunza na kulinda vyanzo vya maji pamoja na maeneo ya hifadhi ya maji; na

(d) Kuendelea kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi, utumiaji na uchangiaji wa huduma ya maji safi na salama na kufanya utafiti wa matumizi ya Nishati ya Jua katika visima na vyanzo vya maji.

**Makazi**

105. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM imefanya juhudi kubwa za kuendeleza ujenzi wa nyumba bora kwa ajili ya makazi ya wananchi Unguja na Pemba. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), huduma za makazi zimeboreshwa na kupatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Nyumba, Sheria ya kuanzisha Shirika la Nyumba la Zanzibar ya mwaka 2014 imepitishwa ili kuwapa fursa wananchi waliopangishwa nyumba za maendeleo mijini na vijijini kuuziwa sehemu ya majengo hayo;

(b) Kazi ya kuufanyia mapitio Mpango Kabambe (Master Plan) wa mji wa Zanzibar ili kuanzisha maeneo maalumu ya ujenzi wa nyumba za ghorofa hususan katika maeneo ya mijini na kuwashajihisha wawekezaji kuwekeza katika Sekta ya Nyumba imefikia katika hatua za mwisho; na

(c) Ujenzi wa Nyumba ya Maendeleo huko Bambi (Mpapa) umekamilika. Jumla ya nyumba (fleti) 24 zimekabidhiwa kwa wananchi wakati wa maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

106. **Ili kuendelea kuwawezesha wananchi kupata nyumba na makazi bora, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), itahakikisha kuwa SMZ inasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba na Sheria "Condominium" pamoja na**

**kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha miradi ya makazi kwa njia ya ubia (PPP).**

**Mamlaka ya Mji Mkongwe**

107. Katika kuendeleza Mji Mkongwe, Mamlaka imefanya ukaguzi wa kitaalamu ili kubaini nyumba zilizo katika hali mbaya ya uchakavu na kuziingiza katika kanzidata *(database)* pamoja na kuwashauri wamiliki au wapangaji wa nyumba hizo kuzifanyia ukarabati unaohitajika ambapo majengo 267 yamefanyiwa ukarabati bila kubadili uhalisia wake.

108. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa, SMZ inaendelea kuchukua hatua za uhifadhi wa Mji Mkongwe ili uendelee kuwa kivutio cha utalii na chanzo cha ajira kwa wananchi kwa kutekeleza yafuatayo:-**
    (a) Kuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar ili uendelee kubaki katika uasili wake na katika orodha ya Miji ya Urithi wa Dunia;
    (b) Kuendelea kuyahifadhi na kuyafanyia ukarabati majengo yote ya kihistoria ndani ya eneo la Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;
    (c) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu na thamani ya kuulinda, kuuhifadhi na kuendeleza Mji Mkongwe kwa maslahi ya kizazi cha sasa na cha baadaye; na
    (d) Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa ukuta wa ukingo wa bahari katika eneo la Mizingani.

**Maeneo mengine ya kipaumbele**

**Utamaduni na Michezo**

109. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Utamaduni na Michezo imepata mafanikio makubwa.

**Michezo**

110. Michezo ni nyenzo muhimu katika kulinda na kudumisha mila na silka njema za jamii. Michezo huimarisha afya na kujenga udugu na

mashirikiano miongoni mwa wananchi na Mataifa mbalimbali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Mabaraza ya Michezo ya Wilaya yameimarishwa na kupatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa shughuli za michezo;
(b) Timu ya Taifa na vilabu mbalimbali vimepata fursa ya kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa;
(c) Timu ya vijana wenye ulemavu wa akili imeshiriki katika mashindano ya olimpiki *(Special Olympics)* yaliyofanyika nchini Ugiriki;
(d) Uwanja wa Amani umewekewa nyasi bandia. Aidha, studio ya kisasa ya kurekodia filamu/muziki imeanzishwa huko Rahaleo na pia Kituo cha Michezo huko Dole (Dole Academy) kimejengwa ambapo zaidi ya vijana 3,000 wameanza kukitumia na kupata fursa ya kushiriki katika mashindano ya ndani na nje ya nchi; na
(e) Uwanja wa mpira wa Gombani Pemba nao umeimarishwa kwa kuwekewa taa, kujengwa paa jipya, njia ya kukimbilia *(running track)* pamoja na kiwanja cha michezo ya ndani.

111. **Ili kuiendeleza Sekta ya Michezo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo kwa lengo la kuimarisha afya zao na kuendeleza Michezo ya Asili hususan mchezo wa Ng'ombe na mashindano ya resi za ngalawa na kutumia sanaa za aina mbalimbali ili kujiajiri wao wenyewe kwa lengo la kupambana na umasikini;
(b) Kukiimarisha Kituo cha Michezo cha Dole *(Dole Academy)* ili kuendeleza michezo ya aina mbalimbali kwa vijana na kuanzisha mfumo wa michezo ya kulipwa na kushiriki mashindano ya Kimataifa;
(c) Kujenga viwanja vya michezo katika Wilaya tano (5) na kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa vijana ili kuwaongezea ujuzi na uzoefu wa michezo kwa kutumia walimu wa ndani na nje ya nchi;

(d) Kukifanyia matengennezo makubwa kiwanja cha michezo cha "Mao Tse Tung" ili kiweze kutumika kwa shughuli za michezo na sherehe za kitaifa; na

(e) Kuvipatia vyama vya michezo vya watu wenye ulemavu fursa stahiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuendeleza michezo ikiwemo michezo ya kulipwa.

**Utamaduni**

112. Utamaduni ni nyenzo muhimu katika kulinda na kudumisha mila na silka njema za jamii. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), yamepatikana mafanikio yafuatayo:-

(a) Sera na Sheria zinazoongoza Utamaduni zimefanyiwa mapitio ili kukidhi matarajio na mahitaji ya wakati na sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni imetungwa. Chini ya sheria hiyo, Bodi ya Sensa ya Filamu na Baraza la Sanaa la Zanzibar vimeunganishwa;

(b) Utafiti wa Urithi wa Utamaduni usioshikika umefanyika na matokeo ya utafiti huo kuhifadhiwa Kimataifa na kuingizwa katika orodha ya UNESCO ya tamaduni zinazohifadhiwa. Sambamba na hatua hiyo, matokeo ya utafiti huo pia yamerejeshwa kwa wananchi wa maeneo husika ili kuzitumia kama sehemu ya ajira na kupambana na umasikini; na

(c) Hatua ya ukaguzi wa kazi za sanaa ili kulinda na kuhifadhi mila, desturi na silka za Mzanzibari imetekelezwa. Aidha, Kamusi za lahaja za Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu zimechapishwa na kusambazwa kwa wananchi.

113. **Ili kuendeleza Sekta ya Utamaduni, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kutekeleza mambo yafuatayo:-**

(a) Kuandaa Sera ya Urithi wa Utamaduni na kufanya utafiti maalumu katika visiwa visivyoishi watu ili kubaini aina ya utalii unaoweza kufanyika na kuongeza fursa za ajira kwa wananchi;

(b) Kuimarisha lugha ya Kiswahili na kuzifanya lahaja za Kiswahili za Zanzibar kuwa chimbuko la Kiswahili fasaha. Jumla ya machapisho mapya 10 ya vitabu na majarida 15 ya kuimarisha lugha ya Kiswahili yatatolewa kwa lengo la kuwawezesha watumiaji wenyeji na wageni kukitumia Kiswahili fasaha katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii;

(c) Kuihamasisha jamii ili kuuenzi, kuulinda na kuudumisha utamaduni wa Mzanzibari na kushiriki katika uandaaji wa matamasha 50 ya utamaduni;

(d) Kuwapatia mafunzo walimu 150 wa utamaduni na wasanii 500 ili kuwawezesha kutumia sanaa zao kwa mambo yenye manufaa kwa wananchi na yenye kuzingatia maadili ya jamii; na

(e) Kuendeleza teknolojia za jadi kwa kutoa mafunzo kwa mafundi 75 ili ziweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi na kuirithisha teknolojia hiyo kwa kizazi kipya.

**Vyombo vya Habari**

114. Vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kutoa habari, kuburudisha na kuelimisha jamii juu ya matukio na masuala mbalimbali yanayojiri ndani na nje ya nchi na kuchangia katika kukuza na kuimarisha demokrasia na utawala bora. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Habari imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Mageuzi makubwa ya kisera na kisheria yamefanyika ili kuiwezesha Zanzibar kuachana na mfumo wa matangazo ya Analogia na kuingia katika mfumo wa Dijitali. Aidha, Shirika la Habari la Zanzibar (ZBC) limeanzishwa ambapo Redio, Televisheni na Gazeti la Serikali (Zanzibar Leo) vimeunganishwa. Hatua hizi zimeongeza ubora wa matangazo na ufanisi katika vyombo vya habari;

(b) Studio za Televisheni (Unguja na Pemba) zimepatiwa vifaa na mitambo ya kisasa ya kurushia matangazo. Waandishi wa habari 114 (wanawake 78 na wanaume 36) wamepatiwa

mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (PhD), Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Astashahada;

(c) Jumla ya vituo vipya tisa (9) vya Radio za FM na Televisheni sita (6) vimeanzishwa;

(d) Chuo cha Uandishi wa Habari kimepatiwa jengo jipya huko Kilimani pamoja na vifaa vya kisasa, walimu wenye ujunzi na kuanzisha mafunzo ya lugha ya Kichina. Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Chuo hiki imeongezeka kutoka 75 mwaka 2010 hadi 180 mwaka 2014; na

(e) Kiwanda cha Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kimehamishwa kutoka eneo la zamani la Saateni na kupelekwa katika majengo mapya huko Maruhubi. Aidha, kiwanda kimepatiwa mitambo mipya na ya kisasa ya uchapaji *(Digital Printing Machine)* na kuanza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

115. **Kwa kutambua uzito wa jukumu la Vyombo vya Habari, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), SMZ chini ya uongozi wa CCM itahakikisha kuwa Uhuru wa Vyombo vya Habari unaendelea kuimarishwa na vyombo hivyo vinatekeleza wajibu wake kwa weledi na kuzingatia maadili ya kazi zao kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kuendeleza mageuzi katika Sekta ya Habari ili kuongeza ufanisi na weledi katika tasnia hii;

(b) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) kwa kulipatia mitambo, vifaa vya kisasa na vitendea kazi pamoja na fursa za mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wafanyakazi 600 wa kada mbalimbali;

(c) Kuendeleza jitihada za kukiimarisha Chuo cha Uandishi wa Habari ili kiwe chachu ya kuendeleza tasnia ya habari na chimbuko la kuibua na kuendeleza vipaji vya uandishi; na

(d) Kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa Kiwanda cha Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukiongezea mitambo na vifaa vya kisasa na wataalamu.

**Huduma za Uokoaji**

116. Huduma za Uokoaji ni muhimu kwa jamii hasa pale yanapozuka maafa na majanga mbalimbali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015) mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Sera ya Maafa ya mwaka 2011 imeandaliwa na Mpango wa elimu ya kukabiliana na Maafa kwa wananchi umetekelezwa;

(ii) Kamati ya Maafa ya Zanzibar, Wilaya na Shehia 277 zimeendelea kuimarishwa na kupatiwa mafunzo ya msingi ya kukabiliana na maafa; na

(iii) Kikosi Maalumu cha Uzamiaji kimeanzishwa na wananchi wamehamasishwa kuanzisha Vikosi na Jumuiya za Uokozi katika maeneo yao.

117. **Ili kuimarisha Huduma za Uokoaji, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa SMZ inatekeleza yafuatayo:-**

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kukabiliana na Maafa na kuanzisha Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa;

(b) Kuanzisha na kusimamia Mfuko wa Kukabiliana na Maafa pamoja na kuimarisha juhudi za kuelimisha jamii katika kukabiliana nayo; na

(c) Kurahisisha uratibu na upatikanaji wa rasilimali fedha na mawasiliano ya moja kwa moja na asasi nyingine za ndani na nje ya nchi katika shughuli za uokoaji.

**Madawa ya Kulevya**

118. Madawa ya kulevya ni moja ya changamoto kubwa zinazowakabili wananchi wengi hasa vijana. Madawa ya kulevya yameathiri sana afya za watumiaji na kudhoofisha nguvu kazi na uchumi wa Taifa letu. Aidha, utafiti umethibitisha kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya madawa ya kulevya na maambukizi ya virusi vya ukimwi (VVU). Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mapambano dhidi ya madawa ya kulevya yameendelezwa na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Mpango maalumu wa utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya *(Road Map)* umeandaliwa;

(b) Hali ya usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume imeimarishwa. Vifaa vya kisasa ikiwemo *"scanner",* Kikosi cha Mbwa pamoja na choo maalumu kwa ajili ya washukiwa wa madawa ya kulevya vimewekwa;

(c) Kwa kushirikiana na taasisi zisizokuwa za kiserikali (NGOs), kazi ya kuhamasisha wananchi kupima afya zao na kuwapitia ushauri nasaha imetekelezwa; na

(d) Jumla nyumba 13 za kurekebisha tabia za vijana walioathirika na madawa ya kulevya *(Sober Houses)* zimeanzishwa na kuhudumia jumla ya vijana 1,020 Unguja na Pemba.

119. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), SMZ chini ya uongozi wa CCM, itaendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Utekelezaji wa Sheria ya Madawa ya Kulevya kwa kuandaa mazingira bora ya utendaji kazi kwa vyombo husika ili kudhibiti uingiaji na usafirishaji wa Dawa za kulevya;

(b) Kuendeleza mafunzo na elimu kwa jamii juu ya athari za madawa ya kulevya na kuandaa mkakati wa kuwasaidia waathirika na madawa hayo ili kuachana na utumiaji. Aidha, kitajengwa kituo maalumu cha kurekebisha vijana walioathirika na madawa ya kulevya;

(c) Kuendeleza na kuimarisha mashirikiano miongoni mwa vyombo vinavyosimamia mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na

(d) Kushirikiana na Taasisi za Kimataifa zinazoendesha mapambano dhidi ya madawa ya kulevya ili kudhibiti usafirishaji na biashara haramu ya madawa hayo bila kujali mipaka ya nchi.

**Demokrasia na Utawala Bora**

120. Demokrasia na Utawala Bora ni moja ya nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Programu maalumu ya elimu ya uraia juu ya Sera ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu imeandaliwa na kutekelezwa;

(b) Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi pamoja na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa imeanzishwa na kuanza kazi. Aidha, Kanuni za kudhibiti Rushwa na Uhujumu wa Uchumi zimeandaliwa na kuanza kutumika;

(c) Mafunzo juu ya mapambano dhidi ya rushwa yametoelewa kwa wafanyakazi na viongozi mbalimbali wa Serikali;

(d) Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi Ndogo ya Wanasheria (Mwera) na nyumba za waendesha Mashtaka wa Mahakama za Wilaya ya Makunduchi na Mkokotoni (Unguja); na Madungu na Chake Chake (Pemba) umekamilika;

(e) Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali lilioko Unguja na lile la Wete Pemba umekamilika. Aidha, mafunzo ya ukaguzi kwa kuzingatia thamani na mazingira yametolewa kwa wafanyakazi. Kutokana na juhudi hizo, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sasa imefikia kiwango kinachokubalika Kimataifa;

(f) Jengo la Mahakama Kuu Unguja na Pemba, majengo ya Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Kadhi yamefanyiwa matengenezo makubwa. Mahakimu wapya 10 wameajiriwa kati yao, saba (7) ni wanawake na watatu (3) ni wanaume;

(g) Mafunzo juu ya matumizi ya Teknolojia ya Habari, uendeshaji na usimamizi wa kesi pamoja na uandishi wa Sheria yametoelewa kwa Majaji, Mahakimu na Waendesha Mashtaka;

(h) Sheria ya kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar imepitishwa na matengenezo ya jengo la Mahakama hiyo

yamekamilika. Aidha, Mahakama ya Watoto imeanzishwa na kuanza kufanya kazi; na

(i) Ujenzi wa jengo jipya la Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi huko Chukwani umekamilika na kuanza kutumika kwa ajili ya mikutano na vikao vyote vya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

121. **Ili kuendeleza Demokrasia na Utawala Bora, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa, SMZ inatekeleza yafuatayo:-**

(a) Utekelezaji wa kazi na majukumu ya Serikali unazingatia misingi ya Demokrasia na Utawala Bora kama ilivyoainishwa katika Katiba za nchi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa wananchi;

(b) Kuandaa na kupitisha Sheria ya Maadili ya Viongozi na kuimarisha mafunzo na elimu ya uraia kwa viongozi wa taasisi za umma na binafsi pamoja na wananchi juu ya misingi ya Demokrasia na Utawala Bora;

(c) Kuimarisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa kuiongezea rasilimali watu, mafunzo na vifaa vya kisasa;

(d) Kuimarisha mfumo wa Sheria kwa kufanya mabadiliko katika utendaji kazi wa Mahakama, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Jeshi la Polisi, Vyuo vya Mafunzo na wadau wengine wa Sheria ili kuwajengea uwezo katika utoaji wa haki;

(e) Kuandaa Sera ya Msaada wa Kisheria ili kutoa fursa kwa wananchi na makundi maalumu ya jamii kupata haki zao kwa urahisi na kuanzisha mfumo wa kitaasisi wa masaada wa kisheria;

(f) Kuimarisha Ofisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali na mifumo ya usajili wa Nyaraka, Biashara, Mali na Hakibunifu na kudhibiti wizi na uharamia wa sanaa; na

(g) Kuimarisha huduma za ukaguzi wa Hesabu za Serikali ili kuhakikisha kwamba miradi inayotekelezwa ina thamani sawa

na fedha zilizotumika. Aidha, mafunzo ya kada mbalimbali yatatolewa kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

**Serikali za Mitaa**

122. Serikali za Mitaa ni chombo muhimu cha kuwashirikisha wananchi katika kusimamia shughuli za utawala na maendeleo yao. Serikali za Mitaa zina mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya wananchi mijini na vijijini na kuendeleza demokrasia na utawala bora. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Sheria za Serikali za Mitaa na Sheria ya Mamlaka ya Mikoa zimefutwa na kutungwa Sheria mpya ya Tawala za Mikoa na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(b) Wananchi wamehamasishwa kuunda Kamati za Maendeleo za Shehia na Majimbo ili kusukuma kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jumla ya Kamati za Maendeleo za Shehia 339 katika majimbo yote Unguja na Pemba zimeanzishwa;

(c) Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya yameendelea kupatiwa ruzuku, vitendea kazi pamoja na watendaji wenye ujuzi. Jumla ya wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali. Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Serikali za Mitaa nao wamepatiwa mafunzo juu ya masuala ya Fedha, Afya na Sheria;

(d) Mradi maalumu wa Huduma za Jamii (ZUSP) umeanzishwa ili kuimarisha mazingira ya Manispaa ya Zanzibar, hifadhi ya eneo la urithi wa Mji Mkongwe na miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani huko Pemba. Mradi huo umekamilisha kazi ya uwekajiwa taa za barabarani pamoja na taa za kuongoza magari zinazotumia umeme wa jua *(solar)* katika maeneo ya Mji Mkongwe; na

(e) Baraza la Manispaa la Zanzibar limeanzisha utaratibu wa kuingia mikataba na vikundi vya kijamii kwa ajili ya kufanya usafi katika maeneo ya masoko, bustani, barabara, mitaro na kuondoa taka ngumu ili kuimarisha usafi wa mazingira ya mji.

123. **Ili kuziendeleza Serikali za Mitaa, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kwamba, SMZ inatekeleza yafuatazo:-**

(a) Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha ubora wa huduma kwa wananchi na usafi wa mazingira ya maeneo ya miji;

(b) Kusimamia, kuratibu na kusaidia utendaji kazi wa Kamati za Maendeleo katika maeneo mbalimbali ili kusukuma kasi ya maendeleo na kudhibiti vitendo viovu katika jamii na kusaidia juhudi za wananchi katika kuimarisha huduma za kijamii na kuwapatia misaada ya aina mbalimbali; na

(c) Kuendeleza utekelezaji wa mradi maalumu wa kuimarisha mazingira ya Manispaa ya Zanzibar, hifadhi ya eneo la urithi wa Mji Mkongwe na miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani Pemba. Aidha, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Wete utakamilishwa.

**Idara Maalumu za SMZ**

124. Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni vyombo muhimu katika utekelezaji wa Sera za CCM kuhusu Ulinzi na Usalama hususan dhana ya ulinzi wa umma ambao unawashirikisha wananchi wote. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ chini ya uongozi wa CCM imeimarisha mazingira ya utendaji kazi na maslahi ya wapiganaji wa Idara Maalumu za SMZ kwa kutelekeza yafuatayo:-

(a) **Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo (KMKM)**
Jumla ya wapiganaji 83 wamepatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali pamoja na kuwapatia vyombo vipya vya usafiri na vifaa vya kisasa. Aidha, ujenzi wa Hospitali ya Kibweni umekamilika na kuanza kutumika.

(b) **Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)**

Jumla ya wapiganaji 86 wamepatiwa mafunzo ya aina mbalimbali. Vijana 2,000 wamepatiwa mafunzo ya uzalendo, uzalishaji mali pamoja na mafunzo ya amali kila mwaka. Aidha, jumla ya vijana 900 wamepatiwa Mafunzo ya Stadi mbalimbali za ufundi katika Chuo cha Amali cha JKU.

(c) **Chuo Cha Mafunzo**
Kazi ya ujenzi wa bweni la kulala wanafunzi huko Kinumoshi imekamilika. Aidha, utaratibu wa wahalifu kutumikia adhabu zao katika jamii badala ya Chuo cha Mafunzo umeanza kutekelezwa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi.

(d) **Kikosi cha Zima Moto na Uokozi (KZU)**
Jumla ya wapiganaji 68 wamepatiwa mafunzo ya zimamoto nje ya nchi. Huduma za Zimamoto na Uokozi zimefikishwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Aidha, huduma za Zimamoto na Uokozi zimeanza kutolewa katika Bandari za Malindi (Unguja) na Mkoani (Pemba).

(e) **Kikosi Cha Valantia Zanzibar (KVZ)**
Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Kikosi hicho huko Mtoni (Unguja) umekamilika na ujenzi wa nyumba ya maafisa na makaazi ya wapiganaji wa Kikosi hicho huko Kisiwani Pemba umeanzishwa.

125. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itaielekeza SMZ kuendelea kuziimarisha Idara Maalum za SMZ kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuimarisha zaidi mazingira ya kazi na utendaji wa wapiganaji wa KMKM, JKU, KZU na KVZ kwa kuwapatia mafunzo, vifaa vya kisasa, maslahi na mahitaji mengine muhimu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya ulinzi kwa weledi na ufanisi mkubwa;

(b) Kukamilisha ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya JKU Mtoni na kukiendeleza Kituo cha Amali cha JKU kwa kupanua wigo wa mafunzo ya Amali kwa vijana wanaojiunga na kituo hicho kwa

kuzingatia mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe; na

(c) Kukamilisha ujenzi wa nyumba za maafisa na makaazi ya wapiganaji wa KVZ Kisiwani Pemba.

**Kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar**

126. Hoja ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar imetokana na Sera ya CCM ya kujenga umoja wa kitaifa, amani na utulivu. Bila ya kuwepo mazingira ya amani na utulivu nchi haiwezi kupata maendeleo na hakuna mwekezaji atakayekubali kuwekeza. Aidha, wananchi watashindwa kuendesha shughuli zao za kiuchumi, kijamii na utamaduni. Katika kipindi cha 2010-2015, Serikali chini ya uongozi wa CCM, imeifanyia mabadiliko Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1985 (Mabadiliko ya 10) na baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa chini ya uongozi wa Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeundwa na kufanikiwa kutimiza malengo yake kwa ufanisi.

127. **Ili kuendeleza Sera ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar, katika kipindi cha 2015-2020, CCM itandelea kuwa muumini wa kweli wa amani, utulivu na kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar kwa kuimarisha mafanikio yaliyokwisha kupatikana na kuielekeza SMZ kutekeleza yafuayo:-**

(a) Kuendeleza jitihada za kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa amani, umoja na mshikamano ili kujenga mazingira ya kuaminiana, kuvumiliana na kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii;

(b) Kuendelea kupiga vita na kudhibiti vitendo vya ubaguzi vinavyojitokeza katika sehemu za utoaji wa huduma za kiuchumi, kisiasa na kijamii miongoni mwa wananchi; na

(c) Kuimarisha mifumo ya taasisi za uratibu na kushughulikia malalamiko na kero za wananchi kwa wakati, haki na uadilifu.

## Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali

### Watoto

128. Watoto kama Taifa la kesho wanayo haki ya kulindwa kwani ndio chanzo cha rasilimali watu na mrithi wa Taifa la kesho. Watoto wanayo haki ya kuishi, kutoa mawazo, kupata lishe bora, malezi na ulinzi, kupewa elimu na kutobaguliwa kwa kwa namna yoyote. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Serikali chini ya uongozi wa CCM imeendelea kusimamia maendeleo ya watoto na mafanikio yafuatayo amepatikana:-

   (a) Sheria ya Mtoto pamoja na Kanuni saba za kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo zimepitishwa ikiwemo miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa nyumba za kulelea watoto. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Kulelea Watoto cha Mazizini umekamilika;

   (b) Jumla ya Mabaraza ya Watoto 239 yameanzishwa Unguja na Pemba ili kupiga vita ajira kwa watoto na kazi ya usajili na kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu imetekelezwa na watoto 12,453 (Unguja 7,711 na Pemba 4,742) wamesajiliwa na kutambuliwa mahitaji yao. Aidha, kampeni maalumu ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto imeanzishwa; na

   (c) Kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru Kariakoo (Unguja) na Tibirinzi (Pemba) vimejengwa upya ili kuwapatia watoto maeneo ya kucheza yenye mandhari nzuri na kuvutia.

129. **Katika kipindi cha miaka 2015-2020, CCM itaendelea kuimarisha haki na maendeleo ya watoto na kuhakikisha kwamba SMZ inatekeleza hatua zifuatazo:-**

   (a) Kusimamia uanzishaji na uendelezaji wa Mabaraza ya Watoto na Kamati za Wazazi katika Shehia, Wilaya na Mikoa yote ya Zanzibar ili kupiga vita vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto;

   (b) Kuendelea kupiga vita ajira za watoto na kusimamia utekelezaji wa Sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu Haki, Usawa na hifadhi ya mtoto; na

(c) Kuratibu na kutathmini huduma inazotolewa na vituo binafsi vya kulelea watoto ili kuhakikisha vinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria.

**Vijana**

130. Vijana walioandaliwa vyema na kujipanga vizuri wanao mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Changamoto kubwa inayowakabili vijana mijini na vijijini ni ukosefu wa ajira, kukosa ujuzi na maarifa ya kisasa pamoja na mitaji hivyo kushindwa kujiendeleza na kutekeleza wajibu wao wa kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa kisasa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ chini ya uongozi wa CCM, imechukua hatua mbalimbali za kuwaendeleza vijana na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Baraza la Taifa la Vijana limeanzishwa na jumla ya asasi za vijana 158 zilipatiwa mafunzo ya aina mbalimbali;

(b) Jumla ya vikundi 258 (Unguja 203 na Pemba 55) vyenye wanachama 2,285 (Unguja 2,015 na Pemba 270) vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali na stadi mbalimbali za maisha. Vile vile, vyama viwili (2) vya SACCOS za vijana vimeanzishwa;

(c) Mfuko Maalumu umeanzishwa ili kutoa mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa Vijana. Mikopo yenye thamani ya Shilingi 813,800,000 (Unguja Shilingi 700,000,000 na Pemba Shilingi 113,800,000) imetolewa;

(d) Kwa kupitia mifuko mingine ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, jumla ya Shilingi 318,600,000 zimetolewa kwa vikundi 130 vya vijana Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo Shilingi 206,950,000 zimetolewa kwa vikundi 99 vya vijana wa Unguja, na Shilingi 111,700,000 zimetolewa kwa vikundi 31 vya vijana wa Pemba;

(e) Jumla ya shilingi milioni 100 zimewekwa katika Benki ya CRDB kama dhamana ya Serikali ili kuiwezesha Benki hiyo kutoa mikopo kwa vijana; na

(f) Jumla ya Vyama vya Ushirika vinne (4) vyenye wanachama 72 (wanawake 42 na wanaume 30) ambao ni vijana waliohitimu

vyuo na vyuo vikuu vimeanzishwa na kuweza kujiajiri wenyewe kupitia kilimo na usindikaji; na kutoa mafunzo na ukaguzi kwenye vikundi vya ushirika. Pia vikundi vitatu (3) vya vijana (Unguja 2 na Pemba 1) vinajishughulisha na kilimo cha mboga mboga kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji (*Drip Irrigation)* vimeanzishwa na kupatiwa msaada wa vifaa vya umwagiliaji maji vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 21,000 kutoka Shirika la Kazi Duniani (ILO).

131. **Katika kipindi cha mwaka 2015-2020, SMZ chini ya uongozi wa CCM, itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto za vijana kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) Kuandaa Programu za Elimu na Malezi Bora kwa Vijana ili kuwawezesha jumla ya vijana 235,817 kupata mafunzo ya stadi mbalimbali za maisha pamoja na kujiajiri;

(b) Kuliendeleza Baraza la Taifa la Vijana ili kuongeza ushiriki wa vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi;

(c) Kuendelea kuimarisha Mfuko Maalumu wa Vijana ili kutoa mikopo kwa vijana wengi zaidi na kujiajiri katika kilimo cha kisasa na kuanzisha *"Green House"* moja katika kila wilaya;

(d) Kuhamasisha vijana 5,000 waliomaliza vyuo na vyuo vikuu kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali na utoaji huduma, kuvipatia mafunzo na mikopo ili waweze kujiajiri. Aidha, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zitahamasishwa kutoa zabuni za kazi na huduma kwa vijana hao; na

(e) Kuandaa mikakati ya malezi bora kwa vijana ili kujenga moyo wa uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao na kuimarisha mahusiano ya vijana ndani na nje ya nchi.

**Wanawake**

132. Chama Cha Mapinduzi kinatambua uwezo na nguvu kubwa ya wanawake katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ chini ya uongozi wa CCM, imechukua hatua mbalimbali za kuwaendeleza wanawake ili kuwajengea uwezo na

uthubutu wa kutumia fursa za kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kisiasa na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Jumla ya vikundi 551 (Unguja 209 na Pemba 362) na SACCOS 53 (Unguja 24 na Pemba 29) za wanawake zimeanzishwa. Aidha, wajasiriamali wanawake 129 wamepatiwa mafunzo juu ya ubora wa bidhaa na masoko;
(b) Kwa kushirikiana na Chuo cha *Barefoot College Tilonia* cha India, kituo cha kuwafundisha wanawake kutengeneza vifaa vya umeme wa jua kimeanzishwa huko Kibokwa Mkoa wa Kaskazini Unguja;
(c) Waratibu 40 na Makatibu watano (5) wa vikundi vya wanawake wamepatiwa mafunzo ya uongozi, umuhimu wa Hati miliki, UKIMWI, Sheria na jinsia. Pia wanawake 98 wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu za kubaini vitendo vya udhalilishaji na kuepukana navyo;
(d) Katika jitihada za kupiga vita udhalilishaji wa wanawake na watoto, Nyumba Salama kwa ajili ya kuwahifadhi na kuwahudumia waathirika wa vitendo hivyo, imeanzishwa. Jumla ya waathirika 26 wa vitendo hivyo wamepatiwa huduma hizo; na
(e) Skuli za Benbella (Unguja) na Utaani (Pemba) zimeteuliwa kuwa Skuli Maalumu za Sayansi kwa Wanawake ili kuwashajiisha wanafunzi wa kike kupenda masomo ya Sayansi na Hisabati.

133. **Ili kuendeleza juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi kijamii na kisiasa, CCM katika kipindi cha (2015-2020), itahakikisha kwamba SMZ inatekeleza yafuatazo:-**

(a) Kuendelea kusimamia upatikanaji wa Haki za Wanawake na kupiga vita mila na desturi zinazowabagua au kudhalilisha wanawake na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Mikataba yote ya Kimataifa inayohusu ustawi wa mwanamke;
(b) Kuendeleza juhudi za kuhamasisha wanawake na kuwajengea uwezo na uthubutu ili kushiriki kikamilifu katika mabaraza ya maamuzi ya ngazi mbalimbali za uongozi; na

(c) Kuanzisha jumla ya vikundi vya kiuchumi 500 vya wanawake na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo ili kujiajiri wao wenyewe.

**Wazee**

134. Wazee ni hazina na chemchem ya busara katika jamii kwa kuwa mchango wao katika ujenzi wa Taifa letu ni wa kutukuka na wa kupigiwa mfano. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ chini ya CCM imeendeleza jududi za kuwaendeleza wazee na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Jumla ya wazee 91 wameendelea kupatiwa huduma ya makazi na mahitaji mengine muhimu katika Nyumba za Wazee za Serikali (Unguja na Pemba). Aidha, jumla ya wazee 149 wameendelea kupatiwa msaada wa fedha kwa ajili ya kuweza kujikimu kimaisha kila mwezi; na

(b) Majengo matatu ya Nyumba za Wazee Sebleni zikiwemo nyumba mbili na ukumbi wa mikutano yamefanyiwa matengenezo makubwa. Miundombinu ya maji na umeme katika majengo hayo pia yameimarishwa.

135. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kwamba SMZ inaendelea kuchukua hatua thabiti za kuwatunza na kuwaendeleza wazee kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuimarisha huduma za kijamii na mahitaji muhimu kwa wazee wanaotunzwa katika nyumba za wazee; na

(b) Kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa programu maalumu ya malipo ya pensheni na huduma nyingine muhimu kwa wazee wote wa Zanzibar zikiwemo huduma za usafiri na matibabu bure.

**Watu wenye ulemavu**

136. Watu wenye ulemavu wanayo haki kwa mujibu wa Katiba ya kutambuliwa utu wao, kuendelezwa, kuheshimiwa na kulindwa dhidi ya vitendo vinavyoshusha utu wao ikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu. Kwa kutambua uwezo mkubwa walionao watu wenye

ulemavu katika kujiendeleza na kuchangia uchumi na maendeleo ya Taifa letu, katika kipindi cha 2010-2015, SMZ chini ya uongozi wa CCM imewaendeleza watu wenye ulemavu ambapo pamoja na mambo mengine imeanzisha Mfuko Maalumu na kuupatia jumla ya Shilingi Milioni 167.6. Aidha, usajili wa watu wenye ulemavu umefanyika katika wilaya zote za Unguja na Pemba ili kufahamu idadi yao kwa lengo la kuwapatia visaidizi pamoja na dawa.

137. **Ili kuwaendeleza watu wenye ulemavu, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa SMZ inaendeleza jitihada za kuimarisha ustawi wa watu wenye ulemavu kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali zenye lengo la kuwaendeleza watu wenye ulemavu na kuwapatia haki zao za msingi bila vikwazo;

(b) Kuimarisha Mfuko wa Watu wenye Ulemavu na kuwapatia huduma ya visaidizi pamoja na dawa bila malipo; na

(c) Kuendeleza mafunzo na elimu kwa wazazi, walezi na walimu juu ya makuzi ya mtoto mwenye ulemavu.

**Wafanyakazi**

138. Wafanyakazi wanao mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi. Ili kuhakikisha kwamba mchango wa wafanyakazi unaongezeka, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), SMZ imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha maslahi yao na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Sheria ya Ajira imefanyiwa mapitio na Kanuni kumi (10) zimetayarishwa na kuanza kutumika. Kanuni hizo zinahusu maslahi ya wanafanyakazi wa Sekta Binafsi, usajili na utendaji kazi wa vyama vya wafanyakazi, mikataba, likizo bila ya malipo na makundi maalumu ya wafanyakazi. Aidha, Kanuni za Utumishi wa Umma zimeandaliwa na kusambazwa kwa wahusika;

(b) Mashirikiano ya utatu kati ya Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi, Waajiri na Serikali yameimarishwa na majadiliano ya pamoja yameendelezwa. Kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), Toleo Maalumu la Sheria za Kazi kwa lugha nyepesi ikiwemo Sheria ya Ajira, Sheria ya Uhusiano Kazini, Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sheria ya Fidia na Sheria ya Usafiri Baharini limetayarishwa na kuanza kutumika;

(c) Jumla ya wananchi 19,758 wamepatiwa ajira. Kati yao 5,667, wameajiriwa katika Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na 7,256 Sekta Binafsi na 6,835 walipata ajira kupitia Vyama vya Ushirika. Aidha, wananchi 3,400 walijiajiri wenyewe baada ya kupatiwa mikopo na wengine 4,000 wamepata ajira zisizokuwa za moja kwa moja;

(d) Ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa ajira hasa kwa vijana, Kituo Maalumu cha Kutoa Taarifa za Soko la Ajira kimeanzishwa. Jumla ya vijana 2,473 wameorodheshwa na 1,978 kati yao wamefanikiwa kuajiriwa nje ya nchi kupitia Kituo hicho;

(e) Maslahi ya Watumishi wa Umma yameimarishwa kwa kuwaongezea mshahara pamoja na posho katika mwaka 2011 na 2014; na

(f) Kwa kuzingatia Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Sehemu za Kazi 351 zimesajiliwa na taarifa zake kuhifadhiwa katika daftari la usajili wa sehemu za kazi. Aidha, taasisi 1,067 za kazi zimefanyiwa ukaguzi (Unguja na Pemba) na kupatiwa ushauri na maelekezo ya kisheria.

139. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa SMZ inaendelea kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuendeleza mashirikiano ya utatu kati ya Serikali, Waajiri na Wafanyakazi kupitia chombo chao (Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi) ili kuimarisha mahusiano mema;

(b) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana na kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma kwa kuandaa programu mbalimbali za mafunzo na upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa, kuongeza maslahi ya watumishi ili kuongeza ufanisi na tija; na

(c) Kufanya ukaguzi katika maeneo 180 na kusajili taasisi za kazi 140 pamoja na programu mbalimbali zinazohusu masuala ya kazi.

**Hifadhi ya Jamii**

140. Katika kuhakikisha kwamba huduma za Hifadhi ya Jamii zinaimarika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Jumla ya wanachama waajiri wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kutoka Serikali Kuu imefikia 295, Mashirika ya Serikali 80 na Taasisi Binafsi ni 3,472. Idadi ya wanachama waajiriwa wa Serikali Kuu ni 133,337, Mashirika ya Serikali ni 10,613;

(b) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) umeanzisha mfumo wa uchangiaji wa hiari ili kutoa fursa kwa wananchi wengi zaidi kunufaika na matunda ya Mfuko huo. Jumla ya wanachama 4,970 kutoka vikundi vya ushirika vya uzalishaji mali, ujasiriamali, watu binafsi na Wazanzibari wanaofanyakazi nje ya nchi wamesajiliwa chini ya mfumo huo na jumla ya shilingi Milioni 122 zimekusanywa;

(c) Ili kutunisha mapato yake na kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, Mfuko umewekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi. Miongoni mwa miradi hiyo, ni ujenzi wa Kiwanja cha kufurahishia watoto cha Umoja – Kariakoo (Unguja) na Kiwanja cha Watoto cha Uhuru – Tibirinzi (Pemba) pamoja na ujenzi wa Mnara wa Kumbukumbu ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mfuko pia umeweza kutoa mikopo kwa taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi. Mfuko pia umenunua jumla ya nyumba 10 katika eneo la Mbweni Unguja ambazo zimepangishwa kwa taasisi za Serikali na watu binafsi; na

(d) Mfuko umeimarisha mafao ya wanachama wake wanaostaafu kwa kuongeza kiwango cha malipo ya kiinua mgongo na pensheni.

141. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM kitaielekeza SMZ kuimarisha zaidi huduma za Hifadhi ya Jamii kwa kufanya mambo yafuatayo:-**

(a) Kusimamia Utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii;

(b) Kuimarisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili uendelee kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi inayozalisha faida kubwa na kukuza mapato ya mfuko huo; na

(c) Kuhakikisha kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unaendelea kuboresha malipo ya pensheni na kuanzisha mafao mbalimbali kwa wanachama wake.

## SURA YA SABA
## MAENEO MENGINE MUHIMU

### Kuimarisha Muungano

142. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa mwaka 1964 ambao umedumu kwa kipindi cha miaka 51 sasa, umekuwa daraja lisilotetereka la kuwafikisha Watanzania katika azma yao ya kupata maendeleo, amani na ustawi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuzisimamia Serikali katika jitihada za kuimarisha Muungano kwa kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoukabili kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na maendeleo.

143. **Katika kipindi cha utekelzaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kizisimamia Serikali zake ili zitekeleze majukumu yake kikamilifu kwa lengo kuhakikisha Muungano wetu unakuwa imara zaidi na kwamba amani na utulivu vinaendelea kuwepo kwa kufanya yafuatayo:-**
    (a) Kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
    (b) Kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizokuwepo kwa kuweka utaratibu wa kikatiba na kisheria wa kutatua changamoto zitakazojitokeza;
    (c) Kuendelea kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha uchumi katika pande mbili za Muungano hususan katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa manuafaa ya pande zote; na
    (d) Kuendeleza harakati za kuulinda na kuutetea muungano kwa kuzishirikisha asasi zisizo za Serikali kuimarisha utoaji wa elimu ya uraia mashuleni, vyuoni na vyuo vikuu pamoja na makundi mengine.

### Utawala Bora na Demokrasia

144. Utawala Bora na Demokrasia ni moja ya nyenzo muhimu katika kuhakikisha Taifa linakuwa na utawala unaozingatia Sheria, Uwazi na

Uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kutokomeza udikteta na umasikini katika jamii. Malengo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii hayataweza kufikiwa iwapo haki, usawa, uwazi na uwajibikaji vitakosekana. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Uchaguzi huru na wa haki umeendelea kufanyika katika ngazi mbalimbali za uongozi;

(b) Hatua zimeendelea kuchukuliwa katika kukuza, kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora katika jamii;

(c) Serikali zimeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(Open Government Partnership - OGP).* Aidha, Serikali imeandaa Rasimu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(d) Mfumo wa Takwimu Huria umeanzishwa ambao utakuwa na Tovuti Kuu ya Takwimu Huria, ili kuwezesha wananchi na wadau wengine kupata taarifa za uendeshaji wa Serikali kwa urahisi na kuzitumia katika shughuli na malengo mbalimbali; na

(e) Mchakato wa kutungwa kwa Katiba mpya umeendeshwa na umefikia hatua ya **Katiba Inayopendekezwa** iliyopitishwa na Bunge Maalumu la Katiba ambayo itapigiwa Kura ya Maoni na wananchi;

(f) Mfumo wa Kujitathmini katika Masuala ya Utawala Bora (APRM) umeandaliwa na umeanza kufanya kazi;

(g) Katika kupanua demokrasia, Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu vimeongezeka kutoka 17 mwaka 2005 hadi vyama 22 mwaka 2015;

(h) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeanza zoezi la kusajili na kutoa vitambulisho vya uraia ambapo hadi Machi 2015 jumla ya wananchi milioni 5 Tanzania Bara na 600,000 Tanzania Zanzibar wameshapata vitambulisho.

145. **Ili kuendeleza Utawala Bora, Demokrasia na Uwajibikaji, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), CCM itahakikisha kuwa, Serikali inatekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuendeleza jitihada za kukuza, kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala wa Sheria katika ngazi zote za uongozi;
(b) Kuifanyia mapitio Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kuiboresha na pia kutunga Sheria mpya itakayotenganisha shughuli za uongozi wa umma na biashara;
(c) Kuimarisha Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia kuanzisha Mahakama Maalumu ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa lengo la kuharakisha uchunguzi na utoaji hukumu kwa makosa hayo;
(d) Kuimarisha mfumo wa utoaji haki kwa kufanya maboresho katika utendaji wa vyombo vya maamuzi ikiwemo Mahakama, Ofisi ya Mwendesha Mashitaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;
(e) Kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi;
(f) Kuendelea na kukamilisha zoezi la uandikishaji na utoaji wa vitambulisho vya uraia;
(g) Kukamilisha mchakato wa kutunga Katiba mpya na kuanza kuitekeleza kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba; na
(h) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM) na kutekeleza mapendekezo yaliyomo katika ripoti zake za mara kwa mara;

**Vyombo vya Ulinzi na Usalama**

146. Kwa kutambua kazi kubwa iliyofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama katika kudumisha amani, usalama na utulivu nchini na kwa kuzingatia umuhimu wa kuendeleza mafanikio haya, katika kipindi cha Ilani hii (2015-2020), CCM itazielekeza Serikali zake kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea raslimali watu na raslimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu.
(ii) Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo: makazi, mafunzo na zana za kazi za kisasa.

(iii) Kuendelea kuweka mazingira yatakayowezesha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria.

(iv) Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika kupeleka askari wetu kushiriki majukumu ya ulinzi wa amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

(v) Kuendeleza na kuimarisha mpango wa ulinzi shirikishi na kuwashirikisha wadau mbalimbali nchini kutoa elimu kwa umma dhidi ya imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino). Aidha, hatua kali na za haraka za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kujihusisha na uhalifu wa aina hii, ujambazi na vitendo vyenye mwelekeo wa ugaidi.

(vi) Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha haramu *(money laundering),* biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu.

(vii) Kuimarisha uwezo wa vikosi vya Zimamoto na Uokoaji kwa kuvipatia mafunzo na zana za kisasa za kupambana na matukio ya moto, ajali na majanga mengine ya asili.

**Serikali za Mitaa**

147. Serikali za Mitaa zimeundwa kwa ajili ya kupeleka madaraka na huduma karibu na wananchi na kuhakikisha wananchi wanashirikishwa katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo mijini na vijijini. Katika kipindi cha 2010-2015, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji zimefanyiwa mapitio kwa lengo la kuboresha mifumo ya usimamizi wa mamlaka hizo;

(b) Kiwango cha ruzuku ya Serikali Kuu kinachopelekwa katika Halmashauri zote kimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 950 mwaka 2010/2011 hadi Shilingi trilioni 2.4 mwaka 2014/2015;

(c) Katika usimamizi wa matumizi sahihi ya fedha, ukaguzi wa mara kwa mara umefanyika na hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya watendaji wa Halmashauri waliojihusisha na vitendo vya ubadhirifu na wizi wa fedha na rasilimali za wananchi zimeendelea kuchukuliwa.

148. **Ili kuziendeleza Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika kipindi cha 2015-2020 ya Utekelezaji wa Ilani hii, CCM itahakikisha kwamba, Serikali inatekeleza yafuatazo:-**

(a) Kuendelea kuzifanyia mapitio Sheria zote zinazohusiana na Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Tawala za Mikoa ili kuharakisha mchakato wa kugatua madaraka kwa lengo la kuziwezesha kutoa huduma bora zaidi kutoka ngazi ya Kitongoji/Kijiji hadi Kata;

(b) Kuendelea kuzijengea uwezo Serikali za Vijiji kwa kuzipatia raslimali watu na fedha ili ziweze kupanga na kusimamia kwa ukamilifu miradi yao ya maendeleo;

(c) Kuendelea kuongeza kiwango cha ruzuku kutoka Serikali Kuu kinachopelekwa kwenye Halmashauri zote nchini kupitia Bajeti ya Serikali ya kila mwaka kwa kadri ya uchumi utakavyokua;

(d) Kuendelea kuzihamasisha Halmashauri zote nchini kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani (own sources) pamoja na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato;

(e) Kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za kijamii hususan afya, elimu, maji na miundombinu ya kiuchumi katika Halmashauri zote nchini pamoja na kuongeza idadi ya wataalamu wa fani mbalimbali; na

(f) Kuendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu na kisheria dhidi ya watendaji wa Halmashauri za wilaya watakaobainika kuhusika na vitendo vya ubadhirifu na wizi wa mali ya umma pamoja na matumizi mabaya ya madaraka.

**Mambo ya Nje**

149. **Ili kuimarisha mahusiano baina ya nchi yetu na nchi nyingine duniani, Chama Cha Mapinduzi kitaihimiza Serikali kufanya mambo yafuatayo katika kipichi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020:-**

(a) Kuendelea kushiriki kwenye utengamano wa kikanda na kuendeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuzingatia maslahi muhimu ya nchi yetu ili kunufaisha Watanzania wote;
(b) Kuendelea kuimarisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine na taasisi za kimataifa;
(c) Kuendelea kupigania mfumo wa haki wa utawala, siasa na uchumi duniani;
(d) Kuendelea kuunga mkono jitihada za kulinda amani na utulivu duniani;
(e) Kuendelea kupigania Diplomasia ya Uchumi na Siasa; na
(f) Kuendelea kujenga au kununua majengo kwa ajili ya balozi za Tanzania kwenye nchi ambazo kwa sasa yanakodishwa ili kupunguza gharama.

**Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)**

150. **Ili kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaihimiza Serikali kufanya mambo yafuatayo:-**

(a) Kutekeleza Mpangokazi wa miaka kumi wa kuelekea katika eneo la Sarafu moja la Afrika Mashariki;
(b) Kutekeleza ujenzi wa mitandao ya reli na barabara zinazounganisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
(c) Kuendelea na utekelezaji wa hatua za awali za mtangamano wa Afrika Mashariki za Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja ili kuhakikisha Watanzania wanaendelea kunufaika na fursa za kibiashara, uwekezaji na ajira zitokanazo na utekelezaji wa hatua hizo;

(d) Kuendelea kushirikiana na wadau kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wazitumie na kunufaika nazo; na

(e) Kuendelea na majadiliano na utekelezaji wa Ubia wa Biashara na uwekezaji baina ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani, Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU Economic Partnership Agreement – EPA) na Kuanzisha eneo Huru la Biashara la Utatu wa EAC-COMESA-SADC.

**Kuhamia Makao Makuu Dodoma**

151. **Chama Cha Mapinduzi kinatambua jitihada zilizofanywa na Serikali za kuunganisha mji wa Dodoma na mikoa mingine kwa njia ya barabara za lami. Aidha, baadhi ya majengo ya Serikali yameendelea kujengwa Dodoma likiwemo jengo la Bunge, Benki Kuu, Hazina, Chuo Kikuu cha Dodoma na Shirika la Nyumba la Taifa limejenga nyumba kwa ajili ya makazi ya wananchi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kutunga Sheria itakayoutambua mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi;

(b) Kusimamia azma ya Serikali ya kuhakikisha majengo yote ya Wizara za Serikali yanajengwa Dodoma badala ya Dar es Salaam; na

(c) Kuongeza kasi ya kupima viwanja kwa ajili ya makazi, viwanda na taasisi; na kuendelea kuboresha miundombinu ikiwemo maji, umeme na barabara.



*Wafanyakazi wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) wakipima viwanja kwa kutumia vifaa vya kisasa*

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

152. **Kupunguza na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni jambo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu. Pamoja na jitihada ambazo zimekuwa zikichukuliwa katika kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, bado zipo changamoto nyingi. Ili kubabiliana na changamoto hizo, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Ilani hii ya 2015-2020, kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**
   (a) Kupanga na kuendelea kutekeleza miradi ya upandaji miti ili kuondokana na hatari ya Taifa kugeuka kuwa jangwa kwa kuhakikisha kila Halmashauri inapanda na kutunza miti isiyopungua milioni 1.5 kila mwaka;
   (b) Kuhakikisha Halmashauri zote nchini zinaweka na kusimamia Sheria ndogo za hifadhi ya mazingira;
   (c) Kuweka utaratibu wa kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi kuhusu usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Utunzaji wa Maeneo ya Fukwe na rasilimali zilizopo;
   (d) Kuendelea kufanya tathmini ya vyanzo vya maji vilivyohifadhiwa, kuongeza vyanzo vipya na kufufua vilivyopotea ama kuharibika ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji safi na salama;
   (e) Kuweka utaratibu wa kupunguza bei ya gesi na majiko yake na kuhamasisha jamii kutumia umeme na nishati mbadala ili kuongeza idadi ya watumiaji wa nishati hizo kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 50 mwaka 2020 ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira; na
   (f) Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za viwanda ili zisiharibu mazingira.

**Kujenga uwezo wa kukabili majanga**

153. **Majanga ni matukio yanayojitokeza na yenye uwezo mkubwa wa kuleta maafa yanayohatarisha maisha ya watu na mali zao, miundombinu na huduma mbalimbali za jamii. Katika kipindi**

**cha miaka mitano ijayo (2015-2020), katika kukabiliana na maafa, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kusimamia kikamilifu Utekelezaji wa Sheria mpya ya Kukabiliana na Maafa katika ngazi zote kuanzia Taifa hadi Vijijini; na

(b) Kujenga Kituo cha Menejimenti ya Maafa na Mawasiliano ili kuongeza uwezo wa nchi katika kukabiliana na maafa.

**Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI**

154. **Katika kipindi cha miaka mitano ya Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kuendeleza kwa nguvu zaidi mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kupunguza au kuondokana kabisa na utegemezi wa wafadhili kwa kuanzisha Mfuko Maalumu wa UKIMWI (AIDS Trust Fund) ukiwa na lengo la kuongeza rasilimali kwa ajili ya kuboresha huduma za UKIMWI zinazotolewa;

(b) Kufanya jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi katika jamii kutoka asilimia 5.1 mwaka 2015 hadi asilimia 3.0 ifikapo 2020;

(c) Kuimarisha huduma za elimu ya UKIMWI kwa njia ya mawasiliano baina ya wanafamilia, watu mashuhuri, programu za mahali pa kazi na viongozi wa dini;

(d) Kuongeza usambazaji wa taarifa zinazohusu kubadili tabia hatarishi na upatikanaji wa huduma bora kwa waathirika wa UKIMWI kupitia Vyombo vya Habari;

(e) Kuendeleza tafiti za UKIMWI na kutathmini vipaumbele kwa ajili ya kufanya maamuzi na kuandaa programu za UKIMWI; na

(f) Kutoa elimu kwa umma juu ya uhusiano uliopo kati ya utumiaji wa dawa za kulenya na maambukizi ya VVU.

**Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

155. **Matumizi ya madawa ya kulevya ni tatizo linaloongezeka si hapa Tanzania tu, bali duniani kote. Madhara ya matumizi ya madawa ya kulevya ni makubwa hususan kwa vijana kwani yanapunguza nguvukazi ya Taifa na kuongeza gharama za**

**kuwatibu na kuwatunza waathirika. Katika kipindi kijacho, Chama kitaielekeza Serikali kuongeza jitihada za kupambana na madawa ya kulevya kwa kutekeleza yafuatayo:-**

(a) Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya;

(b) Kuongeza utoaji wa dawa na matibabu pamoja na kuanzisha vituo vya kuhudumia wananchi walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya;

(c) Kushirikiana na asasi za kijamii na kuziwezesha ili kuinua uwezo wa kushiriki katika kutoa elimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii zinazowazunguka; na

(d) Kusimamia kwa ukamilifu sheria mpya ya kudhibiti madawa ya kulevya.

**Vyombo vya Habari**

156. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Habari imeimarishwa zaidi na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Serikali imeweka mazingira bora yaliyowezesha kuanzishwa kwa vyombo vingi vya habari nchini;

(b) Matangazo ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC):-

(i) TBC imeendelea kuimarisha usikivu wa Radio na Televisheni katika maeneo yenye miinuko;

(ii) TBC imefunga mitambo ya kisasa ya idhaa ya TBC Taifa na TBC FM yenye uwezo wa kusikika kwa ufasaha bila mikwaruzo katika mikoa mbalimbali nchini; na

(iii) Shirika limejenga mitambo ya kurushia matangazo ya Televisheni katika mfumo wa kidijitali katika maeneo mbalimbali nchini.

(iv) Mitandao mingi ya kijamii imeanzishwa na kuwa moja ya njia kuu za upashanaji wa habari kwa haraka.

157. **Ili kuendeleza Tasnia ya Habari na Uhuru wa Vyombo vya Habari, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015-2020, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kwa kufanya mambo yafuatayo:-**

(a) Kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kwa urahisi na kwa wakati kwa mujibu wa Sheria;
(b) Kuharakisha mchakato wa kupitisha na kuanza kutekeleza Sheria kuhusu uhuru wa Wananchi kupata habari na uhuru wa Vyombo vya Habari kupata na kutoa habari;
(c) Kuhakikisha kwamba matangazo ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) yanasikika nchini kote kwa kulipatia uwezo wa rasilimali watu, fedha na vifaa vya kisasa;
(d) Kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari (MAELEZO) kama msemaji Mkuu wa Serikali;
(e) Kuanzisha Mfuko wa kuwaendeleza Wanahabari Kitaaluma;
(f) Kuhakikisha kwamba kunakuwepo Uhuru wa Vyombo vya Habari ili vitekeleze wajibu wake inavyopasa kwa mujibu wa Sheria; na
(g) Kujenga ushirikiano wa Kizalendo baina ya Vyombo vya Habari vya Umma na vya Binafsi katika kuitangaza Tanzania nchi za nje hasa katika eneo la Vivutio vya Utalii na kujenga Taswira ya nchi.

**Utamaduni**

158. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Utamaduni imeendelea kuimarishwa zaidi ambapo maeneo yote muhimu yanayohusu historia hasa ya mapambano ya ukombozi ya nchi yetu na Kusini mwa Afrika yameendelea kutunzwa na kutangazwa kama vivutio vya utalii.

159. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuimarisha na kuboresha Sekta ya Utamaduni nchini ili ichangie kikamilifu katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-**

(a) Kuhakikisha lugha ya Kiswahili inaendelezwa ndani na nje ya nchi na kutumika kama bidhaa ya soko na chanzo cha ajira kwa wataalamu na wapenzi wa Kiswahili. Aidha, kupanua wigo wa misamiati na istilahi za lugha za Kiswahili kwa kufanya utafiti wa Lugha za Kijamii;

(b) Kuandaa Sera ya Utamaduni wa Taifa kuhusu masuala ya Lugha ya Taifa, Filamu, Muziki, Ngoma za Asili na Sanaa;

(c) Kusimamia Utekelezaji wa Sheria zinazohusu shughuli za Filamu, Michezo ya Kuigiza, Muziki, Ubunifu kwa lengo la kulinda haki na Maslahi ya Makundi hayo; na

(d) Kuhamasisha na kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika kuboresha Miundombinu ya Kiutamaduni ikiwemo ya Tasnia ya Filamu, Michezo, Sanaa ya Muziki na Ubunifu kwa lengo kulinda haki na Maslahi ya Makundi hayo.

**Michezo**

160. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Sekta ya Michezo imeimarishwa zaidi na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Ukarabati wa miundombinu ya michezo nchini umefanyika ukiwemo uwanja wa Uhuru (Dar es Salaam), Nyamagana (Mwanza) na Sokoine (Mbeya);

(b) Sekta binafsi imehamasishwa ambapo kampuni binafsi ya AZAM imeanzisha Kituo cha Michezo na kujenga Uwanja wa kisasa wa Michezo;

(c) Jumla ya Vituo vya Michezo 75 vimeanzishwa kwa lengo la kuongeza fursa kwa watoto na vijana kuonesha vipaji vyao ili viweze kutambuliwa na kuendelezwa;

(d) Mashindano ya Michezo ya Shule za Msingi (UMITASHUMTA) na Sekondari (UMISSETA) imerudishwa na yanafanyika kila mwaka; na

(e) Mradi wa majaribio wa kufundisha riadha kwa watoto *(KIDS ATHLETICS)* umeanzishwa na unashirikisha shule 98 katika Mikoa minne ya Tanzania Bara na skuli 18 za Zanzibar.

161. **Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuimarisha Sekta ya Michezo ili kuinua kiwango cha michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuifanya Sekta ya Michezo kutoa**

**fursa za ajira husasan kwa vijana kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-**

(a) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo nchini;

(b) Kupanua wigo wa vyanzo endelevu vya fedha za uendeshaji na ugharamiaji wa maendeleo ya michezo hapa nchini kwa kuanzisha Bahati Nasibu ya Michezo;

(c) Kuhamasisha na kusisimua Maendeleo ya Michezo katika ngazi zote hapa nchini kwa kuendeleza matamasha ya Michezo kuanzia ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa;

(d) Kuweka vivutio vya kuwavutia wawekezaji na washiriki wengine kuwekeza na kugharamia shughuli mbalimbali za michezo nchini;

(e) Kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo na burudani kwa kushirikiana na makundi ya wanamichezo, jamii na mamlaka nyingine zilizopo;

(f) Kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, kuanzisha Kituo cha Kuendeleza Vipaji vya Wanamichezo Mahiri na kutumika kama kituo cha maandalizi ya wanamichezo wanaoiwakilisha Tanzania katika michezo ya Kimataifa (Olympic village);

(g) Kuendelea kufundisha wataalam wa michezo na kuhakikisha wanapatikana katika ngazi zote;

(h) Kuwahamasisha wanamichezo kujiunga na kunufaika na fursa zitolewazo na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ustawi na maisha yao ya baadaye; na

(i) Kuendeleza shughuli za michezo mashuleni ili kuibua vipaji vya michezo mbalimbali nchini.

**Tasnia ya Sanaa**

162. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2010-2015), Serikali imeendelea kuwatambua na kuthamini kazi za sanaa na wasanii nchini.

163. **Tasnia ya Sanaa ikiwemo filamu, muziki, michezo ya kuigiza inayo nafasi kubwa ya kupanua soko la ajira na kukuza pato la**

**mtu mmoja mmoja na Taifa kama ilivyo kwa nchi nyingi duniani. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii (2015-2020) Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali yake kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kuimarisha uwezo wa Bodi ya Filamu nchini ili isimamie kwa ukamilifu maendeleo ya tasnia ya Filamu kwa kuendeleza ujuzi katika sekta hii;

(b) Kuanzisha na kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Tasnia ya Sanaa utakaowezesha upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa wazalishaji, watengenezaji, wawekezaji wakubwa, wa kati na wadogo wa tasnia hii nchini;

(c) Kuwekeza katika mradi wa Ujenzi wa Jumba Changamani la Uzalishaji wa Filamu (Multipurpose Filamu Complex);

(d) Kuendeleza programu za Ujasiriamali kwa vijana na makundi mbalimbali kwa kutoa ushauri, mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi kwa wajasiriamali walio katika tasnia ya sanaa na kuweka msukumo mkubwa katika maendeleo ya tasnia ya sanaa;

(e) Kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Filamu inakuwa na bidhaa zenye ubora, wataalamu wenye weledi na kuondokana na uharamia wa bidhaa za filamu;

(f) Kuhakiksha kazi za wasanii zinalindwa ili zisighushiwe wala kuibiwa;

(g) Kuhakikisha wasanii wanapata maslahi wanayostahili kutokana na kazi zao kwa kuboresha mazingira ya kisheria;

(h) Kuweka msukumo katika kuhakikisha kwamba shughuli na biashara za sanaa zikiwemo filamu, muziki, ngoma za asili, michezo ya kuigiza na kazi nyingine za ubunifu zinarasimishwa ili kuendeleza tasnia hii na wasanii wenyewe;

(i) Kuanzisha maeneo changamani ya shughuli za utamaduni nchini kwa kujenga miundombinu ya kisasa;

(j) Kuweka kumbukumbu na kuhimiza matumizi ya mila na desturi dhidi ya utandawazi kwa kufanya utafiti wa mila na desturi za jamii ya Kitanzania; na
(k) Kuhifadhi kumbukumbu ya ushiriki na mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika kwa kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi.

**Kuendeleza Makundi Maalum**
**Wazee**

164. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuwaenzi wazee kutokana na michango yao katika kulijenga Taifa letu.

165. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**
 (a) Kuhakikisha wazee wanatambuliwa na kupatiwa huduma za matibabu bila malipo;
 (b) Kuhakikisha wazee wanapata haki zao za kisheria na kupata fursa sawa katika ngazi zote;
 (c) Kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili vikiwemo mateso na mauaji;
 (d) Kuwawekea miundombinu na mazingira bora yatakayowawezesha kwenda wanapotaka na kutumia vyombo vya usafiri wa umma kwa gharama nafuu; na
 (e) Kuweka utaratibu na vigezo vitakaowezesha wazee wote nchini kulipwa pensheni.

**Watu Wenye Ulemavu**

166. **Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba: "Binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake". Kwa imani hii, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuhakikisha kwamba:-**
 (a) Walemavu wote nchini wanaendelea kutambuliwa na kulindwa na vitendo vinavyoshusha utu vikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu;

(b) Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) wanalindwa dhidi ya ukatili na ubaguzi wa aina yoyote;

(c) Kuhakikisha wanapata elimu kwa kutumia vifaa maalumu na kushiriki katika nafasi za uwakilishi na shughuli za kijamii;

(d) Kuwawekea miundombinu na mazingira rafiki yatakayowawezesha kwenda wanapotaka, kutumia vyombo vya usafiri na kupata habari;

(e) Kuboresha mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu kwa kuwawezesha kupata taarifa mbalimbali kwa urahisi kwa kutumia lugha ya alama, alama mguso, maandishi ya nukta nundu, maandishi yaliyokuzwa au njia nyingine zinazofaa;

(f) Kuhakikisha wanapata ajira na kufanya kazi; na

(g) Kupata huduma bora za afya, uzazi salama, marekebisho na utengemao.

**Wanawake**

167. Kwa kutambua kwamba wanawake wanao uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko makubwa katika jamii, ipo haja ya kuendelea kuwathamini, kuwalinda na kuwaendeleza ili waweze kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo ya Taifa letu.

168. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020, Chama kitaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kuweka utaratibu wa kikatiba na kisheria utakaowawezesha wanawake kushika nafasi sawa (50/50) za uongozi katika vyombo vya maamuzi katika ngazi zote;

(b) Kuhakikisha wanawake wanapata haki zao za kisheria na kupata fursa sawa katika ngazi zote;

(c) Kupata haki ya kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji, dhuluma, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na mila potofu; na

(d) Kuhakikisha kuwa ajira za wanawake zinalindwa wakati wa ujauzito na pale wanapojifungua.

**Watoto**

169. Kila mtoto ana haki ya kuishi, kukua na kulelewa kikamilifu ili Taifa kwa siku za baadaye lipate raia wema na waadilifu.

170. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015 – 2020, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza mambo yafuatayo:-**

(a) Kuhakisha watoto wanalindwa dhidi ya uonevu, ukatili, udhalilishaji, utumikishwaji na mila potofu;

(b) Kuhakikisha watoto wanapata lishe bora, huduma ya afya, makazi na mazingira yanayomjenga kimwili, kiakili na kimaadili;

(c) Kuwapatia haki ya kushiriki katika shughuli zinazolingana na umri, kuhakikisha kwamba wanapata malezi na ulinzi kutoka kwa wazazi, walezi, jamii au mamlaka ya nchi bila ubaguzi wowote; na

(d) Kuboresha viwanja vya kuchezea watoto katika ngazi za mitaa, vijiji na vitongoji.

**Vijana**

171. Vijana ni chachu ya maendeleo ya nchi katika nyanja zote kwani ndiyo nguvu kazi ya Taifa na yenye fikra ya ubunifu endelevu. Kwa kutambua uwezo na mchango wao jitihada kubwa zimefanywa na Serikali katika kipindi kilichopita kuwashirikisha vijana katika shughuli za maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

172. **Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii (2015-2020), CCM itaielekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

(a) Kuendelea kuwashirikisha vijana kwa kuwapa nafasi za maamuzi katika ngazi zote kutegemeana na sifa, weledi na uadilifu;

(b) Kuwaandaa na kuwawezesha vijana kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za Baraza la Taifa la Vijana;

(c) Kuendelea kutoa elimu kwa vijana kwa kuwatumia wadau mbalimbali ili kuwajenga kuwa wazalendo na kuepuka vishawishi vitakavyowaharibia malengo yao ya baadaye;

(d) Kuvitambua na kuviendeleza vipaji vya vijana katika nyanja za michezo, sanaa, elimu, ubunifu na uongozi; na

(e) Kuanzisha uraghibishi kwa vijana waweze kujiajiri kwa kuthamini kazi nyingine za mikono na utaalamu kama vile kilimo, ufundi, michezo, sanaa na kazi nyingine za kitaaluma.

**Wafanyakazi**

173. Chama Cha Mapinduzi kwa asili yake ni chama cha Wakulima na Wafanyakazi. Wafanyakazi kwa tafsiri pana ni waajiriwa na waliojiajiri. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, jitihada zimeendelea kuchukuliwa ili kuboresha maslahi ya wafanyakazi ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(a) **Mishahara ya Wafanyakazi:**

(i) Bodi za Kurekebisha Mishahara katika Sekta Binafsi zimeongezeka kutoka nane mwaka 2010 hadi 12 mwaka 2013 ambapo kima cha chini cha mshahara katika sekta hiyo kimeongezeka mara mbili. Aidha, nyongeza ya mwaka 2013 ya kima cha chini cha mshahara imeongezeka kati ya asilimia 21 hadi 65 ya viwango vya mishahara vya mwaka 2010;

(ii) Kodi ya Mapato ya Wafanyakazi (PAYE) imepunguzwa kutoka asilimia 18 mwaka 2005 hadi asilimia 11 mwaka 2015;

(iii) Kima cha chini cha mshahara katika sekta ya umma kimeongezeka kutoka Shilingi 65,000 mwaka 2005 hadi Shilingi 300,000 mwaka 2015; na

(iv) Sheria za Kazi zimeendelea kufanyiwa mapitio ili kuwawezesha wafanyakazi kujiunga katika vyama huru vya wafanyakazi kwa hiari yao.

(b) **Afya na Usalama Mahala pa Kazi:**

(i) Jumla ya kaguzi 220,350 zimefanyika ikiwa ni wastani wa kaguzi 40,000 kwa mwaka kwa lengo la kuhakikisha waajiri wanafuata Sheria za Kazi ipasavyo;

(ii) Jumla ya kaguzi za kawaida 26,412 na kaguzi maalumu 53,807 kuhusiana na Afya na Usalama kazini zimefanyika.

Aidha, wafanyakazi 136,076 walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari za kiafya zitokanazo na maeneo wanayofanyia kazi;

(iii) Maafisa 4,931 wamepatiwa mafunzo mbalimbali kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

(iv) Jumla ya sehemu za kazi 5,595 zilisajiliwa na kupewa vyeti vya usajili; na

(v) Jumla ya sehemu za kazi 398 zilipewa leseni za kukidhi viwango vya chini vya Sheria Na. 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

(c) **Migogoro Sehemu za Kazi:**

(i) Migogoro 10,281 imesuluhishwa ambapo uamuzi ulitolewa kwa migogoro 6,057 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA);

(ii) Wastani wa muda wa kusikiliza na kusuluhisha migororo ya wafanyakazi umepungua kutoka siku 30 hadi siku 12 wakati muda wa kusikiliza na kuamua umepungua kutoka siku 90 hadi siku 85;

(iii) Wafanyakazi wapatao 1,908,000 na waajiri 6,890 wamepewa elimu kuhusu Sheria za Kazi;

(iv) Jumla ya Mabaraza ya Wafanyakazi 265 yameundwa katika Taasisi za Umma ikiwa ni sawa na asilimia 86.6 ya lengo;

(v) Jumla ya vyama saba vya wafanyakazi na shirikisho moja la vyama vya wafanyakazi vimesajiliwa kati ya mwaka 2010 na 2015 kwa lengo la kuongeza na kuboresha wigo wa ushiriki, majadiliano na utetezi wa haki za wafanyakazi na waajiri katika sehemu za kazi;

(vi) Vyama vya Wafanyakazi vilivyosajiliwa vimeongezeka kutoka vyama 24 mwaka 2009 hadi 31 mwaka 2015; na

(vii) Waajiri wameendelea kushirikisha wafanyakazi katika hatua za maamuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika maeneo ya kazi.

(d) **Sheria ya Ajira kwa Wageni:-**

Sheria ya Ajira kwa wageni imetungwa mwaka 2015 na kuweka mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni ili kulinda ajira za Watanzania zisichukuliwe na wageni.

(e) **Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

(i) Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) imeanzishwa mwaka 2010;

(ii) Sheria za mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii zimefanyiwa marekabisho ili kuipa SSRA mamlaka ya kusimamia na kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(iii) Kanuni za kukokotoa mafao ya pensheni zimerekebishwa mwaka 2014 ili kupunguza tofauti ya malipo ya mafao ya pensheni kwa wanachama miongoni mwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuanzisha mafao mapya kwa wanachama;

(iv) Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupitia Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 yameruhusu wanachama kujiunga na mfuko wowote wanaoupenda. Aidha, marekebisho hayo yametoa fursa kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kusajili wanachama kutoka katika sekta isiyo rasmi; na

(v) Katika mwaka 2014/2015 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wanaougua au kuumia kazini umeanzishwa.

174. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali yake kuendelea kulinda na kuboresha haki na maslahi ya wafanyakazi kwa kufanya mambo yafuatayo:-**

(a) Kuhakikisha kwamba mfanyakazi atalipwa kima cha chini cha mshahara kinachokidhi mahitaji muhimu ya maisha kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi wa Taifa;

(b) Kuwapunguzia wafanyakazi mzigo wa Kodi ya Mapato (PAYE) kufikia tarakimu moja (single digit);

(c) Kuboresha na kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wakiwa sehemu za kazi;

(d) Kuridhia mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) yenye maslahi kwa wafanyakazi;

(e) Kuboresha mazingira ya utendaji wa wafanyakazi wa Sekta Binafsi ikiwemo kupewa mikataba kwa mujibu wa Sheria;

(f) Kuweka utaratibu wa kupunguza pengo la mapato kati ya wafanyakazi wa ngazi ya chini na juu;

(g) Kuhakikisha kwamba wizi, ubadhirifu, utoro na rushwa vinakomeshwa kwa lengo la kuongeza tija sehemu za kazi; na

(h) Kuweka utaratibu maalumu wa kutoa motisha kwa wafanyakazi wanaofanyakazi katika mazingira magumu.

(i) **Hifadhi ya Jamii:**

  (i) Kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuimarisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili iendelee kutoa huduma bora na endelevu kwa wanachama wao; na

  (ii) Kuhamasisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuanzisha mfuko mkubwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi na wajasiriamali wadogo kwa masharti nafuu.

# SURA YA NANE
# CHAMA CHA MAPINDUZI

175. Ilani hii ya Chama Cha Mapinduzi ya kipindi cha mwaka 2015-2020 imejikita katika kupambana na changamoto kubwa nne ambazo ni: **umaskini, ukosefu wa ajira hasa kwa vijana, rushwa** na **ubadhirifu wa mali za umma;** na **jukumu la kudumisha amani na utulivu**. Hii ndiyo ahadi na nadhiri kubwa ambayo Chama Cha Mapinduzi kinaweka kwa wananchi endapo watakichagua na kuunda Serikali.

176. Kwa muktadha huo katika kipindi cha Utekelezaji wa Ilani hii, Serikali zote mbili zitakazoundwa na CCM yaani Serikali ya Jamhuri ya

Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zitatumia nguvu zote na kwa kushirikisha Sekta Binafsi zitasimamia mambo yafuatayo:-

(a) Kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambayo inategemewa na wananchi walio wengi nchini;
(b) Kuweka msukumo katika uanzishaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi;
(c) Kuweka mipango madhubuti ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na matokeo ya utekelezaji yawe dhahiri;
(d) Urasimishaji wa raslimali za wanyonge na hasa upimaji wa ardhi na utoaji Hatimiliki za Kimila kwa kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi, kifedha na kisheria.
(e) Kuongeza wigo wa kukusanya mapato ya ndani yatayotosheleza Bajeti ya Serikali zetu kwa lengo la kuendelea kupunguza utegemezi wa misaada ya kibajeti kutoka mataifa ya nje;
(f) Kuongeza uwekezaji katika kukuza Sekta ya Sayansi na Teknolojia ambayo ndiyo muhimili wa kuendesha uchumi wa kisasa wenye tija;
(g) Kuboresha miundombinu ya Barabara, Reli, Bandari, Nishati, Vyombo vya Majini na Usafiri wa Anga;
(h) Kuimarisha huduma za kijamii, hasa Elimu, Maji na Afya;
(i) Kuimarisha usimamizi katika Sekta zinazokuwa kwa haraka kama Utalii, Madini, Mawasiliano, Huduma ya Fedha na Biashara; na
(j) Kuviimarisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Vyombo vya Kutoa Haki, na Vyombo vya Udhibiti na Nidhamu.

**Kusimamia Utekelezaji wa Ilani**

177. Wajibu wa CCM hauishii katika kutoa ahadi kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi na kuzikabidhi Serikali zake kwa utekelezaji, bali pia ina wajibu mkubwa wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo. Hivyo, ni muhimu kwa CCM kuzingatia utaratibu iliyojiwekea wa namna ya kusimamia na kukagua utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi.

178. Tukirejea uzoefu wa miaka ya nyuma, jukumu hili la CCM kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika ngazi mbalimbali kuanzia Vijijini

hadi Taifa, limetekelezwa kwa kiwango cha wastani, hasa katika ngazi ya Vijiji, Kata na Majimbo.

179. Kwa utaratibu wa sasa, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika ngazi ya Taifa unafanywa na Wabunge na Wawakilishi kupitia Kamati zao za Kudumu na pia kwa Wabunge na Wawakilishi kuwauliza maswali mawaziri ndani ya Bunge na Baraza la Wawakilishi. Wabunge na Wawakilishi wanaotokana na CCM wanatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa Ilani katika vikao vya CCM, yaani kwenye vikao vya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kupitia Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Wabunge na Wawakilishi wote wa CCM. Utaratibu huu unatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha.

180. Vikao vya Halmashauri Kuu za Wilaya, Kata, Wadi, Jimbo, na Matawi vinapaswa kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika maeneo hayo kupitia taarifa kutoka kwa Wabunge na Wawakilishi wa majimbo husika, na pia kutoka kwa Madiwani kwa upande wa ngazi ya Kata, Wadi, Jimbo na Matawi. Katika ngazi za Kata na Matawi, utekelezaji wa utaratibu huu ni wa wastani.

181. Katika kipindi cha Ilani hii (2015-2020), utaratibu wa vikao vya CCM kupokea taarifa za utekelezaji wa Ilani kutoka kwa wahusika utazingatiwa kwa ukamilifu. Utaratibu huu utakiwezesha Chama Cha Mapinduzi kufanya tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika ngazi mbalimbali kila baada ya miezi mitatu kwa mujibu wa vikao vya kikatiba vya CCM.

182. Njia nyingine ya kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Ilani ya Uchaguzi unaotekelezwa na Serikali zake, ni kwa viongozi wa CCM kutembelea miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ili kujiridhisha juu ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo. Utaratibu huu wa viongozi wa CCM wa Matawi, Kata, Wadi na Majimbo ambako miradi mingi ndiko iliko, utekelezaji wake bado upo chini.

183. Katika kipindi cha utekelezaji wa ahadi zilizomo katika Ilani hii, viongozi wa ngazi zote za CCM ni muhimu wajiwekee ratiba za kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa katika maeneo yao. Endapo watakuta utekelezaji unahitilafu, viongozi hao watoe taarifa haraka kwa viongozi wa Serikali wa ngazi ya juu yao.



*Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Abdulrahaman Kinana (kulia) akishiriki katika shughuli za kilimo katika moja ya ziara za kukagua Uhai wa Chama na Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi alizofanya katika Wilaya zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

**Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu**

184. Kama ambavyo Serikali za CCM zinavyowajibika kutekeleza maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama, vile vile CCM inawajibu wa kutekeleza maelekezo yanayotolewa na Mikutano Mikuu. Mkutano Mkuu

wa CCM wa Taifa wa mwaka 2012 ulitoa maelekezo mengi yanayotakiwa kuzingatiwa.

Kwa hiyo, kupitia Ilani hii, CCM ina jukumu la kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mkutano Mkuu wa Taifa mwaka 2012. Utekelezaji makini wa maelekezo hayo utakipatia Chama Cha Mapinduzi uhai na nguvu thabiti ya kuzisimamia Serikali zake ili zitekeleze kwa ufanisi Ilani hii. Tukumbuke kaulimbiu isemayo; "***Chama madhubuti huzaa Serikali madhubuti"***; na ***"Chama legelege huzaa Serikali legelege"*** (…Mwongozo wa CCM wa 1981).

**Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Nane**

185. Mkutano Mkuu wa Nane wa CCM wa Taifa uliofanyika mjini Dodoma tarehe 11-13 Novemba, mwaka 2012 ulipitisha maazimio mengi yenye umuhimu mkubwa katika kudumisha uhai wa Chama chetu ili kiendelee kuwa na nguvu na uhalali wa kushika dola. Baadhi ya maazimio hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) **Kudumisha Muungano**

Mkutano Mkuu wa Taifa ulielekeza kuwa hatua ziendelee kuchukuliwa za kuuenzi na kuuimarisha Muungano wetu wa kihisitoria wa Tanganyika na Zanzibar wenye muundo wa Serikali mbili. Aidha, changamoto za Muungano huu zitafutiwe majawabu kila zinapojitokeza ili kuimarisha, kudumisha na kuendeleza udugu, umoja na mshikamano uliopo baina ya pande mbili za Muungano.

Katika kutelekeza azimio hili, CCM imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali zote mbili katika kusimamia mchakato wa kupata **Katiba Inayopendekezwa** na ambayo hatimaye itazaa Katiba mpya ya nchi yetu.

Aidha, Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba ndani ya Katiba Inayopendekezwa, kero nyingi za Muungano zimepatiwa

majawabu ya kuridhisha. Hivyo, iwapo Katiba Inayopendekezwa itapitishwa hapana shaka itaimarisha Muungano wetu.

(b) **Uimarishaji wa Chama**

Mkutano Mkuu wa Taifa ulielekeza kwamba jitihada ziendelezwe za kujenga na kuimarisha Chama Cha Mapinduzi, na kwamba Viongozi wa Chama wa ngazi zote waongeze jitihada za kuwa karibu na wananchi na kuwasemea na kuwatetea. Aidha, mikutano baina ya Viongozi wa Chama na wananchi ya kufafanua na kueleza mambo mbali mbali ifanyike mara kwa mara.

Kwa hiyo, katika kipindi hiki viongozi wa ngazi zote wanawajibika kufanya ziara za mara kwa mara katika ngazi zote ili kukutana na wananchi, kusikiliza matatizo yao na kuyatafutia majawabu.

(c) **Maadili na Miiko ya Uongozi**

Mkutano Mkuu wa Taifa ulikemea tabia ya baadhi ya viongozi wa umma wanaotumia nafasi zao kujilimbikizia mali isivyo halali hali inayosababisha madhara makubwa ya kimaadili na kiuongozi katika nchi yetu. Mkutano Mkuu uliiagiza Serikali kuchukua hatua za kuondoa migongano ya kimaslahi inayojitokeza, kwa kusimamia kwa ukamilifu Sheria ya Miiko ya Uongozi. Pia iharakishe hatua ya kutunga sheria itakayotenganisha mtu kuwa kiongozi wa umma na mfanyabiashara kwa wakati mmoja. Lengo ni kurejesha dhamira ya kuwa na **viongozi wanaoutumikia umma kwa maslahi ya umma** na si viongozi wanaotumia ofisi za umma kwa maslahi yao binafsi.

Kwa hiyo, katika kipindi hiki, Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali zake kutekeleza maagizo hayo ya Chama kuhusu kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Miiko ya Uongozi na kutunga sheria mpya itakayotenganisha mtu kuwa kiongozi wa umma na mfanyabiashara kwa wakati mmoja. Aidha, katika kipindi hiki, Chama Cha Mapinduzi kitaendeleza utaratibu wa kuwafuatilia na

kuwachukulia hatua viongozi wake wanaokiuka maadili ya uongozi.

(d) **Mapambano dhidi ya Rushwa**
Mkutano Mkuu wa Taifa ulilaani tabia ya baadhi ya wagombea wa uongozi kutoa rushwa nyakati za uchaguzi, na uliagiza Halmashauri Kuu ya Taifa kuchukua hatua kali dhidi ya watakaothibitika kujihusisha na tabia hii. Kwa hivyo, Chama Cha Mapinduzi kinaziagiza Kamati za Usalama na Maadili na Kamati za Siasa za kila ngazi kuwafuatilia kwa karibu wagombea uongozi katika maeneo yao ili watakaobainika kutoa rushwa wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Kanuni za Chama na Sheria za nchi.

### Kukua kwa tofauti kubwa ya kimapato katika Jamii

186. Mkutano Mkuu wa Taifa ulibainisha tatizo na hatari ya kukua kwa kasi pengo la mapato baina ya walionacho na wasio nacho, na kwamba Serikali zote mbili ziliagizwa kuchukua hatua za kurekebisha hali hii mapema kwani ikiachwa iendelee itajenga chuki na uhasama baina ya matabaka haya mawili na kuathiri amani, utulivu na umoja wa Taifa letu.

Kwa hiyo, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kuchukua hatua thabiti zenye lengo la kupunguza pengo la mapato kwa kutumia njia mbalimbali kama kuziba mianya ya wanaokwepa kulipa kodi, kuimarisha utaratibu wa Bima ya Afya ili iwafikie wananchi walio wengi na hasa wanyonge, kuongeza ajira, kuwapunguzia wananchi mzigo wa ada mbalimbali na hasa wa kipato cha chini.

### Chama Kujitegemea Kimapato

187. Uendeshaji wa shughuli za Chama hutumia gharama kubwa, hivyo moja ya vigezo vya uimara wa Chama ni kuwa na vyanzo vya mapato vinavyotosheleza mahitaji.

Kwa kuzingatia ukweli huu, katika kipindi hiki, Chama Cha Mapinduzi kinawaagiza viongozi katika ngazi zote wabuni miradi itakayokiingizia Chama mapato kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji.

Aidha, Chama Cha Mapinduzi kinasisitiza suala la ubunifu wa miradi ya kukiingizia Chama mapato; kwani zipo fursa nyingi za uanzishaji miradi na kinachohitajika ni ubunifu na uthubutu kwa kila ngazi. Kwa mfano, mikoa, wilaya, kata na matawi wanayo majengo na viwanja vyenye Hatimiliki ambazo zinaweza kutumika kama dhamana ya kupata mitaji kutoka benki ili kuanzisha miradi.

**Mafunzo kwa Makada na Viongozi wa Chama**

188. Mafunzo kwa makada na viongozi wa Chama ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa Chama na njia sahihi ya kuandaa viongozi bora. Hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM kwa kushirikiana na vyama vya kidugu itaongeza kasi ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Makada cha **Ihemi** (Iringa) na kuanzisha ujenzi wa Chuo cha **Tunguu** (Unguja) kwa lengo la kutekeleza azma hiyo.

**Jukumu la CCM**

189. CCM ina jukumu la kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Ilani hii kwa kupata taarifa za kila baada ya miezi mitatu, na pia kwa viongozi kufanya ziara za kutembelea miradi inayotekelezwa katika maeneo yao. Ili Chama Cha Mapinduzi kiendelee kukubalika na kuaminiwa na wananchi ni muhimu viongozi wake wawe karibu na wananchi kwa kuwatembelea, kusikiliza kero zao na kuzitafutia majawabu. Ni muhimu kabisa Chama Cha Mapinduzi kuendelea kuwa msemaji na mtetezi mkuu wa mwananchi na hasa wanyonge kwani kwa asili yake, CCM ni Chama Cha Wakulima na Wafanyakazi.



*Ndugu John Pombe Magufuli akiwa na Mgombea Mweza wakiwa katika ziara ya kujitambulisha kwa wanachama mara baada ya kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

**Imetolewa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM,**
**Julai 2015**